Kikao cha Tano - Tarehe 03 Oktoba, 2017

(Kikao kilianza Saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Zubeir Ali Maulid) alisoma dua

TAARIFA YA SPIKA

Waheshimiwa Wajumbe, Kanuni ya 40 (4) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi toleo la 2016 linahitaji maswali ya nyongeza yanayojibiwa kwa maandishi yawasilishwe mbele ya Baraza kupitia taarifa ya Spika.

Mwanzoni mwa mkutano huu Mhe. Ali Khamis Bakari wa Jimbo la Tumbe aliuuliza swali la nyongeza kwa Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira.

Waheshimiwa Wajumbe sasa namuomba Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira asome jibu la swali la nyongeza aliloulizwa na Mhe. Mjumbe huyu waheshimiwa nawashukuru. Mheshimiwa Waziri.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako wakati najibu swali namba 23 niliulizwa swali la nyongeza la Mhe. Ali Khamis Bakari (Doholo) aliyetaka kujua idadi ya migogoro ya ardhi iliyopatiwa ufumbuzi hadi sasa katika kujibu swali hilo napenda kujibu kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, kupitia Baraza la Ardhi lenye *Trevino* katika kipindi chza mwaka ulimalizika migogoro 241 ilipatiwa ufumbuzi ambapo ni sawa na asilimia 93 ya lengo la mwaka.

Mhe. Spika, kwa upande wa Kamisheni ya Ardhi migogoro 24 ilipatiwa ufumbuzi ikiwemo migogoro 8 inayohusiana na ardhi za eka tatu migogoro 4 ya Ardhi za Uwekelezaji na migogoro 12 kati ya 28 ya viwanja kutokana na zoezi la utambuzi lililofanywa Shehia ya Matarumbeta na Mpendae ya Wilaya ya Mjini Unguja. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Spika: **N**aomba sasa nimwite Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kuwasilisha Hotuba ya Uwasilishaji wa Ripoti ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum ya SMZ Juu ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum kwa mwaka 2016/2017.

Mhe. Spika: Ahsante Mheshimiwa sasa naomba nimwite Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji ili naye aje awazilishe hati mezani.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuweka mezani ya Taarifa ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji Kuhusu Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Ardhi na Mawasiliano ya Baraza lako Tukufu la Wawakilishi kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Mhe. Spika naomba kuwasilisha.

Mhe. Spika: Ahsante naomba sasa nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum ili aje aweke hati mezani.

Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mezani hati mezani Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum Kuhusu Ripoti ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum kwa mwaka 2016/2017, naomba kuwasilisha.

Mhe. Spika: Ahsante Mhe. Machano Othman Said sasa naomba nimwite Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi na Mawasiliano ili naye aje aweke hati mezani. *(Makofi)*

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa (Kny. Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi na Mawawiliano): Mhe. Spika, Kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi na Mawasiliano naomba kuweka hati mezani ya Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Ardhi na Mawasiliano Kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji ya Utekelezaji kwa mwaka 2016/2017, Mhe. Spika naomba kuwasilisha.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Mwanaidi swali letu la mwanzo linaulizwa na Mhe. Machano Othman Said Mwakilishi wa Wananchi Jimbo la Mfenesini

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Spika, naomba sasa nijibiwe swali langu namba 123.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 123

Fursa za Wenyeviti na Wajumbe wa Kamati Kutoa Neno Wakati wa Uzinduzi wa Miradi

Mhe. Machano Othman Said: – Aliuliza

Katika kuimarisha hadhi ya Mabunge hasa ya Jumuiya ya Madola, Serikali nyingi zimekuwa zikitoa vipaumbele vikubwa kwa kamati za kudumu za Mabunge katika kujadili bajeti ya Serikali na kupitisha sheria za nchi katika kufanikisha hilo. Serikali hizo zimekuwa zikiwaalika Wenyeviti na Wajumbe wa kamati kwenye uzinduzi wa miradi ya kisekta na safari za viongozi wa Wizara hizo ili kujenga uelewa na kuimarisha uhusiano mzuri kati ya Serikali na wananchi kupitia viongozi.

(a) Ni sababu zipi ambazo zinapelekea Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kutotoa fursa kwa Wenyeviti wa kamati kutoa neno lolote wakati wa uzinduzi wa miradi ambayo ipo chini ya Wizara ambazo zipo chini ya kamati husika.

(b) Kwani viongozi wa Wizara za Serikali hawaoni umuhimu wa kufuatana wakati wa ziara zao na Wenyeviti au Wajumbe wa kamati ndani na nje ya nchi.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais - Alijibu:

Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais naomba kumjibu Mhe. Machano Othman Said Mwakilishi wa Jimbo la Mfenesini swali lake Nam.123 lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ina mahusiano na ushirikiano mzuri wa kiutendaji na Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi, hivyo katika utekelezaji wa majukumu yake mbalimbali ya Kiwizara haijawahi kutoa zuio la fursa kwa Wenyeviti wa Kamati kushiriki katika ziara za kutembelea miradi ikiwa ni pamoja na kutoa neno wakati wa uzinduzi wa miradi mbalimbali ambayo ipo chini ya Wizara ambazo zinasimamiwa na Kamati hizo. Serikali imelipokea suala hili na itashauri Wizara na Mawaziri husika kuendelea kuwapa ushirikiano zaidi Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi na kuwapa fursa ya kushiriki pale wanapofanya ziara ya kutembelea au kuzindua miradi iliyopo chini ya Kamati hizo.

(b) Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na viongozi wa Wizara za serikali inapenda sana kufuatana na Wenyeviti au Wajumbe wa Kamati wakati wa ziara zao za ndani na nje ya nchi wakati wa utekelezaji wa majukumu ya Wizara yanayosimamiwa na Kamati hizo. Changamoto inayojitokeza ni mwingiliano wa ratiba za kazi za Serikali na Baraza la Wawakilishi wakati wa utekelezaji wa majukumu yao mbalimbali ya usimamizi na ufuatiliaji, nakushukuru Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Mhe. Machano Othman Said swali la nyongeza

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Spika, namkushukuru Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake lakini pamoja na majibu hayo naomba niuulize swali moja lenye kifungu (a) na (b) kama ifutavyo.

(a) Katika majibu mama Mhe. Waziri anasema watazishauri Wizara za Serikali mimi nilifikiria wataziagiza lakini hapa wanasema watazishauri kwamba wanaweza kuzikubali au kukataa na haoni kwamba huu utaratibu tunaoufanya sasa hivi hauleti afya njema kwa Baraza lakini kwa Serikali kwa ujumla.

(b) Katika jibu (b) Mhe. Waziri amesema kwamba hapatani na Waheshimiwa Wawakilishi kwa sababu ya Ratiba ya Baraza na Serikali zimeingiliana lakini najua mpaka sasa hivi Baraza tunaendelea wako Wawakilishi wana safari ya China na kwengine. Jee haoni kwamba Serikali haijawa tayari kuwachukua na ni mwaka gani wa mwisho kwa Viongozi wa nchi hii kuwachukua Wawakilishi kama utaratibu wa zamani ulivyokuwa.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri majibu

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa Niaba ya Makamo wa Pili wa Rais naomba kumjibu Mhe. Machano Othman Saidi swali lake la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

(a) Mhe. Spika, kama ambavyo nimejibu jibu langu la msingi Serikali inashauri lakini tunathamini sana jitihada, busara za viongozi wetu wakuu Mhe. Rais na Mhe. Makamo wa Pili wa Rais, bahati nzuri viongozi wetu hawa wana busara za hali ya juu ushauri wa kiongozi ni agizo la utekelezaji katika ngazi za chini. Haina maana kwamba litoke agizo la mojamoja lakini kiongozi mkubwa wa nchi anaposhauri ina maana jambo lile, ushauri ule linatakiwa liende kwenye utekelezaji wa moja kwa moja.

Kama ambavyo tumesema wakati mwengine mambo haya yote ambayo katika kanuni na busara inahitajika sana busara ya hali ya juu, heshima ya hali ya juu katika kuhakikisha watu hawa wa aina hizi tunaweza kupata mashirikiano ya kutosha.

(b) Lile la mwingiliano wa rasimu Mheshimiwa ameuliziwa mara ya mwisho lini Wizara imekuwa ikishirikiana au ikiwachukuwa baadhi ya wajumbe katika safari zao. Lakini hili tunalisema kwamba bahati nzuri baadhi ya Wizara zimekuwa zikijitahidi sana katika kulifanyia utekelezaji wa jambo hilo.

Mimi nakumbuka wakati ilipokuja ndege ya kufanya upembuzi yakinifu kuhusiana na maswali ya gesi na mafuta. Mhe. Mwenyekiti wa Kamati na Kamati yake walikuwepo pale *Airport* walishirishwa vya kutosha.

Lakini pia nakumbuka hata Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais imekuwa na mashirikiano ya karibu sana na Mwenyekiti hata katika baadhi ya warsha ambazo zimekuwa zikifanyika nje ya visiwa vyetu hivi, walikuwa wakipata fursa kwa namna moja ama nyengine sasa ni jambo ambalo mawaziri kwa ujumla na Wizara na watendaji wengine kuona jambo la busara kuwashirikisha wenyeviti wetu pale ambalo kumetokea mahitaji ya kufanya hivyo, nashukuru Mheshimiwa.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais majibu ya ziada.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, nakushukuru lakini naomba kwanza nimpongeza sana Mhe. Naibu Waziri kwa kujibu maswali kwa

ufasaha mkubwa na imeonesha katika kipindi kifupi uwezo wake mkubwa katika kutenda kazi.

Mheshimiwa baada ya maelezo hayo naomba na mimi niongezea jibu la nyongeza linalohusu Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kuchukuliwa katika ziara mbali mbali nje ya nchi.

Ni kweli utaratibu huo unakuwepo na unaendelea kuwepo inategemea zaidi na uwezo wa Serikali katika kufanya mambo yake mbali mbali, nataka niwahikishe wajumbe wa Baraza letu Tukufu Serikali siku zote inajali mchango mkubwa unaotolewa na wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tutaendelea kushirikiana nao katika ziara zetu za ndani na nje kadiri ya uwezo wa Serikali utakavyo ruhusu lakini nia na dhamira ni kuhakikisha kwamba tunaimarisha mashirikiano na kufanya kazi kwa pamoja.

Na napenda nitowe wito kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi pale wanaposikia Viongozi mbali mbali wana ziara ya kutembelea maeneo mbali mbali katika miradi ya maendeleo ni vizuri sana kushirikiana hususan Mwakilishi wa Jimbo hili na sisi katika Serikali tutachukuwa kila jitihada kuwa tunawaarifu kwa wakati waheshimiwa wajumbe hususan wale ambao maeneo yao majimbo yao yatakuwa yanatembelewa na Viongozi ili waweze kushiriki kwa ukamilifu. Dhamira yetu ni kufanya kazi kwa pamoja bila ya kufanya kazi kwa pamoja kati yetu Serikali na Baraza hili Tukufu mafanikio yetu yanaweza kuwa sio yale ambayo wananchi wanatarajia kwa hiyo, nawahakikishia kwamba uhusiano upo na utaendelea kuwepo wakati wowote ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Mhe. Amina Iddi nilikuona kwa swali la nyongeza.

Mhe. Amina Iddi Mabrouk: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza lakini Mhe. Spika kabla sijauliza swali la nyongeza naomba nichukuwe nafasi hii kukupongeza kwa dhati kwa namna ya kiti chako kilivyopendeza kwa kuzungukwa na Makatibu Mezeni Kinamama Mhe. Spika, kina mama tunaweza bila ya kuwezeshwa. *(Makofi)*

Baada ya pongezi hizo Mhe. Spika naomba kumuuliza Mhe. Waziri swali langu la nyongeza. Mhe, Spika, pamoja na majibu mazuri anotujibu Mhe. Waziri majibu ambayo yana uweledi mkubwa lakini pamoja na hivyo naomba nimuulize swali, kwa kuwa kuna umuhimu mkubwa sana Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kufuatana na Viongozi wakati wa ziara zao za ndani na za nje ya nchi jee Mhe. Waziri ni lini basi wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wataanza kufuatana na Viongozi wa Serikali naomba utuambie kwa sababu umeleza majibu mengi lakini bado hujawahakikishia wajumbe wa Baraza kwamba lini utaratibu huu utaanza.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais mwenyewe majibu.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, naomba kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Makamo wa Pili wa Rais kujibu swali la nyongeza la Mhe. Amina kama ifuatavyo.

Kwanza nataka nikubaliane naye kwamba ni kweli meza yako imependeza kwa kuwa na Makatibu Mezani kinamama na huo ni mfano mzuri kuonesha kwamba kina mama wanaweza na bila ya kuwezesha wanaweza Mhe. Spika.

Mheshimiwa kusema ni lini waheshima wajumbe watashirikishwa kwenye ziara itakuwa ni ngumu lakini kulingana na hali ya uwezo na ziara zitakavyojitokeza nitajihidi pale ambalo uhitaji wa kufanya hivyo unapojiotokeza tutafanya hivyo nataka nimuhakikishe Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwamba dhamira ya Serikali ni kuiweza kuwashirikisha wajumbe katika kila hatua na kila shughuli za kimaendeleo ya nchi yetu.

Lakini lazima tukubali uwezo wetu ndani ya Serikali bado haujakuwa mkubwa sana wa kufanya yele yote ambayo tunataka tuyafanye na ndio maana Serikali inachukuwa jitihada kubwa katika suala zima la kuimarisha uchumi ili kuongeza mapato ili mapato haya tutayopata yaweze kutowa huduma bora kwa wananchi ikiwemo kuwapa fursa mbali mbali Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ili waweze kujifunza na kuelewa zaidi kwa kuona maendeleo ndani na nje ya nchi yetu.

Mhe. Spika, naomba Waheshimiwa Wajumbe wavute subira na pale hali itakapokuwa nzuri tutawashirikisha katika ziara zetu za Kiserikali. Ahsante sana.

Mhe. Spika: Swali linaulizwa na Mhe. Omar Seif Abeid Mwakilishi wa Wananchi Jimbo la Konde.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali lakini nilikuwa na nia na nina nia ya kuliondoa swali hili kwa sababu moja wakati jana nikichangia kwenye hotuba ya Kamati ya Sheria, katiba na Utumishi wa Umma swali hili niliwahi kulilizungumza na lilipatiwa majibu ya undani kwa hivyo kutoka na hiyo nimeona kwamba sitakuwa na sababu ya kuendelea na hili swali, ahsante sana Mheshimiwa.

Nam. 48

Ukiukwaji wa Nidhamu za Kazi kwa Baadhi ya Watumishi wa Umma

(Mhe. Mjumbe aliyetaka kuuliza swali hili ameliondoa)

Mhe. Spika: Ahsante swali liemeondolewa.

Mhe. Spika: Swali linaulizwa na Mhe. Suleiman Sarahan Said Mwakilishi wa Wananchi Jimbo la Chake chake

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nashukuru Mhe. Spika awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa utujaalia na uzima wake huu kutuamisha salama la kutuleta hapa na Mwenyezi Mungu atujaalie turudi majumbani salama usalimini.

Mhe. Spika, naomba swali langu nambari 19 lijibiwe

Nam. 19

Usafi wa Mazingira Maeneo ya Kazi na Biashara

Mhe. Suleiman Sarahan Said – Aliuliza:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inastahili pongezi kwa kuwapa wananchi elimu ya usafi wa mazingira. Hata hivyo, bado inaonekana kuwa uelewa wa suala hilo ni mdogo kwani wananchi wengi wanashindwa kusafisha hata kwenye maeneo ya nyumba zao na kuona kama ni kazi ya Manispaa pekee.

a) Je, suala la mtu kusafisha eneo la nyumba yake ni kazi ya nani kisheria.

b) Kama ni kazi ya mwenye eneo la nyumba ni adhabu gani anapewa kama hakufanya usafi.

c) Ni lini Serikali mara ya mwisho imetoa tangazo la usafi na kuweka tarehe ya mwisho ya tangazo hilo na ni adhabu gani mtu atachukuliwa kwa kutokutii amri hiyo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Suleiman Sarahani Said Mwakilishi wa Wananchi Jimbo la Chake Chake swali lake Nam. 19 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

a) Kwa mujibu wa Kifungu cha 3 cha Kanuni ya Huduma zinazotolewa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ya mwaka 2016, suala la kuhakikisha kuwa nyumba ya kuishi inakuwa katika mazingira safi ni jukumu la mmiliki au mtu anayeishi katika nyumba hiyo. Mmiliki au mpangaji wa nyumba hiyo anatakiwa kisheria kukusanya taka hizo na kuziweka katika chombo maalum cha kuhifadhia taka ili ziweze kuchukuliwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa ajili ya kutupwa katika maeneo rasmi yaliotengwa kwa ajili ya utupaji wa taka.

(b) Mhe. Spika, kwa mujibu Kifungu cha 3(5) cha Kanuni niliyoitaja katika sehemu (a) ya jibu la swali hili, adhabu ya mmiliki au mkaazi wa nyumba ambaye atashindwa kusafisha eneo la nyumba anayoishi ni kutozwa faini ya shilingi hamsini elfu (50,000/-) kwa kosa la kwanza na shilingi laki moja (100,000/-) kwa kosa la pili au kifungo cha wiki mbili au adhabu zote mbili kwa pamoja.

(c) Mhe. Spika, kupitia vyombo mbali mbali vya habari hususan redio na televisheni, Mabaraza ya Manispaa yamekuwa yakielimisha na kuhamasisha jamii kuhimiza masuala ya usafi na utunzaji wa mazingira. Aidha, Mabaraza ya Manispaa yamekuwa yakishiriki katika kampeni za usafi wa mazingira kwa kushirikiana na taasisi mbali mbali.

Mhe. Spika, serikali kupitia Mamlaka za Serikali za Mitaa haijawahi kutoa tangazo la usafi na kuweka tarehe ya mwisho ya tangazo hilo kabla ya kuchukua hatua ya kutoa adhabu kwa wasiotii sheria. Hata hivyo, kwa kuwa sasa tayari Kanuni mpya zimeshachapishwa katika Gazeti Rasmi la Serikali, matayarisho ya kutoa matangazo na elimu kwa umma kuhusu usafi na utunzaji wa mazingira kwa mujibu wa Kanuni na adhabu itatolewa kwa watakaokwenda kinyume na matangazo hayo. Ahsante.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: (a) Nashukuru Mhe. Spika, na mimi nimshukuru sana Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri lakini kwa kuwa zamani tulikuwa na utaratibu wa bwana afya kupita majumbani na kukagua mazingira yote pamoja na choo ambacho kwa kweli ndio sababu kubwa inayosababisha mambo ya kipindupindu na suala lile tumeliacha. Sasa haionekani umuhimu wa kurudia ili kukagua sehemu za nje na ndani ili kuweza kutatua matatizo ambayo yanajitokeza kabla ya dharura hiyo.

b) Kwa kuwa tunajua umuhimu wa masuala ya usafi, kuna baadhi ya watu ambao wanatumia kitoweleo cha nyama kama ng'ombe akiwa mkubwa humburuza na watu wa usafi wanamuona kama yule ng'ombe anaburutwa akiwa ameshachunwa kabisa nyama ile, lakini anaachiwa na kulitundika na watu kwenda kumla tena ukiwauliza wanasema kwamba ataenda kupikwa, lakini wengine inakuwa ni mishikaki ya kuchoma. Haoni umuhimu wa kuweza kuwapa elimu zaidi watu hawa ambao wanatumia utaratibu huu ili kusababisha baadhi ya maradhi.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye (a) na (b).

Nataka nikubaliane nae kwamba utaratibu uliokuwepo zamani na hata hivi sasa ni mabwana afya kukagua nyumba pamoja na vyoo na maeneo mengine ya usafi. Na hili jambo nataka nilithibitishie Baraza kwamba kwa utaratibu huu wa ugatuzi wa madaraka mabwana afya na mabibi afya watakuwa rasmi chini ya vyombo vya Serikali za Mitaa badala kuwa wanasimamiwa na Wizara ya Afya yenyewe. Kwa msingi huo Halmashauri na Mabaraza ya Manispaa na Mabaraza ya Miji yatakuwa yamepata watumishi wa kutosha katika kufanya kazi hizi za ukaguzi na kuwachukulia hatua wale ambao watakuwa wanakwenda kinyume na taratibu ya sheria yetu Nam.7 na Kanuni yetu ya huduma za Mabaraza kwa mujibu wa kifungu cha 94. Kwa hiyo, utaratibu huu utaanza hivi karibuni kwa ajili ya kufanya kazi hizi za kuhakikisha kwamba maeneo yote yanakuwa safi.

Mhe. Spika, kuhusu suala la kuburuzwa kwa nyama ya ng'ombe. Nadhani si sahihi kabisa kwa wanaofanya hivi kufanya kazi hiyo ya kuburuza nyama ya ng'ombe ambayo ni chakula kinacholiwa na binadamu. Kanuni ambayo nimeitaja kwa mujibu wa kifungu Nam.99 imeweka adhabu kwa watu ambao watakuwa wanafanya utaratibu huo kinyume na sheria na hatua kali zitachukuliwa kwa wale ambao watafanya hivyo. Hata hivyo, kama nilivyokuwa nikijibu swali mama ni kwamba ofisi yangu kwa kushirikiana na Mabaraza na Halmashauri itatoa elimu ya kutosha juu ya kanuni mpya ambazo tumezitunga ili tutakapochukua hatua tusije sasa serikali tukapata malalamiko kwamba

tunawachukulia hatua, kwa sababu kanuni zenyewe zimeweka adhabu na adhabu zenyewe ni kubwa. Kwa hiyo, niwaombe Waheshimiwa Wawakilishi pamoja na sisi kutoa taaluma lakini na sisi pia tuwe mabalozi katika kuwaelimisha wananchi ambao tunawaongoza. Ahsante.

Mhe. Viwe Khamis Abdalla: Ahsante Mhe. Spika, na mimi asubuhi hii ya leo kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Nataka nichukue nafasi hii nimpongeze Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri.

a) Mhe. Spika, kwa kuwa nchi za wenzetu wana maeneo maalum ya utupaji wa taka, lakini hapa kwetu Zanzibar kuna baadhi ya Halmashauri wanakuwa wanatupa taka katika maeneo ambayo wanaishi wananchi na kusababisha uchafu mkubwa katika maeneo hayo. Je, Mhe. Waziri wizara yako wanalijua hilo na kama mnalijua wizara yako ina mpango gani wa kuondosha majaa katika maeneo ambayo wanaishi wananchi hawa ili usije ukatokea mripuko wa maradhi ya kipindupindu.

b) Mhe. Waziri wizara yako ina adhabu gani katika Halmashauri hizo ambazo zinatupa taka katika maeneo ambayo kuwa wanaishi wananchi wetu. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye vifungu (a) na (b).

a) Mhe. Spika, ofisi yangu inalielewa suala hili hasa baada ya Mhe. Mwakilishi aliyeuliza swali jana kunipa kadhia hii na tayari kwa mujibu wa taarifa yake nimeshamuarifu Mkurugenzi anayehusika na jambo hili na hatua zitachukuliwa mara moja kutokana na kadhia ambayo ameisema.

b) Tunajipangaje ndio maana nimesema tumetengeneza kanuni za huduma ili kukabiliana na changamoto hizi zinazotokea, kwa sababu serikali hatupendelei kutokea maradhi ya mripuko kila wakati. Lakini kwa hivi sasa serikali imeweka eneo la Kibele kuwa ni eneo mahsusi kwa hapa Unguja kwa ajili ya kutupia taka. Sasa zile taasisi zote ambazo zinafanya hivyo kama nilivyosema katika jibu la (a) kwamba taasisi inayohusika nimeshakaa nao na hatua zitaanza kuchukuliwa na kurekebishwa mara moja. Ahsante sana.

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri sana, sana lakini mbali na majibu mazuri hayo nichukue fursa hii pia kuvipongeza vikundi vya usafi katika Jimbo la Kikwajuni pamoja na Jimbo la Malindi kwa Madiwani wetu na Wawakilishi wa Majimbo hayo mawili kuunda vikundi vya usafi katika majimbo haya. Ili katika kuendeleza usafi katika majimbo yetu na Mji wetu wa Zanzibar je serikali kupitia Baraza la Manispaa haioni kwamba ipo haja kwa kushirikiana na vikundi hivi viwili vya Jimbo la Kikwajuni na Jimbo la Malindi kuandaa siku ya usafi ya mwisho wa mwezi kwa kufanya usafi katika maeneo ya Mjini hususan katika maduka kwa kushirikiana na wenye maduka katika Mji wetu wa Zanzibar.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kujibu swali la nyongeza la Mhe. Mwakilishi. Kwanza nazipokea pongezi kwa niaba ya watumishi wote wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ hususan kwa Taasisi za Serikali za Mitaa, na mimi nimuombe anifikishie salamu kwa wana vikundi wa Jimbo la Malindi, Jimbo la Kikwajuni lakini na majimbo mengine yote pamoja na zile taasisi kama G1 na nyenginezo.

Mhe. Spika, serikali inayo tarehe ya usafi kwa wote kama vile tulivyofanya kwa kushirikiana na G1 katika kufanya suala hili la usafi. Kwa hiyo, ni vyema niwahimize wale wote wenye vikundi vya usafi, vikundi vya michezo na kuwaahidi kwamba serikali itaendelea kushirikiana nao ili kuhakikisha suala hili la usafi linakuwa ni suala la watu wote na silo la Mamlaka za Serikali za Mitaa peke yao. Kwa hiyo, ushauri wako tunauchukua na hivi sasa ndivyo tunavyofanya kazi. Ahsante sana.

Nam. 25

Usafi wa Masoko katika Maeneo ya Mitaro ya Maji

Mhe. Suleiman Sarahan Said – Aliuliza:

Pamoja na jitihada za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar za kuifanya miji yetu kuwa safi, bado suala la usafi hasa eneo la masoko ya kuuzia nyama, samaki sehemu za matunda na sehemu za nje ya masoko imekuwa na changamoto kubwa hasa katika mitaro ya maji machafu na mifereji ya maji safi.

(a) Je, serikali inalijua hilo.

(b) Masoko yetu yanajengwa vipi bila ya miundombinu mizuri ya usafi.

(c) Kama miundombinu sio mizuri ni lini tutaipanga iwe mizuri ikiwemo suala la usafi wa masoko hayo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 25 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ inaelewa umuhimu wa usafi katika masoko ya kuuzia nyama ya ng'ombe, mbuzi, samaki na matunda katika masoko yanayoendeshwa na kusimamiwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuimarisha afya za wananchi wetu.

(b) Mhe. Spika, ni kweli kuwa baadhi ya masoko yetu hasa yale yaliyojengwa kabla ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar ya mwaka 1964 kama masoko ya Darajani

kwa hapa Unguja na Chake-Chake kwa Pemba yamekuwa yakikabiliwa na changamoto zinazohusiana na masuala ya misingi ya maji machafu na mifereji ya maji safi. Hali hii imesababishwa na ongezeko la idadi ya watu wanaohitaji huduma pamoja na ongezeko la wafanyabiashara katika masoko hayo. Ongezeko hilo la watu linasababisha miundombinu iliopo kutokukidhi mahitaji ya sasa katika masoko hayo.

(c) Mhe. Spika, katika kukabiliana na changamoto hizo, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kupitia Mamlaka za Serikali za Mitaa inachukua hatua zifuatazo:-

(i) Katika mwaka wa fedha 2017/2018 Baraza la Manispaa – Mjini limetenga jumla ya shilingi milioni 32 kwa ajili ya matengenezo ya Soko la Darajani katika vibaraza vya kuuzia samaki na nyama ya ng'ombe na mbuzi na kufanya matengenezo katika sakafu, misingi ya maji machafu na mifereji ya maji safi katika soko hilo; na

(ii) Kuhakikisha kuwa suala la kuwepo kwa misingi ya maji machafu na mifereji ya maji safi katika masoko yote mapya yanayoendelea kujengwa hivi sasa linazingatiwa kama linavyooneka katika ujenzi wa masoko ya Kinyasini - Kaskazini "A" Unguja, Tibirinzi – Chake-Chake na Konde - Micheweni Pemba.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nashukuru Mhe. Spika, na mimi nimshukuru Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri sana, na vile vile nimpongeze kwa kunijengea soko zuri la kisasa la Tibirinzi na pia kuniahidi mwaka huu atanijengea barabara yangu ya Msingini, namshukuru sana Mhe. Waziri.

a) Lakini kidogo niongeze swali la nyongeza Mhe. Spika kuna tuhuma au kuna maelekezo ya kwamba katika Soko la Mwanakwerekwe sehemu za kuuzia nyama hakuna misingi mizuri wakati wa kukosha hakuna misingi mizuri ya kutokea maji au maeneo ya kutokea maji. Sijui suala hili ni kweli au si kweli, lakini kama ni kweli nafikiri bora ungelichukua kuliangalia lakini utajibu mwenyewe kama ni kweli au si kweli usafi baada ya kuuza nyama katika Soko la Mwanakwerekwe.

b) Nikushukuru sana katika kujenga soko zuri la kisasa la Pemba, lakini sijui kwa sababu sijaona sehemu ya vyoo na bado Chake-Chake ina matatizo ya vyoo vya mji. Sasa swali langu ni kwamba je ni utafanya utaratibu wa kujenga vyoo ambavyo vitakuwa vya mji na kama sio hivyo je kuna nafasi ya mtu binafsi kujenga akaweza kutumia yeye kama biashara fulani.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza. Katika Soko la Mwanakwerekwe iko misingi katika maeneo ya kuuzia nyama ya ng'ombe na mbuzi ambayo inatakiwa iende katika mashimo maalum ambayo yanahifadhia maji hayo. Hata hivyo, kutokana na sababu nilizozieleza katika jibu mama kwamba ongezeko la idadi kubwa ya wafanyabiashara kinyume na mpango mzima wa

matumizi ya soko lile unasababishwa msongamano na hivyo matumizi kuwa makubwa zaidi ya kupokea taka na uwezo wa ile misingi ya kupokea maji taka au maji machafu imekuwa ni mdogo kuliko uwezo wake. Hivyo, Baraza la Manispaa litafanya mapitio upya ya misingi hii ili kukidhi mahitaji yaliyopo hivi sasa, lakini vile vile tutahakikisha kwamba ile miundombinu iliyopo ya wale waliotakiwa kuuza biashara hiyo ambayo nimeisema na wewe umeitaja wanakuwa wale waliopangwa na sio kuvuka idadi ya watu kuliko wale waliopangwa.

Mhe. Spika, kuhusu Soko la Chake-Chake Tibirinzi kwanza nataka nimpongeze sana Mhe. Mwakilishi kwa mashirikiano yake mazuri na ufatiliaji katika kuhakikisha kwamba Mji wa Chake-Chake unakuwa kweli ni mji mkuu kwa Pemba. Suala la ujenzi wa vyoo ndani ya soko vitakuwepo vyoo tena vya kisasa ambavyo vitakidhi haja ya watumiaji au wafanyabiashara na wale watakaokwenda kutafuta mahitaji pale sokoni.

Mhe. Spika, lakini kuhusu watu ambao wanataka kushirikiana na Baraza la Mji Chake-Chake kujenga vyoo tunawakaribisha kama wewe unao walete tutashirikiana nao, tutakubaliana nao ili waweze kufanya hiyo huduma ambayo ni muhimu kwa maslahi ya wananchi wetu.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Nashukuru na mimi kwa kuniona nataka nimuulize Mhe. Waziri maswali madogo sana ya nyongeza yenye kifungu (a) na (b).

a) Mhe. Waziri kwa muda mrefu soko kuu la Marikiti ambalo linaingiza fedha nyingi naamini katika masoko yote lile linaongoza na imekuwa historia kwa kisiwa chetu cha Zanzibar pamoja na watalii. Mhe. Spika, soko lile nafikiri halijafanyiwa marekebisho muda mrefu na mwenyewe unakumbuka uzuri suala hili tokea kipindi cha Baraza lilopita pana shimo pale kwenye mnada karo ndogo tu ambapo haifiki laki saba mpaka nane kuendea kwa Shamsu, kadhia ile umenipa Mkurugenzi sasa hivi ameshakuwa Mkuu wa Wilaya lakini mpaka leo gari mle kwenda ni shilingi elfu mbili. Ni lini serikali itaenda kuangalia hatuataenda kuangalia hatua ile na lini tutafanya ziara mimi na yeye hasa ili akajionee hali ile ilivyo. Ni hatari huku tunakusanya shilingi 2,000 kutengeneza tunashindwa ni lini tutakwenda mimi na yeye tukaione *physical*. Hilo la mwanzo.

La pili, hebu wale wafanyabiashara wanaofanya biashara usiku pale marikiti, kwanza niipongeze serikali kwa kuwajali wananchi wale, lakini huwa wanachangishwa shilingi 2,000. Hivi juzi kama leo ya nne au ya tano pana taka zilikaa pale mpaka asubuhi hazijaondoshwa ule ndio uhalali kweli?

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba nimjibu Mhe. Jaku Hashim swali lake la nyongeza lenye a na b kama hivi ifuatavyo:

Ni kweli Mhe. Spika, Mhe. Jaku Hashim amekuwa akiliulizia suala hili la shimo liliopo njiani karibu na eneo linalopigwa mnada wa samaki. Shimo hili Baraza la Manispaa wamekuwa wakilitengeneza mara kwa mara. Hata hivyo, kama nilivyosema kwenye jibu mama katika marekebisho makubwa ambayo yatafanywa kwenye soko hili la Darajani

kwa kuuona umuhimu ule ule ambao ameusema Mhe. Jaku tunategemea safari hii tutaweka mfuniko ambao hata ikipita gari, au ukipita mkokoteni liwe haliwezi kuvunjika. Kwa hiyo, *concern* yake Mhe. Jaku tunaithamini na tutahakikisha hilo jambo linafanyika katika mpango huu wa bajeti ambayo imepangwa mwaka huu 2017/2018.

Kuhusu suala la taka kukaa siku tatu. Sina taarifa hiyo, lakini kama hilo limetokea wahusika wapo juu pale wananisikia na yeye wamemsikia watachukua hatua zinazofaa. Mana hatuwezi sisi kuweka kanuni za kusimamia usafi na kutoa adhabu lakini sisi wenyewe tukawa hatutekelezi wajibu wetu. Kwa hiyo, kupitia Baraza hili namuagiza Mkurugenzi wa Baraza la Manispaa ahakikishe kwamba kama hilo jambo limetokea halitokei tena. Ahsante sana.

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Spika, ahsante nakushukuru sana kwa kuniona na mimi pia. Katika mchango wangu wa Mkutano wa Bajeti ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar nilichangia kwa upanda sana juu ya umuhimu wa kujengwa soko la Kaebona na nimshukuru sana Mhe. Waziri aliliona hilo ili katika kusogeza huduma za mahitaji kwa wananchi Mkoa wa Kusini hasa katika maeneo husika katika vijiji vya Unguja Ukuu Kaebona, Tindini, Kisiwa cha Uzi, Kikungwi pamoja na barabara mpya inayotoka kutoka Jendele kuja mpaka Unguja Ukuu Kaebona. Swali langu liko hapa.

Je. hadi hivi sasa Mhe. Waziri ameanza utaratibu gani wa mazungumzo pamoja na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hasa waziri husika ambaye ni wa ulinzi ili tuweze kuangalia utaratibu mzima wa kuweza kutusaidia lile eneo kwa ajili ya kujenga hili soko.

Pia Mhe. Spika, nikiwa kama Mwakilishi wa Wananchi Jimbo la Tunguu nimeanza hatua za awali za kupatikana mchoro ambao ni mapendekezo na nimshukuru sana Bi Fatma Kara ambaye ni mchoraji maarufu Mzanzibari mzalendo ambaye ananisaidia. Je waziri atakuwa tayari kuunda kamati ya wataalamu ili iweze kunisaidia mimi pamoja na wananchi wa eneo husika tuweze kuanza utaratibu wa awali na kuja mapendekezo katika ofisi yake pamoja na Baraza la Mapinduzi ili kuanza utaratibu wa ujengaji wa soko hili. Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Simai Mohammed Said (Mpakabasi) swali lake lenye kipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:

Ni kweli kwenye Mkutano wa Bajeti Mhe. Mwakilishi aliwasilisha hoja hii na majibu yake yalikuwa *very straight forward* na *very clear* na leo nataka nirejee hapa kwamba, Mwakilishi yoyote na Madiwani wanayo haki ya kuibua mradi kuhusu maendeleo ya wananchi katika jimbo lao. Mimi nikasema, wazo hili ni zuri lakini inafaa wazo hili lipelekwe katika ngazi ya Halmashauri ya Wilaya na hatimaye lijadiliwe katika Kamati ya Maendeleo ya Mkoa kwa mujibu wa sheria yetu Nam. 7 ya mwaka 2014 na sheria Nam. 8 ya mwaka 2014 ya Tawala za Mikoa na Waheshimiwa Wawakilishi wote ni wajumbe. Jambo hili likipelekwa kwa sababu utaratibu wetu wa ugatuzi kwamba mambo ya maendeleo sasa yanaanzia chini huko yanakuja huku juu. Ni imani yangu kwamba

hatua hiyo atakuwa ameifanya vizuri kwa sababu tayari halmashauri na mkoa wanalo wazo hili kwa ajili ya kulifanyia kazi.

Mhe. Spika, lakini suala la kuzungumza na Waziri wa Ulinzi kuhusu pahala pa kujenga soko hili nadhani suala la ardhi halina tabu. Kwa hiyo, kwa sababu suala la ardhi ni suala si la Muungano ni pahala pa kujenga soko hili katika eneo lote lile ambalo limependekezwa patapatikana hata kama patakuwa sio pale katika uwanja ule wa mazoezi ya Kijeshi.

Mhe. Spika, nichukue nafasi hii kujibu swali (b) kumpongeza katika hatua hizo ambazo amezifanya. Nadhani hakuna haja ya kuunda timu, timu ni Mkurugenzi wangu wa Baraza la Manispaa pamoja na sekreterieti ya mkoa wakishirikiana na yeye wanatosha kabisa katika kuibua mradi huu na kuuleta serikalini ili uweze kuchukuliwa hatua zinazofaa. Mhe. Spika, ahsante sana.

Nam. 81

Mkataba wa Ujenzi wa Jengo la Hoteli ya Bwawani

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:

Kwa muda mrefu sasa jengo la Hoteli ya Bwawani limekuwa katika matengenezo ambayo hayaonekani maendeleo yake. Hoteli hiyo ilivunjwa wakati ikiwa inazalisha fedha kutokana na shughuli mbali mbali zilizokuwa zikifanyika ndani ya hoteli hiyo.

Je, ni lini serikali italeta mkataba wa ujenzi wa Hoteli ya Bwawani ili kujua maendeleo ya ujenzi na wananchi kujuwa kiasi gani cha fedha kinapotea.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango - Alijibu:

Mhe. Spika, naomba uniruhusu kujibu swali Nam. 81 lililoulizwa na Mhe. Jaku Hashim Ayoub. Kabla ya kujibu swali hilo naomba kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, ni kweli kwamba tarehe 17 Novemba, 2015, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ililikodisha Hoteli ya Bwawani kwa Kampuni ya *QUALITY GROUP* ya Dar es Salaam. Hata hivyo, sio sahihi kwamba hoteli hiyo imevunjwa, kilichofanyika ni kuanzwa hatua za ukarabati uliokusudia kuigeuza hoteli hiyo kuwa yenye hadhi ya nyota tano. Hata hivyo, utekelezaji wa mkataba wa ukodishaji huo umekumbana na changamoto mbali mbali na kusababisha kuchelewa kwa mradi huo.

Mhe. Spika, miongoni mwa changamoto hizo ni kutokamilika kwa wakati kwa tathmini ya athari ya mazingira na athari ya mradi huo katika urithi wa Mji Mkongwe. Tathmini hizo zinapaswa kufanywa na Mwekezaji kwa muongozo wa mamlaka husika na kuchelewa kwake kunazuia uendelezaji wa uwekezaji huo. Serikali inaendelea na juhudi za kumharakisha muwekezaji kukamilisha matakwa hayo muhimu ya uwekezaji katika maeneo ya Mji Mkongwe ili tija iliyokusudiwa iweze kupatikana.

Mhe. Spika, kwa upande mwengine, wakati ukodishaji huo ukifanyika, sehemu kubwa ya Hoteli ya Bwawani tayari ilishasita kutoa huduma kutokana na uchakavu wake. Hivyo, kwa wakati huo haikuwa ikichangia kwa kiasi kikubwa katika mapato ya serikali.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kukumbusha kuwa hatuna utaratibu wa kuleta mikataba hapa Barazani na pia kuleta mikataba hiyo hapa Barazani hauwezi kusaidia kupatikana taarifa ya maendeleo ya ujenzi kwa wananchi. Taarifa hizo zitawafikia wananchi kwa njia nyengine ikiwemo taarifa maalum zinazoweza kutolewa na serikali na taasisi zake katika muda unaohusika.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsane sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kumuuliza swali dogo la nyongeza lenye kifungu (a) na (b).

(a) Kwa nini tathmini ya mradi haikufanyika mwanzo kabla ya hoteli kuvunjwa na kusababisha hasara katika mradi huo na kipi kinachokuja mwanzo kati ya mchoro na ramani.

(b) Baraza la Wawakilishi ni chombo cha wananchi ambacho kipo kisheria na kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ukurasa wa 60 ibara ya 38 Baraza la Wawakilishi ni pamoja na kuongoza shughuli zake kutokana na vifungu vya katiba hii itafanya kazi kwa mambo yafuatayo ya utekelezaji, kutunga sheria pale ambapo utekelezaji wa jambo unahitajika kuwepo kisheria (a), (b) kujadili shughuli za wizara wakati wa kikao cha mwaka na bajeti ya wawakilishi, (c) kuuliza maswali mbali mbali kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Baraza la Wawakilishi. Hoja yangu iko hapo katika (c).

Ni sababu gani ili wawakilishi au waheshimiwa wapate kujua na wananchi kupitia chombo hikiukizingatia tupo kisheria.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Kwanza kama nilivyosema kwamba mkataba umetiwa baina ya *Quality Group* na serikali kwa ajili ya ukarabati wa jengo lile la Hoteli ya Bwawani. Michoro imekamilika kwa sababu hiyo ilikuwa ni kazi ya mkodishwaji mwenyewe, lakini moja ya masharti aliyotakiwa kufanya kwanza ni kufanya tathmini ya athari ya kimazingira. Hapa niseme tu, hivi karibuni tathmini hiyo ya athari ya kimazingira imekamilika, kilichobakia hivi sasa ni athari ya urithi wa Mji Mkongwe kwa maana ya *Heritage impact assessment*. Hiyo haijakamilika na kama ulivyo utaratibu wetu kwa miradi ambayo inatekelezwa ndani ya eneo la Mji Mkongwe ni lazima vipatikane vibali kutoka *UNESCO*, *permit* ipatikane ili iweze kutengenezwa kwa majengo yaliyoko ndani ya urithi wa Mji Mkongwe.

Sasa kwa sababu haya hayajakamilika na vibali havijapatikana ndio suala ambalo limecheleweshe utekelezwaji wa mradi ule, lakini niendelee kusema kwamba hivi sasa timu ya *UNESCO* iko hapa ya watu wawili na wao pia walisema kwamba watakapokuja nchini watajaribu kuhakikisha miradi yote inayotaka kutekelezwa na serikali katika eneo la Mji Mkongwe basi waikague kwa wakati huo watakapokuwepo nchini ili yote iweze kupata kibali kwa pamoja. Nasema hilo kwamba tayari wameshafanya ziara katika taasisi mbali mbali na wameshakagua miradi hiyo ukiwemo huo wa Bwawani, lakini kuna ile *Chawal Building* ambayo nayo ina tatizo karibu linafanana na hilo la ukamilishaji wake kwa sababu kibali hakijapatikana, lakini kuna maeneo mengine pia ya Beit-el-Ajaib, kuna

lile jengo la *Majestic Cinema*. Hayo yote sasa yanakaguliwa hivi sasa ili kiweze kupatikana kibali na hatua za ujenzi wa hoteli hii ziweze kuendelea.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Mhe. Spika, ahsante sana kwa kuweza kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Fedha juu ya swali mama alilouliza Mhe. wa Jimbo la Paje nina swali moja la nyongeza lenye kifungu (a) na (b).

(a) Kutokana na majibu mama ya swali hili Mhe. Waziri alieleza kuwa ukarabati ulianza lakini tathmini haijafanyika au haijakamilika. Je, kibali cha kuanza kwa ukarabati huu bila ya kuwepo kwa tathmini za mazingira na zile za athari kutokana na Mji Mkongwe ambao unaeleweka kwamba ni moja kati ya miji ya urithi wa dunia, kibali hicho kilipatikana wapi.

(b) Katika jibu mama hii ilikuwa ni miongoni mwa changamoto ambazo zimaelekea katika kuzuwia au kutoendelea kwa mradi huo. Mhe. Waziri atwambie ni changamoto gan nyengine ukiacha hizi ambazo zimeleta mkwamo katika mradi huu. Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Rashid Makame Shamsi swali lake la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:

La kwanza ni kwamba kama nilivyosema huu mradi unahusisha maeneo makuu matatu, eneo la kwanza ni hoteli yenyewe, lakini eneo la pili ni eneo la Lagoon na eneo la tatu ni nyuma ya ile hoteli ambako kulikuwa kufanyike *reclamation* kufukia ile bahari. Eneo lile la bahari kwa ajili ya kutengeneza *Marine* pale. Sasa ukarabati wa hoteli wenyewe usingekuwa na athari kubwa sana ya kimazingira kwa sababu ni jengo lile lile lilikuwa linafanyiwa ukarabati, lakini haya maeneo mengine ambayo yangefanyiwa kazi yangehitaji kufanyiwa *environmental impact assessment*. Sasa kwa kazi za hatua ya mwanzo ya ukarabati isingekuwa na tatizo hilo na ndio maana kazi ile ilianza, lakini *heritage impact assessment* kwa maana *impact* kwenye urithi wa Mji Mkongwe hiyo lazima *permit* ingehitajika kama ilivyo kwa *Chawal Building*, ilianza kwa sababu lile jengo lilihitaji kuimarishwa zaidi kwa hivyo ilianza kazi hiyo, lakini wakati huo tuna *process* kupatikana kwa *permit* ya kulikarabati jengo hilo. Kwa hiyo, hilo ni jibu (a)

Jibu la pili la mwanzo ambalo lilikwamisha ilikuwa ni mikataba ya ukodishwaji wa ardhi, kwa hoteli mwanzo ilikuwa haina matatizo na mwanzoni kabisa ilikuwa ikodishwe na serikali kwa *lease* ya miaka 33, lakini mwekezaji akaomba aongezewe muda na yeye alitaka miaka 90 kutokana na *investment* kubwa atakayoifanya katika eneo hilo. Lakini vile vile ilikuwa ipatikane *lease* kwenye eneo la *Lagoon* na kule nyuma katika eneo litakalofukiwa bahari. Kwa hivyo, hiyo ilicheleweshe kwa sababu kulikuwa na majadiliano baina ya serikali na mwekezaji huyu.

Lapili lililocheleweshe ni kupatikana hizo *permit* kutoka *UNESCO* kwa mujibu wa sheria zetu. Lakini la tatu ndio kufanyika hizo *Environmental impact assessment* na hiyo *heritage impact assessment.* Lakini hayo yote sasa yanakamilika kwa sababu ujumbe kutoka *UNESCO* tayari uko nchini umeshafanya ziara katika miradi yote hiyo na tuna

matumaini makubwa sana kwamba shughuli hizi zitaanza si muda mrefu kutoka sasa. *(Makofi)*

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Mhe. Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Waziri naomba kumuuliza kwamba katika ujenzi wa Mji Mkongwe kulikuwa na ujenzi wa *Park Hyatt* ambao ilikuwa ni *open space*, ilichukua muda mdogo kupata vibali na kujenga. Vyereje leo Hoteli ya Bwawani ambapo tayari jengo lipo isipokuwa tunalikarabati tu na kutengeneza hoteli ya kisasa kabisa iwe tatizo kupata vibali vya kuendeleza ujenzi ule. Sasa hatuoni kwamba hatumtendei haki Mhe. Rais wa Zanzibar kwa mawazo yale ya kuletewa hoteli nzuri katika mji huu.

Pili, ni sababu gani zilizopelekea kwamba tokea Novemba, 2015 ulivyoingia mkataba wa ujenzi huo na Mamlaka ya Mji Mkongwe ambayo ni sehemu ya serikali kushindwa kurekebisha zile changamoto zinazostahiki na *UNESCO* ili ujenzi ule mara baada ya kuingia mkataba tu uendelee na kujengwa na lini utaanza ujenzi ukilinganisha na kwamba hivi sasa tunapata wasiwasi hata yule mmiliki wenyewe wa kampuni ya *Quality Group* ana mazonge ambayo hatujui kama atakuwa na nguvu zile za kuendeleza ujenzi ule. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Abdalla Maulid Diwani swali lake la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo: Kwanza mradi wa *Park Hyatt* na mradi wa Hoteli ya Bwawani ni miradi miwili tofauti, ina mazingira tofauti, na muda pia ni tofauti. Kwa hivyo, nimhakikishie na Mhe. Spika, kupitia kwako niwahakikishie Wajumbe wa Baraza hili na wananchi kwa ujumla kwamba serikali na taasisi zake inachukuwa kila juhudi ya kuhakikisha kwamba mradi ule unatekezwa kama ulivyopanga kabla.

Maswala yaliyokwamisha tayari nimeyaeleza na juhudi ambazo serikali inazichukuwa tayari nimeyaeleza na nisema kwamba wenzetu wa *UNESCO* walitushauri kwamba miradi yote ambayo serikali inakusudia kuitekeleza ndani ya Mji Mkongwe basi yote iwekwe pamoja ili watakapokufanya ziara waje waikague kwa pamoja na wakitoe kibali waweze kutoa miradi yote ya Mji Mkongwe.

Miradi hiyo hivi sasa iko mingi kuna hiyo Hoteli ya Bwanani nimeisema hapa lakini kuna Darajani *corridor* pia ambao ni mradi mkubwa sana. Lakini kuna ile *Chawal Building* kuna Bet Al Jaibu, kuna jengo la Majestik. Sasa miradi yote hii ilipatiwa kibali kwa pamoja, sasa hilo nafikiri ni jambo la muhimu sana la serikali tujue kwamba inachukuwa juhudi kubwa sana ili kuhakikisha mji wetu unabadilika, urithi wetu unabaki kwa mujibu wa sheria tulizozitunga sisi wenyewe.

Kwa hivyo, hilo naomba Mheshimiwa Mwakilishi aamini hivyo na watendani wanamsaidia sana Mhe. Rais Mawaziri wanamsaidia sana Mhe. Rais na naamini pia Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tunamsaidia sana Mhe. Rais. (*Makofi*)

Nam. 9

Ufaulu mdogo kwa wanafunzi wenye Ulemavu Maskulini

Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis - Aliuliza**:**

Idadi ya ufaulu kwa wanafunzi wenye ulemavu wa aina mbali mbali inaonekana ni ndogo sana kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali siku ya Ijumaa tarehe 23 June, 2017.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia wanafunzi wenye ulemavu kuwa na mazingira bora ya kielimu yatakayowawezesha kufaulu kama wanafunzi wengine wasio na ulemavu.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali – Alijibu**:**

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 9 kama ifuatavyo:-

Serikali imekuwa ikifanya kila linalowezekana kuwajengea wanafunzi wenye ulemavu mazingira bora ya kujifunzia na mazingira bora ya kufundishia kwa walimu ili waweze kufanya vizuri katika masomo yao.

Ili kuwajengea wanafunzi wenye ulemavu mazingira bora yanayowawezesha kufanya vizuri katika mitihani yao; Serikali imetekeleza yafuatayo:-

i. Kuwatambua wanafunzi wenye ulemavu wa aina mbalimbali ili kuweza kuwasaidia katika mahitaji yao ya kupata elimu.

ii. Iliteua Washauri wa Elimu Mjumuisho katika Vituo vyote kumi na moja vya walimu vya Unguja na Pemba na kuwajengea uwezo katika kuwasaidia watoto wenye mahitaji maalum kuweza kujifunza kupitia elimu mjumuisho.

iii. Imeandaa vitini vinne vya kufundishia walimu Washauri wa Vituo hivyo vya Walimu juu ya namna bora ya kuwafundisha wanafunzi wenye ulemavu katika mazingira ya mjumuisho.

iv. Ilianzisha Kozi ya Elimu Mjumuisho ngazi ya Cheti katika Chuo cha Kiislamu Mazizini tokea mwaka 2006 na hadi mwaka 2016 tayari walimu 4002 wameshahitimu na kusambazwa katika skuli mbalimbali za Unguja na Pemba ili kuwahudumikia wanafunzi wenye mahitaji maalumu katika kujifunza.

v. kuanzisha kozi ya Elimu Mjumuisho ngazi ya Diploma katika Chuo Kikuu cha SUZA mwaka 2014 ili kuzalisha walimu wa kutosha watakaoukuwa na utaalamu wa Elimu Mjumuisho, ambapo kwa awamu ya kwanza walimu 34 wamehitimu na kurudi katika maeneo yao ya kazi.

vi. Wizara inaendelea kutoa mafunzo ya Elimu Mjumuisho kwa walimu kuanzia maandalizi, msingi na sekondari na hadi sasa zimefikiwa skuli 142 (Unguja 91 na Pemba 51).

vii. Vifaa vya aina mbalimbali vimenunuliwa kwa wanafunzi wenye ulemavu vikiwemo

Miwani 284, mashine za kuandikia wanafunzi wasioona (*Braille mashines*) 46 na karatasi za kuandikia maandishi ya wasioona rimu 2,000, miwani zenye kukinga jua (plano photo 448), mashine za kuchapa maandishi ya wasioona (*embosser*) 8, kompyuta mpakato (*laptop*) 25, vifaa vya kujifunzia kupitia njia ya michezo (*parcels*)160, karatasi za manila (*reams*) 680, fimbo nyeupe 364, "*marker pens"* 1,000, kuandaa kamusi za lugha ya alama 882 kwa matumizi ya wanafunzi viziwi, wasiokuwa viziwi, walimu na jamii kwa ujumla, vyarahani 5 kwa matumizi ya wanafunzi wenye ulemavu wa akili walioko kwenye vitengo, jozi 135 za jezi kwa matumizi yao katika michezo, shime sikio (*hearing aids*) 188 kwa wanafunzi viziwi pamoja na gundi, madaftari ya kuchorea, penseli za rangi na vifutio. Vifaa vyote hivyo vimegawiwa kwa wanafunzi hao katika skuli mbalimbali ili kukuza uwezo wao wa kiakili na uelewa wao katika kujifunza.
Wizara itaendelea na jitihada za kuimarisha elimu kwa watoto wenye mahitaji maalum kwa kufanya yafuatayo:-

i. Kuajiri walimu 50 waliohitimu kozi ya Shahada na Stashahada ya Elimu Mjumuisho kwa mwaka wa 2017/18.

ii. Kutoa mafunzo kwa walimu katika skuli 150 za Unguja na Pemba kwa miaka 3 kuanzia 2018 – 2021 katika fani ya Elimu Mjumuisho kupitia programu ya *GPE* ili kuwajengea walimu uwezo wa kufundisha wanafunzi wenye mahitaji maalum kwa ufanisi zaidi.

iii. Kuweka miundombinu rafiki kwa watoto wote wakiwemo wenye mahitaji maalum, ikiwemo ujenzi wa '*ramps'* katika skuli 50 (30 Unguja na 20 Pemba).

Programu zote hizo zimeandaliwa ili kuwaandalia wanafunzi wenye ulemavu na wenye changamoto nyengine katika kujifunza waweze kufanya vizuri katika mitihani yao na kuendelea hadi kufikia ukomo wa uwezo wao. Ahsante sana.

Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis: Ahsante Mhe. Spika, kwanza nimpongeze Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri yenye ufafanuzi mpana. Lakini pia pamoja na majibu mazuri ambayo Mhe. Naibu Waziri ameyatoa hapo ya kutengeneza mazingira ya kuwawezesha wanafunzi wenye ulemavu waweze kujifunza bila ya matatizo. Bado kumekuwa na malalamiko kwa wanafunzi hao kukosa mahitaji muhimu ya kujifunzia ikiwemo walimu wenye sifa hasa vijijini.

(a) Je, wizara ina mpango gani wa ufatiliaji ili kuhakikisha yale mazingira wanaowajengea watu wenye ulemavu yanafanikiwa.

(b) Kutokana na taarifa tulikuwa tunao katika Vyombo vya Habari wizara ikifanya ziara katika maskuli mbali mbali kutembelea kuona hali ya elimu inavyoendelea. Je, katika ziara zile ni skuli zipi zenye Elimu Mjumuisho ambazo wameweza kutembelea na kuona hali halisi ya watoto wenye ulemavu.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali napenda kumjibu suala lake la nyongeza a b Mhe, Mwantatu Mbarouk Khamis kama ifuatavyo:-

(a) Ni kweli viongozi mbali mbali wa Wizara ya Elimu tumekuwa tukifanya ziara ya kutembelea katika skuli zote zikiwemo hata hivi vituo Mahsusi. Niseme kwamba madhumuni hasa ni kuona kwamba maelekezo na miongozi yote ya wizara yanatekelezwa kwa ufanisi.

Kwa hivyo, niseme tu kwamba ili kuona mipango na maelekezo yanafutwa kwa ukamilifu ikiwemo skuli hizi za mjumuisho ni kwamba wizara pamoja na taratibu zake za kawada za ufatiliaji kupitia wakaguzi. Lakini pia imeandaa mpango maalum wakiwemo Wakurugenzi wote katika Wizara ya Elimu kupitia katika skuli zote zikiwemo hizi ili kuona yale maelekezo yanafanyiwa kazi kama ilivyo, na mimi mwenyewe nimekuwa nikifanya ziara hizo.

(b) Niseme kwamba nimewahi kutembelea skuli hizi mimi binafsi Skuli ya Michakaeni, Skuli ya Pandani na hata Skuli ya Jangombe na Mwanakwerekwe hizi zote nimezipitia na nimepitia wakati mwengine na kuzungumza na walimu wote wanaohusiana na elimu hii ya vitengo wakaeleza changamoto zao na matokeo ya mazungumzo hayo ni kupatikana hivi vifaa ambavyo tumevitaja hapa. Ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe maswali yaliyobaki bado mengi na muda tulionao ni mchache. Sasa ningeshauri sana Mawaziri mjitahidi kujibu *specifical* kwenye yale maswala mliyouliza. Lakini na maswala ya nyongeza kutoka kwa Wajumbe wajitahidi sana yawe mafupi maswala yamekuwa na maelezo yaani kama mtu anahutubia.

Kwa hivyo, ili kuokoa huo wakati nitaenda sasa kwenye wizara nyengine ili kujaribu kumaliza maswali tuliyonayo. Katibu Wizara inayofuata. (*Makofi*)

Nam. 28
Ununuzi wa Zao la Mwani

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza**:**
Tarehe 22/8/2017 Vyombo vya habari vilitangaza kwamba wanunuzi wa mwani wamekuwa wakilalamikia Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kupata vikwazo wakati wa usafirishaji wa mwani wao kupelekwa nje ya nchi.

(a) Je, kuna Kampuni ngapi zinazonunua mwani Unguja na Pemba.

(b) Je, tunawasaidia vipi wakulima wa mwani baada ya kupoteza muda wao katika kilimo hicho kwa kuzingatia agizo la Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuagiza Wizara nne (4) ambazo ni Wizara ya Afya, Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko, Wizara ya Fedha na Mipango na Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi zikae pamoja kutatua tatizo hilo.

(c) Je, Serikali iko tayari kujipanga katika kununua zao hilo kama inavyonunua zao la karafuu ili kuwanyanyua kiuchumi wakulima hasa akina mama.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko - Alijibu**:**
Mhe. Spika, kwa ruhusa aomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 28 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, Kampuni kubwa zinazosafirisha mwani kwa Pemba na Unguja ambazo ni ZANEA, SEAWEED, TAWAKAL, ZANQUE, SM RASHID, BIRR, GIM na LEDO BIASHARA. Hata Kampuni zinazochukua vibali kupitia Wizara ya Biashara ni ZANEA, GIM na hawajaripoti kuwa wanapata matatizo. Wasafirishaji hawa baada ya kukamilisha taratibu zote hupatiwa kibali ndani ya masaa 24 tena bila ya malipo.
Kampuni nyengine zinazosafirisha mwani huwa hazichukui vibali na hazifuati taratibu za usafirishaji na husafirisha kwa utaratibu wanao ujua wenyewe ndio maana hupata matatizo wakati wa usafirishaji. Matatizo yanaojitokeza pale ambapo wanafika bandarini bila ya kuwa na kibali maalum cha usafirishaji na kupelekea kuzuiliwa bidhaa yao hadi wapate kibali cha usafirishaji.

(b) Kupitia Idara ya Viwanda Wizara imeanzisha *cluster* maalum kwa ajili kusimamia suala la kilimo cha mwani hapa Zanzibar.

(c) Suala la kuitaka *ZSTC* inunue zao la mwani, Wizara imelipokea wazo hilo na italifanyia kazi ikiwa utaratibu utaruhusu.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja ma majibu ya Mhe. Waziri naomba kuuliza maswala madogo sana ya nyongeza na kama ulivyosema tuulize kwa ufupi kidogo.

(b) Je, ni wananchi ili	Kilio cha wakulima ni kuona serikali inanunua mwani kama zao la karafuu. lini itafanya maamuzi mazito ya kununua zao hilo kwa manufaa ya kuliendeleza zao la mwani.
(b) mwani wakulima	Kwa nini serikali inaendelea kulinda zao la karafuu huku wakulima wa wakiendelea kuhangaika na soko hilo. Je, kilo ya mwani huko nje wanauza shilingi ngapi.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, naomba nijibu suala la Mhe. Jaku Hashim Ayoub kama hivi ifuatavyo:-

Serikali imechukuwa kila jitihada kuona kwamba zao la mwani linashughulikiwa na kuweza kuwanufaisha wakulima ambao wengi wakulima wa mwani ni wanawake ambao Serikali hii ya Mapinduzi ya Zanzibar inawathamini sana na inawapa kipaumbele.

Kwa hiyo, kwamba serikali imechagua zao la karafuu na kuliacha zao la mwani si kweli na haiwezi kufanya hivyo hata siku moja serikiali ambayo inawajali wananchi wake kama hii Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Kwa hiyo, ni kwamba kamati zimeundwa maamuzi yamechukuliwa na suala la kwamba *ZSTC* ichukuwe mwani sio jawabu la kudumu na zao la mwani kwa sababu zao la mwani linatokana na utaratibu mzima wa zao hili tafauti na zao la karafuu ilivyokuwa historia yake na kama hapa ilipo.

Naomba nimuhakikishie Mhe. Jaku Hashim Ayoub na Waheshimiwa wote na wananchi kwamba serikali inalifanyia kazi na mapendekezo mbali mbali yamechukuliwa na hatua zitakazokuwa mjarabu zitachukuliwa hivi karibuni ili kuona kwamba zao la mwani linawapatia tija wakulima wake.

Sasa hivi Mhe. Spika, mwani wanalipwa shilingi mia nne kwa kilo lakini hata huko nje vile vile bei yake imeshuka vile vile hailingani kama ilivyokuwa huko nyuma. Ahsante.

Mhe. Spika: Katibu kwa wizara inayofuata.

Nam. 53

Kukamilisha mradi wa ujenzi wa Miundombinu ya Umwagiliaji Maji

Mhe. Omar Seif Abeid- Aliuliza**:**

Mradi wa ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji maji mashambani wenye thamani ya Dola million 50 za Kimarekeani ambao ungelikidhi kutumika kwa jumla ya hekta 1560, haukukamilika kutokana na kukosekana Mkandarasi wa ujenzi huo wa miundombinu ya umwagiliaji maji.

(a) Je, ni lini taratibu za zabuni ya kupata mkandarasi mwengine itakamilika ili kuwezesha mradi huo mkubwa kuanza.

(b) Iwapo mradi huo utakamilika ni wakulima wangapi wanaotarajiwa kunufaika na mradi huo, na maeneo gani zaidi yaliolengwa na ni kilimo cha aina gani kilichokusudiwa katika maeneo hayo.

(c) Je, Dola 50 Millioni za Marekeani ambazo zitatumika kwa mradi huo ni mkopo au ni ufadhili wa wahisani.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi - Alijibu**:**

Mhe. Spika, Kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 53 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kabla ya kumjibu suala la Mhe Mwakilishi naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli kwamba Mradi wa Ujenzi wa Miundombinu ya Umwagiliaji Maji Zanzibar ni miongoni mwa miradi inayosimamiwa na Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi na ambao ufadhili wake unatokana na mkopo kutoka Benki ya Exim ya Korea. Fedha hizo za mkopo zilikisiwa kuwa ni Dola za Kimarekani milioni hamsini (*USD 50,000,000*) ambazo ziligaiwa katika awamu mbili. Awamu ya kwanza ni kwa ajili ya usanifu michoro, kutengeneza kabrasha la zabuni na usimamaizi wa ujenzi wa miundombinu hiyo; na awamu ya pili ya matumizi ya fedha hizo imelengwa kwa ajili ya kazi za ujenzi wa miundimbinu hiyo ya umwagiliaji maji Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, zabuni ya kumpata Mkandarasi wa kazi hiyo ilikumbana na changamoto mbalimbali. Miongoni mwa changamoto zilizojitokeza katika zabuni hiyo ilikua ni pamoja na kukosekana kwa ushindani katika mchakato wa zabuni hali hii ilitokana na kuwasilishwa kwa zabuni moja tu; jambo ambalo linakwenda kinyume na Sheria ya Manunuzi ya Zanzibar ya mwaka 2015.

Mhe. Spika, mbali ya changamoto hizo, napenda kumuelewesha Mheshimiwa Mwakilishi kwamba azma ya kuutekeleza mradi huu iko pale pale na utekelezaji wake utaanza mara tu baada ya mchakato huu ulioanza wa kumpata mkandarasi wa ujenzi kukamilika.

Baada ya maelezo hayo mafupi,sasa naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swala lake namba 53 lenye kifungu a, b na c kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, taratibu za kumpata mkandarasi mwengine zinaendelea na kabrasha la zabuni *''Tender documents''* kwa ajili ya kutangaza na kumpata mkandarasi limeshatengenezwa kwa mashiriakiano na Mshauri Mwelekezi na limeshatumwa *Exim Bank-Korea* kwa hatua nyengine na Wizara inasubiri kupokea hayo makabrasha na kupata ridhaa hiyo tu kutoka *Exim Bank Korea* kwa ajili ya kuendelea na mchakato huo.

(b) Mhe. Spika, mradi huu unategemea kuwanufaisha zaidi ya Wakulima 1,524 Unguja na Pemba hususan kutoka katika maeneo ya Chaani, Kinyasini, Cheju, Kibokwa na Kilombero kwa upande wa Unguja na Mlemele na Makwararani kwa Pemba. Aidha, Mradi huu umekusudiwa zaidi kwa zao la mpunga. Hata hivyo, wakulima wanaweza kutumia vizuri fursa hii ya rasilimali maji kwa mazao mengine ikiwemo mboga ili kuongeza uzalishaji na mapato kwa wakulima na kwa Taifa kwa ujumla.

(c) Mhe. Spika, fedha zitakazotumika katika kutekeleza mradi huu ni mkopo kutoka *Exim Bank ya Korea*. Ahsante.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Spika, nashukuru sana kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Lakini nachukuwa fursa hii kumpongeza Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri aliyoyatoa, lakini naomba kidogo niulize swala la ngongeza.

Kwa kuwa fedha hizo ni mkapo na kwa kawaida mkopo huwa una riba na wao nyie mmsema kwamba bado mnatengeneza hayo makabrasha mnayasubiri kutoka huko *Exim* ndio tufanye utaratibu wa kumpa huo mkandarasi muelekezi kwa ajili ya ujenzi.

(a) ni ya Exim — Mkandarasi mwelekezi kwa ajili ya ujenzi. Sasa swali langu liko hapa. Je, asilimia ngapi ya riba ambayo serikali sisi tutawajibika kuilipa hiyo Benki ya Korea kutokana na mkopo huu. Hilo la kwanza.

(b) mkopo wa ambao mkataba wa — Napenda nijuwe ni utaratibu gani wa kuanza kufanya marejesho ya huo hao Exim Benki wametupa, ni baada ya kukamilika kwa huo mradi wetu tunakusudia kuufanya au ni baada tu ya pale mara tutakapo saini huo kuupokea huo mkopo. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Spika, naomba kujibu swali la Mhe. Omar Seif Abeid, swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri kwamba huo ni mkopo nafuu, na mkopo nafuu una masharti yake na masharti ya mkopo nafuu, riba inakuwa haizidi asilimia 2, ndio mikopo ambayo tunachukua, na huu utakuwa baina ya asilimia 1.5 mpaka asilimia 2 hautazidi hapo. Lakini mazungumzo yanaendelea na wenzetu wa Exim Benki, kwa sababu fedha hizi zinatoka katika shirika moja la mashirikiano na maendeleo ya kiuchumi la Korea, kwa maana ya *Economic*

Cooperation and Development Fund. Hawa wametufikishia fedha hizi kwa kupitia Benki ya Exim na masharti ni hayo.

Lakini vile vile kunakuwepo na masharti nafuu ya muda wa kuanza kulipa mkopo huu, kwa maana ya *grace-period* na hiyo inaweza kuwa baina ya miaka sita mpaka miaka minane, lakini pia mkopo huu ni wa muda mrefu, kwa hivyo malipo yake yatalipwa kwa kipindi kirefu baada ya kukamilika kwa ule mradi.

Nam. 127

Ukosefu wa Huduma za Afya Katika Kijiji cha Uzi Ng'ambwa

Mhe. Hidaya Ali Makame - Aliuliza:-

Katika kijiji cha Uzi Ng'ambwa wananchi wamekuwa wakipata dhiki kubwa sana katika suala zima la huduma za afya kutokana na ukosefu wa madaktari na huduma nyingi muhimu katika Kituo cha Afya kilichopo kijijini hapo. Kwa kuwa huduma za Afya ni miongoni mwa mambo muhimu yanayohitaji kupewa kipaumbele cha hali ya juu na Serikali katika kuhakikisha kuwa wananchi wake wanaishi kwa uhakika wa kupata huduma bora za afya, kwa kuwa ni mpango wa Serikali kuhakikisha kuwa inawapatia wananchi wake wote huduma bora za afya kwa wakati bila usumbufu wowote.

Je, Wizara inafahamu kuwepo kwa hali hiyo kijijini hapo na imechukua hatua gani kukiboresha kituo hicho hasa ikizingatiwa kuwa nyumba ya madaktari ipo na ni nyumba ya kisasa lakini haitumiwi na madaktari jambo ambalo linapelekea usumbufu mkubwa kwa wananchi wanapohitaji huduma za afya kituoni hapo.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 127 kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Kituo cha Afya Uzi Ng'ambwa ni kituo cha Daraja la Kwanza, hivyo huduma zitolewazo ndizo ambazo zinapaswa kutolewa katika kituo chenye hadhi ya daraja hilo. Ni kweli kituo hiki kilikuwa na uhaba wa wafanyakazi, lakini kwa sasa kituo hiki cha afya cha Uzi Ng'ambwa kina wafanyakazi watatu, ambapo mfanyakazi mmoja kati yao aliyekuwa akiishi katika nyumba ya madaktari, na kwa bahati mbaya mfanyakazi huyo amepata maradhi na wizara imemuondosha na kumpeleka mfanyakazi mwengine kushika nafasi yake.

Mhe. Spika, huduma katika kituo cha afya cha Uzi Ng'ambwa zinaendelea kutolewa kama kawaida. Mhe. Spika, kituo cha Uzi Ng'ambwa wafanyakazi wawili kati ya watatu waliopo sasa wanaishi hapo hapo katika kijiji cha Uzi katika nyumba zao za kifamilia. Kwa hivyo, wananchi ni rahisi sana kuwafikia wafanyakazi hao pindi itokeapo dharura yoyote.

Mhe. Spika, wizara yangu imo katika hatua za kuhakikisha inaweka mfumo wa kuwa na daktari atakayekaa katika nyumba hiyo, ili wananchi waweze kuhakikishiwa kupata huduma bora zaidi kwa wakati wote na kwa ukaribu zaidi. Ahsante *(Makofi)*

Mhe. Hidaya Ali Makame: Ahsante Mhe. Spika, kwanza nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa majibu yake ambayo yako tofauti na niliyopewa mimi na leo pia. Mhe. Spika, napenda nimuulize tena Mhe. Waziri swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa wafanyakazi wawili ndio wanaoishi ndani ya kijiji cha Uzi Ng'ambwa na tunafahamu kwamba ndani ya kijiji hiki kunahitaji huduma za pekee kwa vile kijiji hiki ni cha kisiwa na watu ni lazima wavuke.

(a) Je, huduma hizi za daraja la kwanza ambazo umetuambia kwenye majibu mama, unahisi kwamba zinastahiki katika kijiji hiki ambacho wananchi wanaoishi ndani ya kijiji hiki wengi wao ni wakulima, wavuvi na ni wananchi wa kawaida.

Je, ni hatua gani ambazo zitachukuliwa kukiimarisha kijiji hiki ili huduma nyingi au karibu ya zote ziweze kupatikanwa kwa urahisi zaidi na kwa kuwajali wananchi hawa kutokana na hali ya kijiji chao cha usafiri na kila kitu.

(b) Je, ni hatua gani ambazo nyinyi kama wizara mmezichukua kwenda kuangalia utaratibu wa huduma ndani ya kijiji kile ambapo tunaambiwa kwamba ndani ya kijiji kile na nimefanya uchunguzi mimi mwenyewe nikiwa kama mjumbe wa kamati ya Wizara ya Afya, kwenda kufanya uchunguzi na pale huduma zao wanazitoa mwisho saa 3:00 kwa huduma za upimaji wa watoto yaani *clinic*.

Je, ni taratibu gani ambazo mtazichukua ili kuhakikisha kwamba katika kijiji hiki huduma zinatolewa muda wote na masaa yote. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mjumbe maswali yake ya nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Spika, kijiji cha Uzi kipo karibu sana na kijiji cha Unguja Ukuu, kwa hivyo huduma nyingi ambazo wanazikosa wananchi katika Kituo cha Afya cha Uzi Ng'ambwa, huwa wanazipata katika kituo cha Unguja Ukuu ambapo ni kituo ambacho kinafanya huduma zote kwa masaa 24.

Hata hivyo, wizara ina mpango maalum inajiandaa katika vijiji vyote ambavyo viko kwenye kisiwa kikiwemo kijiji cha Uzi Ng'ambwa, kuweka vituo vyenye huduma maalum vya masaa 24, ili kuweza kuwaondoshea kadhia hii ya wananchi kufuata huduma katika vijiji vya jirani ambavyo ni lazima wavuke.

Mhe. Spika, wizara imo katika mkakati huu na mara baada ya kukamilisha mipango yake katika vijiji ambavyo vitaanzwa kwa matengenezo basi nitaishauri wizara yangu ianze na kituo cha kijiji cha Uzi Ng'ambwa. Ahsante Mhe. Spika. *(Makofi)*

Nam. 18

Ubovu wa Daraja la Tingatinga

Mhe. Suleiman Sarahan Said – Aliuliza:-

Katika Mji wa Chake Chake, barabara inayokwenda Wesha ni njia moja tu na kuna daraja la zamani la Pondeani ambapo zikinyesha mvua kubwa maji hupita juu na daraja hilo si la kuaminika sana kutokana na uchakavu. Lakini ipo njia nyengine mbadala ya kiwanja cha watoto kupitia daraja la Tingatinga ambayo tatizo lake ni daraja.

(a) Je, Serikali haioni umuhimu wa kulijenga daraja hilo kwa sasa kabla ya dharura hio haijajitokeza kwa kuzingatia umuhimu wake wa kuunganisha na eneo la Wesha ambapo ndipo kwenye mafuta yanayotumika kwa kisiwa chote cha Pemba na pia kituo cha Umeme cha Wesha.

(b) Barabara hiyo ya Tingatinga kwa sasa inapitwa na waenda kwa miguu lakini alama ya barabara ya zamani ipo, ni lini Serikali itaipima kabla haijavamiwa kwa kujengwa nyumba.

(c) Je, Serikali haioni umuhimu wa kupima na kusafisha barabara hiyo kwa kuweka alama ya upana na kuongeza eneo la ziada kwa vile eneo hilo bado halina majengo.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Manaibu Mawaziri mlioko upande huu, ukijua kwamba swali lako linakaribia basi ni vyema ukasogea kiti kile pale, kwa sababu mnapoteza muda mwingi sana kuja kujibu. Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji karibu.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 18 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo.

(a) Mhe. Spika, serikali inatambua umuhimu wa daraja hilo la Pondeani ambalohufurika wakati wa mvua za masika. Napenda kumthibitishia Mhe Mjumbe kuwa daraja ni imara tatizo ni udogo wa mlango wa kupitishia maji. Kutokana na umuhimu wa barabara hiyo, wizara yangu imepanga kulijenga upya daraja hilo kwenye bajeti ya mwaka wa fedha 2018/19, ili liweze kukidhi haja ya maji yanayopita hapo pamoja na usalama kwa wanaoitumia barabara hiyo.

(b) Serikali haina mpango wa kuipima barabara ya zamani inayotumiwa na wananchi kupitia Tingatinga isipokuwa tunaushauri Uongozi wa Baraza la Mji wa Chake Chake uhakikishe kuwa eneo hilo halivamiwi kwa kujenga jengo la aina yoyote, kwa vile hiyo ni njia mbadala inayotumiwa na wananchi waendao kwa miguu.

(c) Suala la kupanua na kuweka alama kwenye barabara hiyo, linaweza kufanywa na uongozi wa Baraza la Mji na wizara yangu iko tayari kutoa wataalam kama watahitajika. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nakushukuru Mhe. Spika, mimi nataka waziri kwanza kutokana namajibu yake nimuulize tu. Je, ile barabara ni ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji au ni wizara ya serikali za mitaa.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Spika, hivi sasa katika kugatua madaraka kuna barabara ambazo ziko chini ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji ambazo zimegawika katika sehemu tofauti na zaidi zile ambazo tunaita *Trunk Road* na barabara nyengine muhimu.

Lakini vile vile kuna barabara ambazo ziko katika Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ. Lakini katika kufanyakazi wakati wowote sisi tunakuwa tunashirikiana na pale ambapo kutakuwa na agizo la kufanya hiyo kazi, basi tunaifanya kazi kwa ajili ya nchi yetu na kwa vile sote serikali tunafanyakazi kama timu moja. Ahsante Mhe. Spika.

Nam. 131

Urasimishaji wa Usafiri wa Pikipiki (Bodaboda)

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Aliuliza:-

Kutokana na ongezeko la magari katika mji wa Zanzibar imekuwa ni tatizo kubwa kusafiri kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyengine. Tatizo hilo huzidi kujitokeza wakati watu wanapokwenda na kutoka kazini, ambapo nchi za wenzetu tatizo hilo limepatiwa ufumbuzi kwa kurasimisha usafiri wa pikipiki au hata bajaji. Usafiri huo unatumika zaidi pale linapotokea jambo la dharura kwa mtu kuweza kufika kwenye eneo husika au kutaka kuwahi anapokwenda.

(a) Kwa vile usafiri huu unatumika sehemu nyingi duniani, nini kinatuzuia sisi Zanzibar tusirasimishe usafiri huu ili kuwaondelea adha wale wanaotaka kuwahi asubuhi kama wale wanao kwenda kazini au katika shughuli zao binafsi ili kufukuzana na wakati.

(b) Kwa vile hata bila ya ruhusa rasmi usafiri huo sasa umeshakuwa maarufu na unawasaidia wengi hasa katika sehemu ambazo hawana usafiri wa gari, kwa nini Serikali inaendelea kulifumbia macho jambo hilo.

(c) Kwakuwa Serikali haina ajira za kutosha kwa vijana wetu, na wenye bodaboda wameamua kujiajiri na kuanzisha umoja wao ili waweze kusajiliwa rasmi, Je mtakataa kufanya hivyo kwa sababu ni chombo cha magurudumu mawili kama ambavyo mlitujibu kikao kilichopita.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu:-

Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 131 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, serikali haijakataza matumizi ya bajaji, pikipiki kutumika katika usafiri katika mji wa Zanzibar kwa watu wote ambao wanataka kutumia usafiri huo kwa matumizi yao binafsi au kwa kukodisha ili mtu aendeshe mwenyewe isipokuwa dereva na abiria wanatakiwa lazima wavae kofia ngumu na kufuata sheria za barabarani.

(b) Mhe. Spika, serikali haijatoa leseni kwa pikipiki kusafirisha abiria kwa njia ya biashara na atakaekuwa anatumia pikipiki kwa kusafirisha abiria kwa biashara atakuwa anakwenda kinyume na sheria yetu kifungu cha 66 cha sheria nambari 7 ya mwaka 2003.

(c) Kweli serikali haina ajira za kutosha kwa vijana wetu lakini mara nyingi inawashajihisha na kuwashauri vijana wafanye ajira halali zilizoruhusiwa kisheria. Katika utafiti uliofanywa katika miaka ya nyuma mjini Dar es salaam, imeonekana madhara yanayopatikana katika usafiri wa bodaboda ni mkubwa zaidi kuliko faida zake.

Kwa mfano, katika hospitali ya Muhimbili kila siku wanapokewa majeruhi wasiopungua 15 wa ajali za Bodaboda. Aidha, dereva na abiria wa chombo cha maringi mawili 2 anatakiwa avae kofia ngumu, lakini kutokana na kofia ngumu ya abiria kuvaliwa na kila abiria atakaepakiwa. Kwa hivyo, upo uwezekano mkubwa wa maambukizi wa maradhi ya ngozi na chawa, na abiria wengine kukataa kuvaa kofia hiyo kutokana na uchafu wake au harufu mbaya inayotoka katika kofia hiyo ya abiria, inayotokana na majasho ya abiria tofauti wanaopakiwa katika vyombo hivyo. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa: Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kumuuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo.

(a) Mhe. Naibu Waziri ni hatua gani mnazochukua kwa madereva wa bodaboda waliojaa katika maeneo ya Donge ya zamani, barabara ya kwendea Kwarara Masingini ambao wanakinzana na sheria na mpaka sasa wanaendelea kuchukua abiria.

(b) Je, ni madereva wangapi wa bodaboda hadi sasa wametiwa hatiani ambao wamekwenda kinyume na kifungu cha sheria hiyo ya barabara.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mjumbe maswali yake yenye vifungu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo. Mhe. Spika, kama nilivyosema kweli inawezekana ikawa watu wanafanya biashara hiyo ambayo iko kinyume na sheria, lakini kama nilivyosema kumkamata sasa yule abiria anayepakiwa na kwenda kutoa ushahidi Mahakamani inakuwa ni kazi ngumu sana.

Mhe. Spika, kwa baadhi ya wakati sasa Polisi pamoja na watu wetu wanatumia njia ya kwenda kukodi ile bodaboda na baadae pale anapothibitika kwamba yule mtu tayari anachukua pesa, basi pale ndipo tunachukua hatua za kumpeleka Mahakakani. Lakini kama nilivyosema ni kazi ngumu na hadi hivi sasa tumeweza katika kufanya msako huo na ukaguzi ili kuwakamata watu wasiozidi watano wanaofanya biashara hii ya bodaboda. Ahsante Mhe. Spika.

Nam. 112

Ahadi ya Mhe. Rais ya Ujenzi wa Njia ya Ukongoroni

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dkt. Ali Mohammed Shein anastahiki pongezi kwa kutekeleza ahadi mbali mbali alizotoa wakati wa Kampeni. Hata hivyo, kuna ahadi ya ujenzi wa njia ya Ukongoroni aliwahi kuitowa kwenye uwanja wa zikri tokea alipokuwa anawania kuchaguliwa katika kipindi cha kwanza cha uongozi wake ambayo bado haijatekelezwa hadi sasa.

Je, ahadi ile ya muda mrefu ya ujenzi wa njia ya Ukongoroni itatekelezwa lini?

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 112 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli kwamba Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi wakati wa kampeni alipokuwa akiomba ridhaa ya wananchi, ili aweze kuchaguliwa kuwa Rais wa Zanzibar kupitia tiketi ya Chama cha Mapinduzi, aliahidi kuwa chini ya uongozi wake atahakikisha barabara ya Jozani – Charawe – Ukongoroni – Bwejuu yenye km 23 inajengwa kwa kiwango cha lami, ili iweze kuwaondolea usumbufu wananchi katika maeneo hayo. Ndio maana katika ilani yetu ya mwaka 2015/2020 imewekwa barabara hii.

Aidha, mnamo tarehe 15/08/2017 wakati Mhe. Rais alipofanya ziara ya kutembelea Wilaya ya Kati Unguja, alikumbushia ahadi yake hiyo na kusisitiza kwamba barabara hiyo itaanza kujengwa katika mwaka huu wa Fedha 2017/2018.

Mhe. Spika, naomba nimthibitishie Mhe. Mwakilishi kwamba, wizara yangu inalifanyia kazi suala hilo, ili barabara hiyo ianzekujengwa katika mwaka huu wa fedha 2017/2018 kama tulivyoahidi Mhe. Rais. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri kwanza nichukuwe fursa hii kuwapongeza sana *UUB*, pamoja na changamoto ya vitendea kazi hawana, lakini wanafanyakazi kwa jitihada bila ya kujali mvua wala jua, niwapongeze sana na niwapelekee salamu chini ya uongozi wa Ali Tahir.

Mhe. Spika, baada ya hapo, serikali iliahidi kuwa ujenzi huo utafanyika mwaka ujao wa fedha. Je, tathmini gani iliyofanyika mpaka sasa kwa gharama za ujenzi huo wa barabara ili wananchi wapate kujua, na vile vile kumrahisishia mwakilishi wa jimbo hilo Mhe. Issa Ussi Haji Gavu ili kutembea kwa vizuri kwa wananchi wake.

Mhe. Spika, ni faida gani za kiuchumi ambazo zitapatikana mara baada ya barabara hiyo kumalizika?

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake la nyongeza lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

(a) Mhe. Spika, kama unavyojua na kama alivyosema yeye mwenyewe anawapongeza sana Idara ya *UUB* na kweli baada ya lile agizo la Mhe. Rais, basi watu wangu wamekwenda mara moja kuangalia lile eneo lote na kufanya tathmini na jana tu limezungumzwa na Mkurugenzi na nampongeza sana, kwa sababu wakati wowote unapomwita basi anakuwa tayari kufanyakazi na nilimpa maagizo kwamba aende mara moja kufanya hiyo tathmini na baadae atuletee serikalini ili kukaa pamoja na Wizara ya Fedha na Mipango tuangalie namna gani ya kuanza kutimiza ile ahadi.

(b) Kuhusu faida. Mhe. Spika, kama unavyojua kuna mazao kule na utalii. Kwa hivyo, faida kubwa sasa itapatikana kwa wananchi kuongeza kipato chao na vile vile serikali nayo itaendelea kupata pato la taifa, kwa sababu kama unavyojua pia kuna shamba kubwa sana la ndimu kule Bwejuu, na Mhe. Rais juzi alitembelea na kuna vipando vingi tu. Kwa hivyo, faida kubwa sana itapatikana kwa wananchi na taifa letu, hasa katika sekta hii ya kilimo. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Ahsante Waheshimiwa Wajumbe, wakati wa maswali umekwisha. Nina matangazo. Tangazo letu la mwanzo ni tangazo la wageni, wageni wetu wa leo wa kwanza ni wageni wa Mhe. Nadiri Abdul-latif Yussuf Al Wadir mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Chaani jumla yao ni wanne

Mhe. Nadiri Abdul-latif Yussuf: Mhe. Spika, utaratibu.

Mhe. Spika: Wapo wameshasimama nimewaona, wamenyanyuka huko nyuma. Jumla yao ni wanne, hawa ni Madiwani wa jimbo hilo. Naomba mnyanyuke;

1. Ndg. Twaha Hija Kheir
2. Ndg. Omar Abdalla Kuteuliwa Chaani
3. Ndg. Miza Makame Haji Kuteuliwa Chaani
4. Ndg. Raya Ali Makame Kuteuliwa Chaani

Karibuni sana madiwani kwenye Baraza la Wawakilishi. *(Makofi)*

Wageni wanaofuata ni wageni wa Mhe. Machano Othman Said Mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Mfenesini, jumla yao ni 9, hawa ni wajumbe wa Kamati ya Siasa ya Wadi ya Kama. Wageni wenyewe ni kama wafuatavyo.

1. Ndg. Salum Said Seif — Mwenyekiti
2. Ndg. Abdalla Said Washoto — Katibu
3. Ndg. Fatma Mpendakazi Kudema — Katibu Mwenezi
4. Ndg. Alawi Abdalla Alawi — Mjumbe
5. Ndg. Nia Waziri Seif — Mjumbe
6. Ndg. Fatma Haji Mohamed — Mjumbe
7. Ndg. Shaaban Seif Mohamed — Mjumbe
8. Ndg. Khamis Makame Mussa — Mjumbe na
9. Ndg. Mustafa Kheir Milad — Mjumbe

Karibui sana kwenye Baraza la Wawakilishi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, tangazo jengine nililonalo ni tangazo la Mhe. Ali Suleiman Ali Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii ambaye anawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati hii ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii, kwamba wanaombwa wakutane katika ukumbi wa chumba cha kamati namba 2 mara tu baada ya kipindi cha maswali na majibu.

Waheshimiwa Wajumbe kuna mambo mengine madogo madogo ambayo yamejitokeza. Moja ni suala la Uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi kwenye ngazi ya Wilaya. Suala hili nimekuwa naletewa vibarua vingi sana vya kuniaga ili watu wakashiriki kwenye huo uchaguzi lakini naona ni bora tutalitolea maelezo jioni baada ya kukaa na mwenyekiti, kwa sababu Mwenyekiti wetu tunae humu humu ndani wa *cocas* tutalizungumzia hili hili halafu tutaweza kuwa na majibu mazuri ya kuwapa.

Lakini pamoja na hayo kuna wale wenzetu ambao wanatokea Pemba ambao wanaaga kwa ajili ya suala hili hili lakini wale ambao wanaaga kwa ajili ya mwenge pia, wamekuwa wakiniletea maombi katika nyakati tofauti kila mtu analeta kivyake lakini sasa ninahofia kutoa ruhusa kwa sababu ya *quorum* kwa sababu pia Alhamis Baraza litakuwa lipo kama kawaida na ndio maana nasema tutajariliana na mwenyekiti wetu kwa ajili ya kuona nama gani, au namna ipi nzuri ambayo itatuwezesha kushiriki kwenye hizo chaguzi lakini wakati huo huo kuweza kuwepo hapa kwenye Baraza la Wawakilishi.

Mwisho wa matangazo Ahsanteni.

HOJA ZA SERIKALI

Ripoti ya Afisi ya Rais Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ ya utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Sheria Utawala Bora na Idara Maalum kwa Mwaka 2016/2017

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kuwasilisha taarifa ya utekelezaji wa hoja na maoni wa Kamati ya Baraza la Wawakilishi ya Sheria Utawala Bora na idara Maalum za SMZ .

Awali ya yote naomba kwanza kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutujaalia kuwa na afya njema na kutuwezesha kukutana hapa katika kikao hiki muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu. Vilevile, naomba kuchukuwa fursa hii kukushukuru wewe Mheshimiwa Spika, Naibu Spika, Wenyeviti wa Baraza na Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi kwa uongozi wenu wenye hekima, busara na uadilifu katika kuliongoza Baraza na kuliwezesha kusimamia vyema majukumu yake.

Mhe. Spika, Pia, natoa shukrani zangu za dhati kwa Mwenyekiti na Wajumbe wa Kamati kwa mashirikiano makubwa wanayoipatia Ofisi yetu na kwa ushauri na maelekezo yao kwetu yanayotusaidia sana katika kutekeleza majukumu yetu kwa ufanisi na ndio chachu ya maendeleo yetu.

Mhe. Spika, Ofisi yangu ilipokea hoja za Kamati ya Baraza la Wawakilishi ya Sheria, Utawala bora na Idara Maalum za SMZ zinazohusu Mamlaka za Mikoa na Serikali za Mitaa, Idara Maalum pamoja na Ofisi ya Usajili wa Vizazi, Vifo na Kadi za Utambulisho.

Mhe. Spika, Jumla ya Maoni na ushauri 95 tumeyapokea na kuyafanyia kazi. Kati ya hayo, maoni 71 yalihusu Mamlaka za Mikoa na Serikali za Mitaa, 21 yalihusu Idara Maalum za SMZ na 3 yalihusu Ofisi ya Usajili wa Vizazi, Vifo na Kadi za Utambulisho.

Mhe. Spika, Hata hivyo, baada ya kuyapitia na kuyafanyia kazi ushauri na maoni hayo, tumegundua baadhi yake yanafanana hivyo, tumeyaweka katika kifungu kimoja na sasa katika uwasilishaji wa utekelezaji tutabaki na vifungu 62 badala ya vifungu 95.

Mhe. Spika, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ imezingatia ushauri na maoni yaliyotolewa na Kamati na kuchukuwa hatua za utekelezaji kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, maoni na ushauri huo tumeyaweka katika Utaratibu wa Bangokitita lenye mnasaba wa namba za maoni, Taasisi husika suala lenyewe tuliloletewa pamoja na utekelezaji wake. Mhe. Spika, kwa ridhaa

yako naomba nisome maoni na ushauri na halafu nisome utekelezaji wako, naomba ridhaa yako nifanye hivyo kwa ajili ya kuokoa muda kwa sababu masuala ni mengi 62, vile vile kama utaniridhia niyasome yote moja baada ya jengine au namna gani natumai umeniridhia yote hayo.

Moja Kamati inashauri Ofisi ya Mrajis wa Vizazi na Vifo kutoa elimu kwa wananchi kuhusu umuhimu wa kujisajili katika vyeti vya kuzaliwa, vifo, ndoa na talaka. Utekelezaji wa Ofisi ya Mrajis wa Vizazi na Vifo ilianza kutekeleza ushauri huu kwa kufanya semina tatu za Masheha na semina moja kwa wakunga wa Mkoa wa Mjini Magharibi. Aidha, Ofisi iliendelea kutoa mafunzo kwa Masheha wapya walioteuliwa katika Mkoa huo.

Kwa mwaka wa fedha 2017/2018 Afisi imejipanga kutoa elimu kwa jamii kupitia vipindi viwili vya radio na viwili vya televisheni pamoja na marejeo ya vipindi hivyo na tayari vipindi hivyo vimeshaanza kutolewa.

Pili Kamati inashauri Ofisi ya Mrajis wa Vizazi na Vifo kuhakikisha vyeti vinapatikana kwa wakati unaotakiwa bila ya kuchelewa na hivyo wananchi kupata haki yao ya msingi kwa wakati.

Utekelezaji Ofisi ya Mrajis wa Vizazi na Vifo imeyafanyia kazi maoni na ushauri huo, kwa hivi sasa kwa kutumia mfumo wa usajili wa kielektroniki katika Mkoa wa Mjini Magharibi wananchi wanapewa muda wa wiki mbili kuja kuchukua vyeti vyao na wanapokuja vyeti hivyo vinakua vipo tayari. Kwa upande wa Wilayani, vyeti vinapatikana kwa wakati isipokuwa pale tu panapokuwa na uhaba wa magamba, na Afisi inajitahidi kadri ya uwezo wake kuhakikisha kuwa huduma zote zinapatikana na zinatolewa kwa wakati

Tatu Kamati inashauri kuwa utaratibu wa utoaji wa vitabu vya vyeti vya ndoa vilipiwe mwanzo na wahusika badala ya kuvirejesha wakati wanapomaliza kutumia.

Utekelezaji

Ofisi imeupokea ushauri huo ambapo kuanzia tarehe 01 Oktoba, 2017 vitabu vya vyeti vya ndoa vitaanza kulipiwa mwanzo na wahusika badala ya malipo hayo kufanyika wakati wa kurejesha vitabu kama ilivyokuwa hapo awali

Nne Kamati inashauri uongozi wa Mkoa kwa kushirikiana na taasisi husika wanasimamia migogoro yote ya ardhi na kusuluhishwa kwa mujibu wa taratibu na kuzingatia haki za wahusika.

Utekelezaji Mamlaka za Mikoa zinaendelea kudhibiti Migogoro ya ardhi isitokee katika maeneo yake. Hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kutoa taaluma kwa Masheha, Madiwani na watendaji kuhusu Sheria za Ardhi. Migogoro kadhaa ya ardhi imeendelea kutatuliwa katika ngazi za Wilaya na Mikoa na ile iliyoshindikana mashauri yake yamefikishwa katika vyombo vya sheria. Kwa upande wa Mkoa wa Kusini Unguja jumla ya migogoro tisa ya ardhi ikihusisha uvamizi, mipaka, na umiliki imeripotiwa na kupatiwa ufumbuzi. Kwa upande wa Mkoa wa Kusini Pemba Migogoro ya ardhi iliyojitokeza kwa kipindi cha mwaka ni 36, kati ya hiyo Wilaya ya Mkoani ni minne na Wilaya ya Chake Chake ni 32. Kwa upande wa Wilaya ya Mkoani yote imetatuliwa na Wilaya ya Chake Chake iliyotatuliwa ni mitano, inayoendelea kufatiliwa ni ishirini na tano na miwili imepelekwa katika vyombo vya sheria.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri kumradhi kidogo naomba kutoa kiti.

(Hapa Mhe. Mwenyekiti Mhe. Shehe Hamad Matar alikalia kiti)

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. Tano Kamati inashauri kuchukuliwa hatua zinazostahiki watu wanaolaza magari katika barabara zote za Mkoa wa Mjini Magharibi kuhakikisha wanakomesha vitendo vya udhalilishaji na ubakaji wa watoto na watu wenye ulemavu ili kutoa fursa sawa ya kuishi kwa amani.

Utekelezaji Katika kukabiliana na tatizo la kulaza magari barabarani Mkoa kwa kushirikiana na Manispaa ya Mjini inaendelea kuchukua hatua za kuziondosha gari zinazoegeshwa barabarani pamoja na kutafuta maeneo maalum ya kuziweka gari hizo, kwa sasa Baraza linaendelea na mazungumzo na wamiliki wa uwanja wa Alabama na Mlandege kwa ajili ya kuyatumia maeneo hayo kwa maegesho ya magari ili kupunguza magari kulala katika maeneo yasiyo husika. Aidha maeneo hayo yatakapokuwa rasmi yatawekewa ulinzi hali itakayopelekea kupungua vitendo vya udhalilishaji.

Sita. Kamati inaishauri Serikali ya Mkoa kuwa vituo vyote vya maegesho ya magari vilivyopo Mjini ni bora kubinafsishwa na Mamlaka husika kukusanya kodi kupitia kwa wamiliki wa *parking* hizo

Ukusanyaji wa mapato ya ada za maegesho ni moja kati ya vianzio muhimu vya mapato ya Baraza, hivyo kinachofanyika ni kuimarisha ukusanyaji huo ili kuongeza mapato. Hivi sasa Baraza limeshaandaa nyaraka za zabuni za kumpata mbia wa kushirikiana nae kufanya kazi ya ukusanyaji kwa kutumia mifumo ya kielektroniki ambayo itasaidia ufanisi wa ukusanyaji wa mapato kupitia chanzo hicho. Mapendekezo ya nyaraka hizo za zabuni tayari yameshawasilishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kwa kupatiwa ushauri wa kisheria.

Saba Kamati inaishauri Serikali kuharakisha ujenzi wa kituo kikuu cha daladala cha Kijangwani. Vile vile Kamati haikuridhishwa kuwepo kwa kituo cha daladala mbele ya Ofisi Kuu ya CCM Kisiwandui mpaka Tobo la Pili Michenzani, hivyo Kamati inashauri kuondolewa kwa kituo hicho.

Utekelezaji:

Kituo cha daladala Kisiwandui kilikuwa ni kituo cha muda ingawa muda huo umekuwa mrefu sasa. Baraza la Manispaa ya Mjini kwa kushirikiana na Mamlaka husika za Serikali linaandaa kituo kipya katika eneo la Kijangwani ambapo daladala zote ziliopo eneo la Kisiwandui CCM zimepangwa kufikia hapo. Baraza linaamini mpango huu utakapokamilika utaondosha usumbufu kwa madereva na waendao kwa miguu wanaopita eneo hilo la Kisiwandui. Kwa kufanya hivyo kituo cha Kisiwandui kitakuwa cha kushusha na kupakia tu na gari hazitoruhusiwa kusubiri abiria.

Nane. Kamati inashauri Serikali kuhakikisha suala la majengo ya Ofisi za Serikali linapatiwa ufumbuzi, ili kuepuka kukodi majengo kila siku kwa ajili ya Ofisi na kutumia pesa nyingi za Serikali kwa kulipa gharama za kodi hizo.

Ushauri umepokelewa na Ofisi imeanza na inaendelea kulifanyia kazi suala la kukodi majengo kwa Taasisi zilizo chini yetu kwa kadri ya hali inavyoruhusu. Kwa kuanzia Ofisi tayari imerejesha jengo lilikodiwa na kutumika kwa ajili ya Ofisi ya Afisa Mdhamini Tibirinzi na kuhamia katika jengo lake Machomanne, Sambamba na kurejesha Ofisi ya Baraza la Mji Wete iliyokodiwa na kuhamia katika Ofisi mpya iliyojengwa chini ya ufadhili wa Benki ya Dunia.

Tisa Kamati inashauri kudhibitiwa kwa maji taka katika barabara kuu inayoingia Uwanja wa Ndege wa Zanzibar ili kuweka mji safi na haiba nzuri hasa kwa wageni wanaoingia kila siku.

Utekelezaji:

Kazi za kusafisha misingi iliyopo inaendelea vizuri. Hata hivyo, tatizo la kutuwama maji ya mvua linasababishwa na udogo wa misingi yenyewe. Baraza la Manispaa Mjini kupitia programu ya *ZUSP* limepanga kujenga msingi wenye urefu wa kilomita 1.6 utakaopitisha maji machafu kutoka Uwanja wa Ndege kuelekea pwani kupitia Baraza la Wawakilishi. Gharama za ujenzi wa msingi huo ambazo zinazokadiriwa kufikia Shilingi bilioni 2.5 zinatarajia kuombwa katika progamu ya *ZUSP* awamu ya tatu

Kumi: Kamati inashauri uongozi wa Mkoa wa Mjini Magharibi kwa kushirikiana na vyombo vya ulinzi kuhakikisha kwamba suala la dawa za kulevya linapigwa vita kwa nguvu zote.

Utekelezaji:

Mkoa kwa kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama tayari umeanza kuchukua hatua mbalimbali ili kukabiliana na tatizo hilo, miongoni mwa hatua hizo ni pamoja na kuwataka vijana wanaotuhumiwa kujihusisha na madawa ya kulevya na vitendo vya kihalifu kujisalimisha ambapo vijana 220 tayari wamejisalimisha katika vituo vya Polisi. Pia, Mkoa umetoa taaluma kwa vijana 336 juu ya umuhimu wa kuwa raia wema.

Aidha, kesi 157 za watu wanaotuhumiwa kujihusisha na biashara haramu zikiwemo kesi 53 za unga, bangi 68 na shisha kesi 36 zimeanza kuchukuliwa hatua za kisheria. Mkoa pia umeanzisha kampeni ya ***MIMI NA WEWE*** inayowafahamisha vijana juu athari ya matumizi ya dawa za kulevya na kuwahamasisha kuachana nazo. Vijana 55 wamehamasika kuachana na matumizi ya dawa hizo kwa hiari na hivi sasa wapo *sober house* kwa kupatiwa huduma za matibabu.

Kumi na Moja: Mhe. Mwenyekiti, kutokana na athari ya Matukio ya kesi za udhalilishaji na ubakaji kamati ilishauri Serikali na Taasisi zinazohusika kusimamia sheria na kuchukua hatua kali katika kudhibiti tatizo hili ili iwe funzo kwa watendaji na wahalifu wengine wenye kufanya vitendo kama hivi.

Mhe. Spika, katika maeneo ambayo niliyasema kwamba tumeyaunganisha na kupunguza idadi vifungu ni pamoja na kifungu cha 11, 17,61,23,21,51,

mpaka 56 kwa hivyo naomba nisome kifungu cha ushauri ambao unafanana halafu uniruhusu Mwenyekiti, nisome utekelezaji wake na hususan wajumbe tayari kitabu hiki wanacho watajisomea wenyewe ule ushauri ambao tumepewa.

Utekelezaji.
Mikoa kwa kushirkikana na wahusika wengine wamefanya ufuatiliaji wa matukio ya kesi za udhalilishaji zilizoripotiwa, Mikoa pia imefanya uhamasishaji wa wananchi juu ya kuondoa ukimya na kutoa taarifa ya vitendo vya udhalilishaji vinavyotokea ikijumuisha kamati z Shehia, aidha kwa upande wa Mkoa wa Kaskazini Unguja kwa mwaka 2016, katia ya kesi 122 zilizoripotiwa 29 zipo Mahakamani, 70 zinaendelea na upelelezi 15 majalada yake yamefungwa na kesi 8 washitakiwa wake wametiwa hatiyani.

Katika kipindi cha Januari hadi Julai 2017 jumla ya kesi 136 zimeripotiwa kati ya hizo 23 zipo Mahakamani, 91 zinaendelea na upelelezi 19 majadala yake yamefungwa na kesi 3 washtakiwa wake wametiwa hatiani. Katika kudhibiti vitendo hivyo kamati 19 za kupinga udhalilishaji katika ngazi ya Shehiya zimeundwa na kupatiwa ufumbuzi ya namna ya kukabiliana na tatizo la udhalilishaji aidha Mkoa umefanikiwa kuwa na dawati la kijinsi la Mahonda kituo cha Mkono kwa mkono Kivunge na Mahakama ya Watoto Mahonda ambapo zinasaidia katika kuhakikisha suala la udhalilishaji yanapatiwa ufumbuzi na yanakomeshwa kabisa

Katika kipindi cha Januari hadi Disemba 2016 jumla ya kesi 101 za udhalilishaji zimeripotiwa. Kati ya kesi hizo 55 zimepatiwa ufumbuzi, kesi 27 zipo Mahakamani na kesi 19 zinaendelea na uchunguzi katika vituo vya Polisi. Aidha katika kipindi kilichoanzia Januari hadi Julai 2017, jumla ya kesi 41 zimeripotiwa. Kati ya kesi hizo 18 zimepatiwa ufumbuzi, 11 zipo Mahakamani na 12 zipo Polisi.
Vile vile Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa Serikali za Motaa na Idara Maalum za SMZ kwa kushirikiana na Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto imeandaa mkutano uliowajumuisha Makatibu Tawala wa Mikoa na Wilaya ili kuwapa maelekezo ya utekelezaji wa Mpango wa Kitaifa wa Kumaliza Udhalilishaji dhidi ya Wanawake na Watoto (2017-2022).

Katika utekelezaji wa mpango huo Mamlaka za Mikoa zimeagizwa kuunda kamati za kudhibiti udhalilishaji dhidi ya wanawake na watoto katika ngazi ya Wilaya na Shehia ambazo pamoja na mambo mengine kamati hizo zimepewa jukumu la kuratibu na kufuatilia masuala yote yanayohusu udhalilishaji ikiwa ni pamoja na kuongeza uwelewa na ufahamu wa masuala ya udhalilishaji kwa jamii na kuhakikisha kuwa kesi za

udhalilishaji zinaripotiwa na kushughulikiwa kwa mujibu wa sheria na muongozo uliopo kupitia vikao vya kila wiki.

Mhe. Mwenyekiti, Suala Nam. 12 Kamati ilishauri kuendelezwa kwa mabaraza ya vijana ili kuwawezesha vijana kupambana na mazingira yaliyowazunguka kifikra na kiuchumi ili kuachana na mawazo potofu ambayo ni kikwazo cha maendeleo.

Utekelezaji kwa kushirikiana na wahusika wengine Mabaraza ya Vijana yanaendelea kupatiwa elimu ya ujasiriamali, kuzifahamu fursa zilizowazunguka katika maeneo yao ili waweze kuzitumia vizuri kwa kuibua miradi pamoja na kuandaa Mipango Kazi na kusimamia utekelezaji wake. Mabaraza ya vijana yameanza kujishughulisha na uzalishaji baada ya kupatiwa elimu. Mabaraza hayo yameanza kufanya shughuli za ushoni, kilimo, uzalishaji wa sabuni, dawa za kusafishia vyoo, vigae, shampoo, mafuta ya mgando, siki, na shughuli za ufugaji.

Mhe. Mwenyekiti, Nam.13. Kamati ilishauri Mkoa wa Kusini kusimamia kikamilifu ongezeko la matumizi ya Bandari bubu ili kuziba mianya ya upotevu wa mapato ya rasilimali za Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, utekelezaji Mkoa unaendelea kufanya ufuatiliaji kwa kushirikiana na vyombo vya Ulinzi kudhibiti wanaojihusisha kutumia bandari bubu. Mkoa pia unatoa elimu katika maeneo yanayotumika kufanya biashara hiyo. Sambamba na juhudi za kuirasimisha bandari ya Kizimkazi Mkunguni ili kupunguza matumizi ya bandari bubu na kuongeza mapato zaidi serikalini yanayotokana na ushuru wa forodha, kodi ya mapato na tozo la ada kupitia harakati za kibiashara zitakazoongezeka. Aidha, Mkoa una jumla ya bandari bubu 17 ambazo zinaendelea kudhibitiwa ili kupunguza upotevu wa mapato.

Mkoa wa Kaskazini Unguja una bandari bubu 12. Hata hivyo, hakuna bidhaa za magendo zilizokamatwa katika kipindi cha Aprili-Juni 2017/18.

Kamati inashauri Mkoa wa Kusini Unguja kufanya tathmini na kujua idadi ya maeneo na majengo ya Ofisi za Serikali ambayo hayana hatimiliki na kuyatafutia kwa mujibu wa taratibu za Idara husika.

Mkoa tayari umeshaanza hatua za awali za ufuatiliaji wa majengo ambayo hayana Hati miliki na kuwasilisha katika sekta husika (Afya na Elimu) kwa ajili ya upatikanaji wa hatimiliki kwa kufuata utaratibu. Kati ya vituo 37 (3%) vya afya viliopo Wilaya ya Kati, kituo cha afya Tunguu pekee ndicho chenye hatimiliki. Aidha, kati ya skuli 81 ziliopo katika Mkoa, skuli 16 (20%) tu ndio zenye hatimiliki. Hata hivyo, skuli 8 zimeshapimwa kwa ajili ya kupatiwa hatimiliki.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, kati ya skuli 74 ziliopo, skuli 12 (16%) tu ndio zenye hatimiliki. Aidha, kati ya vituo 26 vya afya viliopo Mkoa wa Kaskazini, kituo 1 (4%) tu ndicho chenye hatimiliki. Mikoa itaendeleza juhudi za kuzipatia hatimiliki taasisi hizo mara tu baada ya kukabidhiwa kupitia mpango wa upelekaji wa madaraka kwa wananchi

(D by D).

Kamati inashauri juhudi za pamoja zifanyike kati ya wazazi, walimu na uongozi wa Mkoa kuinyanyua sekta ya elimu katika Mkoa huo

Mkoa kupitia Bodi za Elimu na Kamati za Skuli husika unaendelea kuelimisha jamii na kuzisimamia Kamati za Wazazi kutekeleza majukumu yake ili kuimarisha Sekta ya elimu. Aidha, walimu hutumia muda wa ziada kusomesha wanafunzi hususan wale waliokabiliwa na mitihani. Uongozi wa Mkoa unafanya mikutano na walimu wakuu kwa lengo la kuhakikisha wanasimamia ipasavyo majukumu yao.

Mhe. Mwenyekiti, katika kusimamia ukosefu wa takwimu na data sahihi za wageni walioingia katika Mkoa huu, Kamati inashauri uongozi wa Mkoa wa Kaskazini Unguja kupitia ofisi yake inayoshughulikia Utalii kutafuta na kuwekwa takwimu halisi za watalii wote wanaoingia katika Mkoa huu ili kudhibiti upotevu wa mapato ya Serikali.

Kamisheni ya Utalii Zanzibar imeanza kuandaa Mfumo wa Kidijitali *(Online Registration)* ambao utawezesha kufahamu wageni wanaoingia katika kila mkoa. Mfumo huo unalenga kuwa na takwimu sahihi za Watalii wanaoingia Nchini. Nimatumaini yangu kwamba mpoango huu utakapokamilika basi suala hili litaweza kutatuka.

Aidha Kamati inashauri kusimamia vyema suala la maendeleo ya Elimu katika Mkoa huu kwa kupatiwa vifaa vya kujifunzia pamoja na kupatiwa walimu wa kutosha katika masomo ya sayansi na hisabati.

Mhe. Mwenyekiti, Uongozi wa Mkoa kwa kushirikiana na kamati za wazazi za skuli, madiwani, baraza la elimu, Waheshimiwa Wabunge na Wawakilishi na Asasi zisizokuwa za Serikali umeendelea kutoa vifaa vya kujifunzia wanafunzi pamoja na kuwapatia mafunzo walimu wa sayansi na hesabati katika Vituo vya Walimu (TCs) vilivyopo ndani ya Mkoa. Aidha, ufuatiliaji wa uajiri wa walimu wapya hasa katika masomo ya sayansi na hisabati umefanyika na Walimu wanaendelea kuajiriwa na Wizara husika ili kuziba pengo la walimu 95 wanaohitajika katika Mkoa huwo.

Kamati ilishauri Serikali na Wizara kufanya jitihada za makusudi katika kuhakikisha kuwa imewapatia vitendea kazi watendaji wa Mkoa huwo ili kuweza kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ imekuwa ikitoa maagizo mara kwa mara kwa Mamlaka za Mikoa na Serikali za Mitaa kuweka vipaumbele vya mahitaji katika mipango na bajeti zao ikiwemo suala la ununuzi wa vitendea kazi vya Mamlaka hizo. Hata hivyo, Ofisi yetu itaendelea kuzihimiza Mamlaka hizo juu ya umuhimu wa kuwa na vitendea kazi vya kutosha kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yao.

Kamati ilishauri Serikali ijiangalie na kujitathmini kama kuongezeka kwa shughuli za starehe kuna faida kwa wananchi wa Mkoa wa Kaskazini.

Mhe. Mwenyekiti, Serikali ya Mkoa wa Kaskazini Unguja imepiga marufuku kufanyika kwa baadhi ya shughuli za starehe ikiwemo ya *"Full Moon Party"* inayokwenda kinyume na maadili ya Wazanzibari. Hata hivyo juhudi hizo za Mkoa zinahitaji kuungwa mkono na Taasisi nyengine ili ziweze kukamilika hususan Wajumbe wa Baraza lako tukufu Mhe. Mwenyekiti.

Kamati ilishauri Serikali ya Mkoa kuzingatia mahitaji ya msingi kwa watu wenye ulemavu wakati inapotoa misaada ya kijamii na kiuchumi.

Ushauri umepokelewa. Kwa kuanzia Mkoa umetoa fomu kwa Masheha wote ili kukusanya taarifa za mahitaji ya watu wenye ulemavu katika maeneo yote ya Mkoa ili kupata takwimu sahihi za mahitaji.

Kamati ilishauri serikali kukomesha vitendo vya baadhi ya wananchi wenye tabia ya kuharibu mazao ya wakulima kutokana na chuki za kisiasa.

Ushauri umepokelewa, Ofisi za Mikoa hasa Kusini na Kaskazini Pemba zitaongeza juhudi za kuwaelimisha wananchi kuachana na hujuma hizo na kuchukua hatua kali kwa wanaohusika na hujuma hizo.

Kamati ilishauri kwa Wakuu wa Mabaraza ya Miji Pemba kuajiri kwa muda wataalamu kwa mikataba kwa mujibu wa mahitaji yao yalivyo kama wanavyofanya Unguja.

Ushauri unapokelewa na utatekelezwa kwa kuwa Sheria na taratibu zinaruhusu Mamlaka za Serikali za Mitaa kuajiri wataalamu kwa mikataba.

Mhe. Mwenyekiti, suala hili limeungana na suala Nam. 30, 38, 43, na 92.

Kamati inashauri Uongozi wa Mkoa kusimamia Mabaraza katika kutumia vyema fedha za maendeleo pamoja na zile za mfuko wa Jimbo kwa kushirikiana na Wabunge na Madiwani. Nalo suala hili linaungana na suala Nam.40, 59.

Utekelezaji Mkoa unaendelea kuyasisitiza Mabaraza kuzingatia Sheria, kanuni na miongozo ya usimamizi ya matumizi ya fedha za umma. Aidha, Mabaraza yamesisitizwa kuzitumia Kamati za Mifuko ya Majimbo kufanyakazi kwa uwazi na uadilifu.

27. Kamati imeshauri Serikali ya Mkoa kwa kushirikiana na Baraza la Mji Chake Chake kuajiri Muhandisi wa Ujenzi kutokana na Miradi mikubwa ya ujenzi inayofanyika katika Mkoa huo. Suala hilo pia linaungana na suala 41.

Utekelezaji Ushauri umepokelewa na kwa sasa usaili tayari umefanyika na hatua za ajira zinaendelea.

28. Kamati imeona kuwa Mabaraza ya Miji Pemba yameshindwa kukusanya kodi zake vizuri kutokana na kutozishirikisha Mahakama, hivyo wafanya biashara kupata fursa ya kukwepa kulipa kodi, Kamati inashauri pawepo mashirikiano mazuri baina ya Mabaraza na Mahakama ili kuhamasisha na kuongeza upatikanaji wa kodi.

Mabaraza ya Miji yamechukua hatua ya kuzungumza na uongozi wa Mahakama ili kujua changamoto zinazoikabili Taasisi hio na kuzichukulia hatua ya utatuzi na mabadiliko yameanza kuonekana, kwa upande wa Baraza la Mji Mkoani jumla ya kesi 62 zimeshughulikiwa na kupatiwa ufumbuzi wake.

29. Kamati inashauri uongozi wa Manispaa kwa kushirikiana na uongozi wa *ZECO* kukaa pamoja na kutafuta njia sahihi ya kulipatia ufumbuzi suala liliopo katika Baraza la Mji la deni la umeme.

Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ imeamua kukutana na Wizara ya Fedha na Mipango kuangalia uwezekano wa deni hilo kufutwa au kulipwa na Serikali kwa kuwa deni hilo limekuwa ni mzigo mkubwa kwa Baraza la Manispaa Mjini kuweza kulilipa. Hivi sasa Baraza la Manispaa linakatwa asilimia hamsini kulipia deni kila linapofanya manunuzi ya umeme.

Napenda niliarifu Baraza la Wawakilishi kwamba tayari suala hili limechukuliwa na serikali na hasa kwa sababu serikali kuu inawalipia deni Shirika la Umeme *ZECO* kule *TANESCO* kwa hivyo deni hili litachukuliwa katika zile Fedha ambazo serikali tunawalipia deni Shirika la Umeme *ZECO*.

31. Kamati ilishauri kuboreshwa kwa maslahi ya wafanyakazi wa Mabaraza ya Manispaa, hii itaongeza ari na hamasa katika kukamilisha majukumu ya watumishi.

Baraza la Manispaa ya Mjini linaendelea na mpango wake wa kuwapa motisha wafanyakazi wake kila wanapovuka malengo yaliyowekwa kulingana na uwezo uliopo kifedha. Kwa kawaida Baraza la Manispaa ya Mjini huwa linatoa motisha ya shilingi 50,000 kwa kila mfanyakazi alieko katika kitengo cha ukusanyaji wa mapato. Kwa mfano mwaka wa fedha 2016/2017 wafanyakazi wa Idara ya leseni walipatiwa motisha hiyo baada ya kuvuka lengo la ukusanyaji wa mapato.

33. Kamati ilishauri kuimarishwa kwa vitendea kazi ili kujenga mazingira bora ya kazi pamoja na kuongeza ufanisi na ubora wa kiutendaji.

Kupitia bajeti za kila mwaka Mabaraza ya Manispaa yamendelea kufanya manunuzi ya vifaa mbalimbali kama vile kompyuta, vyombo vya usafiri na samani ili kujenga mazingira mazuri ya kazi katika Mamlaka hizo.

34. Kamati ilishauri Baraza la Manispaa ya Magharibi “A” kulisimamia eneo la ujenzi wa Hospital ya Mbuzini kwa kulipatia Hatimiliki na kulitafutia wafadhili kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha Afya.

Ufuatiliaji wa hatimiliki wa eneo hili utaanza baada ya makabidhiano ya rasilimali baina Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ na Wizara ya Afya kupitia utekelezaji wa Ugatuzi wa Madaraka.

35. Kamati ilishauri Serikali kuu kuzisaidia Manispaa hizi katika ujenzi wa barabara za ndani kwa sababu Manispaa hizo ni mpya na changa kiuchumi.

Ushauri umepokelewa na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ itakaa pamoja na Wizara ya Fedha na Mipango kuangalia uwezekano wa kupatiwa fedha katika mwaka 2018/19 Mabaraza ya Manispaa ya Magharibi "A" na "B" ili yaweze kukidhi gharama za matengenezo ya barabara za ndani. Maelezo haya pia yamezingatia ushauri uliotolewa wa kuzifanyia matengenezo barabara zinazoingia katika kambi za Idara Maalum za SMZ.

32. Kamati inashauri katika kusimamia suala zima la ukusanyaji wa mapato na fursa za kiuchumi ni bora kusimamia vyema kwa Manispaa ya Magharibi "A" na Magharibi "B" ili kuziba mianya ya upotevu wa mapato. Suala hili pia linaungana na suala Nam. 36 na suala Nam. 41.

Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ imekuwa ikiwasiliana na viongozi wa Mabaraza mara kwa mara kujadili mikakati ya kuimarisha ukusanyaji wa mapato, miongoni mwa mikakati hiyo ni kuanzisha "data base" ya vyanzo vya mapato na kuhifadhi taarifa za wafanyabiashara wa ngazi mbalimbali pia kuhakikisha elimu inatolewa kwa watendaji na wafanyabiashara. Aidha, Ofisi imechapisha kanuni za Mamlaka za Serikali za Mitaa zinazohusiana na utoaji wa huduma na ada za uchangiaji wa huduma kwa kila aina ya biashara.

37. Kamati inashauri Serikali iwe na utaratibu wa kuwapima wakusanyaji wa mapato uwezo wao wa kukusanya mapato na iwapo watagundulika wameshindwa kukusanya mapato basi waondolewe katika maeneo yao ya kazi. Suala hili pia linaunga na suala Nam. 57.

Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ imeziagiza Mamlaka za Serikali za Mitaa kufanya tathmini ya ukusanyaji wa mapato kwa kuangalia viwango vinavyokusanywa na Maafisa husika. Mamlaka zimetakiwa kuchukua hatua stahiki kwa walioshindwa kufikia malengo waliopangiwa na kuwachukulia hatua stahiki.

57. Kamati ilishauri uongozi wa Halmashauri kukaa pamoja na wamiliki wa jumuiya zote zinazojihusisha na ukusanyaji wa kodi ili kujadili mustakbali mzima wa ukusanyaji wa mapato katika Halmashauri**.**

Ushauri umechukuliwa na hatua za awali za kukutana na Taasisi zinazojihusisha na ukusanyaji wa kodi zinaendelea kufanyika.

39. Kamati imeshauri Baraza kulitumia vizuri soko jipya la Wete katika ukusanyaji wa mapato, aidha, kamati inapendekeza kujengwa uzio wa kutenganisha baina ya Ofisi na soko ili kuondoa msongamano kwa watumiaji wa soko hilo.

Ushauri umepokelewa unaendela kufanyiwa kazi kwa kushauriana na wahusika wengine.

45. Kamati inashauri Baraza la Mji Mkoani kujiwekea Sheria na kanuni ndogo ndogo katika kukabiliana na changamoto ndogo ndogo ndani ya Mamlaka zao.

Ushauri huu umeanza kufanyiwa kazi kwa kupitia kanuni mpya ili kuangalia maeneo ambayo Baraza linahitaji kuweka kanuni ndogo ndogo yaani *(By-laws).*

Agizo namba 46
Kamati inashauri Ofisi ya Mkuu wa Wilaya kwa kutumia Kamati yake ya Ulinzi na Usalama kuhakikisha askari jamii wote kabla ya kupewa majukumu, wapewe elimu ya kutosha juu ya majukumu yao kwa raia na viongozi pamoja na wageni wanaoingia, ili kuepuka migogoro isiyo ya lazima.

Ushauri kuhusu askari jamii umepokelewa na unafanyiwa kazi, kuhusu askari jamii wa Mji Mkongwe waliongia Mkataba na Baraza la Manispaa la Mjini hautaendelea tena kufikia mwishoni mwa mwezi wa Septemba 2017 baada ya malalamiko mengi kutoka kwa wananchi na Waheshimiwa Wawakilishi wa Baraza hili.

Napenda niwaahidi kwamba kuanzia tarehe mosi mwezi wa Oktoba tumeachana Askari Jamii wa mji Mkongwe kufanya kazi za Baraza la Manispaa.

Agizo namba 47
Aidha, katika kuboresha utoaji wa msaada wa fedha za wazee, kamati inashauri kuwekwa kwa *Data Base System* ambayo itahitaji taarifa za wazee wa Wilaya nzima ya Mjini hivyo, kuepusha kujirudia kwa majina ya wazee waliokwisha sajiliwa.

Utekelezaji
Katika kuimarisha utoaji wa msaada wa fedha za wazee, Wilaya imeanza utaratibu wa kuwapatia kompyuta na mafunzo ya usimamizi wa Takwimu maafisa wa ustawi wa jamii na kuwekewa mfumo mpya wa ki *electronic*.

Agizo namba *48*
Kamati inashauri wazee ambao wanapewa pesa za wazee ambao hawajastahiki kupewa na kutakiwa kuzirejesha fedha hizo, ni vyema wakaachiwa na adhabu hiyo ya kurejesha fedha wakapewa waliohusika kuwasajili wazee hao bila ya kuzingatia sifa.

Utekelezaji
Ushauri umepokelewa na utafanyiwa kazi kwa nguvu zote.

Agizo namba 49
Kamati inashauri uongozi wa Ofisi kusimamia vyema vitendo vya uhalifu vinavyojitokeza siku hadi siku katika kulinda amani kwa wananchi na mali zao.

Utekelezaji
Katika kuhakikisha hali ya ulinzi na usalama unaimarika Mkoa kwa kushirikiana na kamati zake za ulinzi na usalama imechukua hatua za kusimamia utaratibu wa kudhibiti muda wa kuanza na kumaliza burudani za muziki katika kumbi za starehe, kusimamia

utaratibu wa uuzaji na matumizi ya vileo na kufanya operesheni za kushtukiza katika kumbi za starehe na nyumba za kulaza wageni.

Agizo namba 50
Kamati imeshauri Ofisi ya Wilaya ya Magharibi "A" kuwaita Masheha na kuwataka wafanye uchunguzi dhidi ya watoto wenye ulemavu ambao hawapati mahitaji yao ya msingi katika familia zao kama vile elimu na matibabu ili kuweza kusaidia kwa mujibu wa uwezo uliopo.

Utekelezaji
Wilaya imeorodhesha watoto wenye ulemavu katika kila Shehia na wale wanaoishi katika mazingira magumu kwa lengo la kuwatambua pamoja na kuwapatia misaada ya kielimu na kimatibabu pale inapohitajika. Vile vile, Wilaya imehamasisha wazazi na walezi wa watoto wenye ulemavu kuwafichua na kuwawezesha kupata elimu na mahitaji mengine ya msingi ya kijamii.

Agizo namba 52
Kamati inashauri uongozi wa Wilaya kuwahamasisha Masheha wao kutojiingiza katika migogoro ya Ardhi na ikitokea kesi hizo katika Ofisi zao basi ni vyema kuelekeza katika taasisi zinazohusika na utatuzi wa migogoro ya Ardhi.

Utekelezaji
Wilaya imechukua hatua ya kuwaelimisha Masheha na kuwatahadharisha juu ya kushiriki katika migogoro ya ardhi na kuzipeleka kesi hizo katika Taasisi husika za kisekta na Taasisi za kisheria.

Agizo namba 53
Kamati inashauri Uongozi wa Wilaya kuhakikisha wamesimamia vya kutosha suala la upatikanaji wa hatimiliki za maeneo wanayoyamiliki pamoja na majengo ya Ofisi wanayoyatumia.

Utekelezaji
Wilaya inaendelea kufuatilia na kushauriana na Taasisi husika kuyapatia hatimiliki maeneo yote ya Taasisi zetu ingawa kumekuwa na tatizo la ucheleweshaji wa upatikanaji wa hati miliki hizo.

Agizo namba 54
Kamati inashauri Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ pamoja na Wizara ya Afya kulipatia ufumbuzi suala la uwekaji wa kitengo cha madawa cha DHMT kufanya utaratibu wa kukihamisha ndani ya Ofisi ya Mkuu wa Wilaya na badala yake kitafutiwe sehemu inayostahiki.

Utekelezaji
Ofisi ya Rais, Tawala Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum, Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Magharibi "B" na Baraza la Manispaa Magharibi "B" zinaendelea na matayarisho ya kukihamisha Kitengo cha Madawa cha DHMT kama ilivyoshauriwa na madawa yake kuyahamishia katika eneo la Mkemia Mkuu wa SMZ.

Agizo namba 55
Kamati inashauri kuongezewa na kupatikana kwa wakati Bajeti ya Ofisi ya Wilaya ya Magharibi "B" ili kuweza kutatua matatizo mbalimbali yanayowakwaza ikiwemo ufinyu wa Ofisi.

Utekelezaji
Mkoa unaendelea na jitihada kwa kushirikiana na Taasisi mbalimbali ili kuweza kutatua tatizo linalowakwaza Wilaya ya Magharibi "B" na kuweza kuondoa ufinyu wa ofisi. Aidha hatua zinazoendelea za kuihamisha Ofisi ya Timu ya Afya ya Wilaya (DHMT) kwenda katika Ofisi ya Baraza la Manispaa ya Magharibi "B" zinalenga kuiwezesha Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Magharibi "B" kuwa na nafasi zaidi za matumizi ya Ofisi.
60. Kamati ilishauri watendaji wa Halmashauri wanaohusika na usimamizi wa afya kupitia nyumba hadi nyumba katika kusimamia na kuhakikisha usafi katika suala zima la afya na kuhamasisha wazazi kupeleka watoto wao kupatiwa chanjo mbalimbali za kujikinga na magonjwa hatari.

Tayari Afisi za Halmashauri zinawatumia Maofisa wa Afya katika kuhamasisha usafi na kuwahamasisha wazazi kuwapeleka watoto wao katika vituo vya Afya kwa ajili ya kuwapatia chanjo pamoja na suala la uhamasishaji wa Nyumba kwa nyumba. Kazi hii sasa imepata nguvu zaidi baada ya kuanza kutekelezwa kwa Sera ya Ugatuzi wa Madaraka.

Swali namba 62. Kamati inashauri viongozi wa Halmashauri kusimamia vyema ukusanyaji wa mapato na kuhakikisha kuwa hakuna mianya ya kupotea kwa mapato hayo.

Utekelezaji
Halmashauri zipo katika kujiimarisha zaidi katika masuala ya ukusanyaji mapato kwa kuwa na 'database' na kufika katika hatua ya ukusanyaji kwa njia ya ki-elektroniki ili kuziba kabisa mianya ya kupotea kwa mapato. Aidha, baadhi ya malipo kwa sasa yanalipwa kupitia Benki.

Vile vile Halmashuri zimefanya mabadiliko kwa wafanyakazi katika maeneo yao ya kazi hasa ukizingatia baadhi yao wamekaa eneo moja muda mrefu sana.

Aidha, utaratibu wa kuwalipa Wafanyakazi kwa baadhi ya maeneo kwa kuangalia asilimia ya kila anacho kikusanya, haya ni maeneo ambayo yanategemea utendaji kazi na uaminifu kwa mkusanyaji mapato. Pia baadhi ya Wafanyakazi wanaoshindwa kwenda na mageuzi ya uimarishaji wa mapato kuacha kazi kwa hiari yao. Katika kipindi cha July-Septemba, 2017 tayari wafanyakazi watatu wameacha kazi kwa hiari yao kwa sababu hawaendani na kasi ambayo tunaitegemea iwepo.

Swali namba 64. Kamati ilishauri Serikali katika kupigania majengo na makaazi mazuri, *Uniform* za askari wake pamoja na mambo mengine, basi isiwaachie vikosi pekee yake katika kuzishughulikia changamoto hizi.

Suala hili namba 66 linaungana na suala namba 66 mpaka 76.

Utekeezaji
Katika kushughulikia suala hili majengo na makaazi kwa Idara Maalum, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaaa na Idara Maalum za SMZ kwa kushirikiana na Tume ya Mipango imeanza kuwapatia fedha Vikosi vya Mafunzo na KMKM kwa mwaka wa fedha 2017-2018 kwa matengenezo ya majengo na makaazi kwa Maafisa na Wapiganaji. Kwa upande wa sare Serikali imeendelea kuwalipia sare askari wake kutoka bajeti ya Wizara. Kwa mwaka wa fedha 2017-2018 Ofisi ina mpango wa kuviimarisha Viwanda vya Ushoni kwa kuvipatia vifaa vya kisasa vya ushoni na fedha za ununuzi wa vitambaa kwa ajili ya ushoni wa sare hizo.

Kwa upande wa suala la sare kwa Idara Maalum tayari limeshapatiwa '*Invoice'* kutoka kampuni ya 'Exim' ya China, India na kupelekwa Wizara ya Fedha na Mipango kwa ajili ya malipo sambamba na ununuzi wa mashine za kiwanda cha ushoni cha Vikosi SMZ na Kiwanda cha Viatu cha Valantia. Shughuli za ujenzi wa kiwanda kipya cha viatu unaendelea pale KVZ.
Swali namba 65. Kamati inashauri katika uandaaji wa Bajeti ya Idara Maalum, wakuu wote wa Vikosi vilivyopo Pemba washirikishwe katika maandalizi ya Bajeti zao pamoja na wahasibu wao kule Pemba suala hili lina ungana na swali namba 77, 78, 83 na 85 na utekelezaji uko kama hivi ifuatavyo.

Kuanzia Bajeti ya mwaka 2017/18, Kamandi zote kupitia Wakuu wa Kamandi zimeshirikishwa kikamilifu katika hatua zote za maandalizi ya Bajeti ambayo yatazingatia vipaumbele ya mahitaji ya Idara Maalum husika.

Swali namba 67.

Mhe. Mwenyekiti:

UTARATIBU

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti inaonyesha kwenye makabrasha yetu kuna baadhi taarifa humu hazimo sababu tumejaribu kufatilia majibu ya Mhe. Waziri naona kuna mpaka namba 62 sasa yeye kishafika 66 au sijui labda kuna namba nyengine hizi ambazo ziko kati kati nilikuwa najaribu kufuatilia ili tupate kwenda sambamba na majibu ya Mhe. Waziri. Sasa kidogo nilikuwa naomba tupate ufafanuzi ili tuende sambamba kwa sababu huku kuna nambari ambazo ziko pembeni za maswali halafu kwenye majibu kuna nambari nyengine vile vile kwenye maoni na ushauri, sasa Mhe. naomba utuongeza kwa sababu wewe ndio uliotupa hayo makabrasha.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Mjumbe, Mhe. Waziri toa ufafanuzi utaratibu mzima wa hili kabrasha naona hajaopata kuelewa lakini uko vizuri mueleze vizuri yeye anangalia kwengine.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti mwanzo nilipokuwa nikianza na utangulizi wangu nilisema tulipokea hoja 95 lakini hoja nyingi zilikuwa zinajirejea rejea kwa hiyo jibu lake

linakuwa ni lile moja pamoja na kwamba ni hoja nyingi, kwa hiyo hoja hizi tutaziweka katika jibu moja na nikatoa mfano kwa mfano hoja kadhaaa na hoja kadhaaa na hoja kadhaaa jibu lake ni hilo hilo hata ukiamua kuchukuwa muda kulijibu bado linabakia kuwa jibu ni lile lile na ndio maana utakutia kifungu kwa mfano cha 63 ambapo ndipo ambapo tulikuwa tumefika nadhani ndicho 67 au 63 utakutia jibu lake limeunganisha 64, 66 na 76 kwa hiyo hata ukienda utakikuta kile kifungu kimeandikwa lakini jibu lake linakuwa lile na nilomba ridhaa ya Mhe. Spika na Mhe. Spika nadhani aliniruhusu nifanye hivyo.

Kwa hiyo nadhani Mheshimiwa angalie yale maswali na ushauri na majibu ambayo nimeyatoa mengi yalikuwa yanafanana na ndio maana nikasema tutatoka kwenye 95 mpaka vifungu 62 ambavyo tumeviwekea majibu na vile vifungu ambavyo majibu yake hayakuja moja kwa moja yatakuwa yanaungana na lile jibu la kile kifungu kimoja, ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe nadhani tumelielewa

Mhe. Hamza Hassan Juma: Sawa tuendelee

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri endelea.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:
Kifungu namba 67 kinaungana na kifungu namba 82, 93, Kamati ilishauri Serikali kuandaa Bima ya Afya kwa wafanyakazi wote wa Idara Maalum kuwajengea mazingira mazuri ya utendaji wao. Aidha, Kamati inaitaka Serikali kuanzisha mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa upande wa Idara Maalum za SMZ kwa kuangalia utaratibu wa vikosi vya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Swali namba 83 na 84 kama nilivyosema yanaungana lakini yameuliza tofauti tofauati jibu lake

Utekelezaji
Serikali inalizungumza suala hili na liko katika ngazi ya wataalamu linashughulikiwa ambapo likikamilika Serikali itatoa taarifa rasmi ya utekelezaji wa jambo hilo.

Kuhusu swali la ZSSF na Idara Maalum za SMZ zimeunda kamati maalum ili kutafuta uwezekano wa kuwaunganisha watumishi wa Idara Maalum za SMZ katika ZSSF

Swali namba 68 linaungana na swali namba 72, 80 na 94 swali lilisema Kamati inashauri Ofisi kufuatilia maeneo yote ya kambi za Idara Maalum na kusimamia upatikanaji wa Hatimiliki za maeneo hayo hususan kwa upande wa Pemba.

Utekelezaji
Vikosi vyote vya SMZ vinaendelea na hatua ya kuyapima maeneo yao ya kambi Unguja na Pemba ili yaweze kupatiwa hatimiliki zikiwemo Kamandi za Pemba.

Kwa upande wa Chuo cha Mafunzo kina jumla ya kambi 10 na hadi sasa tayari kimeshayapima maeneo yake 3 ambayo ni Hanyegwa Mchana, Langoni na Kinumoshi hadi sasa utaratibu wa kuzipatia hatimiliki Kambi hizo unaendelea. Maeneo yaliyobakia ambayo hayajapimwa ni Makao Makuu, Ubago na Bumbwini kwa upande wa Unguja kwa upande wa Pemba kazi ya upimaji kwa kambi ya Tungamaa imeshafanyika na fedha kwa ajili ya upimaji wa kambi zilizobakia zipo. Kengeja, Kangagani, na Wete zimeshatengwa na upimaji wake utafanyika mwaka wa fedha 2017/2018.

Maeneo yote 11 ya kambi za KVZ Unguja na Pemba yameshapimwa na gharama za hatimiliki zimeshalipiwa, eneo la Mtoni kwa Unguja limeshapatiwa hatimiliki na eneo la Pujini kwa Pemba limeshapatiwa hatimiliki na maeneo yaliyobaki utaratibu wa upatikanaji wa hatimiliki unaendelea.

Kwa upande wa Kikosi cha KMKM maeneo sita ya vituo yameshapimwa ambapo hatua za upatikanaji wa hatimiliki zinaendelea. Kwa Kambi za KMKM Tundaua na Fundo utaratibu wa upimaji unashugulikiwa.

Kwa upande wa KZU Kikosi cha Zima moto na Uwokozi maeneo 3 yameshapatiwa hatimiliki. Maeneo hayo ni Kijichame kwa upande wa Pemba na Tunguu na Mchangamle kwa upande wa Unguja.

Kwa upande wa JKU kambi zilizo na hatimiliki ni JKU Kama, Skuli za ufundi na Sekondari Mtoni, JKU Furniture A na B na JKU Makao Makuu Saateni. Kambi zilizopimwa ambazo bado hazijapatiwa hatimiliki na zinaendelea na utaratibu wa kupatiwa hati hizo ni Upenja, Bambi Kim, Bambi Matola, Cheju, Dunga Chokaa, Dunga Chuoni, JKU Msaani, Kwapweza, Pujini, Chambani, JKU Muambe, Gombani, Ngezi na JKU Chokocho.

Swali namba 69 kama nilivyosema kwa*wa vile* Serikali imeamua kuanzisha tena utaratibu wa vijana kujenga taifa. Hivyo, Kamati inashauri Serikali kuwapatia Jeshi la kujenga Uchumi vijana wakutosha ili kuweza kuzalisha mali kwa kiwango kizuri.

Utekelezaji
Jeshi la kujenga Uchumi tayari limeshaanza kuchukua vijana wa kujenga taifa kwa lengo la kuongeza kiwango kikubwa cha uzalishaji. Takriban vijana wapatao 2,000 wanatarajiwa kuwepo makambini ifikapo January, 2018. Kati ya hao 500 watakuwepo kwenye Kambi za Pemba na 1,700 Unguja.

Kupitia vijana hao uzalishaji wa mazao unatarajiwa kuongezeka kwa wastani wa tani 10 kwa mwaka. Pia uzalishaji wa matunda na mbogamboga unatarajiwa kuongezeka kwa tani 7 kwa mwaka. Suala Nam.70, kamati inashauri ipo haja ya kuwa na vituo vya afya katika kambi zote za Unguja na Pemba ambazo pia hutumiwa na wananchi walio karibu na maeneo ya kambi hizo. Suala Nam.70 na 71 linalingana.

Utekelezaji

Ushauri umepokelewa kwa kipindi hiki Idara Maalum za SMZ zina vituo vya afya 25 ambavyo vinatoa huduma kwa wapiganaji na raia walio karibu na maeneo ya kambi kwa Unguja na Pemba. Kwa sasa KMKM ina jumla ya vituo 6; Unguja 4 na Pemba 2, Chuo cha Mafunzo ina vituo 4; Unguja 3 na Pemba 1, KVZ ina vituo 5; Unguja 4 na Pemba 1, JKU ina jumla ya vituo 10; Unguja 7 na Pemba 3. Hata hivyo, uwezo wa kifedha utakaporuhusu tunatarajia kujenga vituo vya afya zaidi hasa kwa kambi za Pemba. Ushauri umepoekelewa hasa kwa upande wa Pemba na suala hili limefanyiwa kazi kwa kuvipatia vifaa vya mawasiliano… Samahani suala Nam.71 linajitegemea. Kamati inashauri KMKM Pemba kuimarishwa mawasiliano katika kukabiliana na wahujumu wa uchumi katika njia za baharini.

Utekelezaji

Ushauri umepokelewa na suala hili limefanyiwa kazi kwa kuvipatia vifaa vya mawasiliano vituo vyote vya Unguja na Pemba. Serikali itaendelea kuimarisha mawasiliano kadri ya hali ya fedha itakavyoruhusu.

Suala Nam. 73. Kamati inashauri serikali kununua… Mhe. Mwenyekiti, naomba suala hili naomba Wajumbe wa Baraza wanivumilie nisilisome, nawaomba wajumbe wakitizame kifungu Nam.73 niwaombe nisikisome wakijue wao tu. Naomba sana Mhe. Mwenyekiti, nadhani wajumbe wameniridhia…

Mhe. Mwenyekiti: Umeridhiwa endelea.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Kifungu Nam.74, kamati ilishauri katika kuimarisha shughuli za kilimo, Kikosi cha JKU kiweke mikakati madhubuti ya kupata maji ili kujikita katika kilimo cha umwagiliaji badala ya kusubiri msimu wa mvua. Aidha, kwa yale mashamba yaliyochoka ni vyema kupumzishwa ili kuyapa nafasi ya kujirudia au kubadilisha aina ya kilimo.

Utekelezaji

Jeshi la Kujenga Uchumi katika bajeti ya 2017/2018 ilipanga kuchimba visima viwili vyenye thamani ya shilingi milioni 40 katika Kambi ya Bambi Matora. Visima hivyo vinatarajiwa kumwagilia ekari 20 zilizotengwa katika kambi hiyo kwa bajeti ya mwakani idara imepanga kuweka mfumo wa umwagiliaji katika kambi ya Kwapweza na Msaani kwa upande wa Pemba. Aidha, kwa yale mashamba yaliyochoka upo utaratibu wakubadilisha mazao ya kilimo kulingana na msimu. Mfano, baada ya kilimo cha mpunga kumaliza kuvunwa kinachofatia ni kilimo cha kunde ili kuweka rutba katika ardhi inayolimwa na Jeshi la Kujenga Uchumi.
Kifungu Nam.75 Kamati pia inashauri Jeshi la Kujenga Uchumi kuwapatia zaidi askari wake utaalamu wa kilimo baada ya kutegemea askari wachache ambao muda wao wa kustaafu umekaribia.

Utekelezaji

Jeshi la Kujenga Uchumi limejipanga kuwapatia zaidi askari wake utaalamu wa kilimo kupitia mafunzo mbalimbali kutoka JKT na taasisi nyengine za mafunzo ya kilimo kikiwemo Chuo cha Sokoine, Tengeru na Chuo cha Kilimo Kizimbani kwa ngazi ya Cheti, Stashahada na Shahada katika fani ya kilimo. Kwa sasa tayari maafisa na askari wapatao 12 wameshapatiwa mafunzo ya muda mrefu na askari 16 wanapatiwa mafunzo ya muda mfupi kutoka JKT.

Kifungu cha 79, kamati ilielezwa kuwa baadhi ya Taasisi za Serikali zinadaiwa na Idara ya Chuo cha Mafunzo, hivyo kamati inashauri madeni hayo yalipwe na wizara isimamie kuhakikisha madeni yamelipwa kama mikataba yao inavyoelekeza.

Utekelezaji
Hatua za kufuatilia madeni mbalimbali inayodai Chuo cha Mafunzo kwa taasisi mbalimbali zimeanza kuchukuliwa na hadi hivi sasa kati ya fedha hizo shilingi 109,000,000 inazodai Chuo cha Mafunzo shilingi 5,000,000 zimeshalipwa sawa na asilimia 5% na shilingi 104,000,000 sawa na asilimia 95% hazijalipwa.

Kifungu cha 81, kamati inashauri serikali kuangalia uwezekano wa kujenga vituo vipya vya Zimamoto na Uokozi katika sehemu ambazo hazina vituo na vile vile kutoa kipaumbele kwa maeneo ambayo yameanzishwa na yameshapatiwa hati za ujenzi, maeneo hayo ni kama vile eneo la Kijichami Wilaya ya Micheweni Pemba.

Utekelezaji

Kikosi katika mkakati wake wa kusogeza huduma za Zimamoto na Uokozi karibu na wananchi, kikosi kimeweza kupatiwa maeneo ya ujenzi wa vituo vipya ambavyo tumeshapata hatimiliki navyo ni Kijichame, Tunguu na Mchangamle. Kutokana na gharama kubwa za ujenzi wa vituo hivyo, kikosi kinategemea kupatiwa fedha za mradi wa ujenzi wa vituo hivyo katika mwaka wa fedha 2018- 2019.

Kifungu cha 84, kamati inashauri serikali kufanya juhudi za makusudi ya kuwapatia kikosi vifaa vya Zimamoto pamoja na kuongeza ukomo wa bajeti katika kutekeleza majukumu yake. Kutokana na ziara yake ya vituo tofauti. Kamati ilielezwa kuwepo kwa changamoto ya vifaa na hivyo kuwapa wakati mgumu katika utendaji wao.

Utekelezaji

Kwa mwaka wa fedha 2017-2018 kikosi kimeongezwa fedha za matumizi ya kawaida ili kukidhi mahitaji ya upatikanaji wa vifaa, vile vile kikosi kinaendelea kutafuta washirika wa maendeleo ili waweze kutusaidia katika upatikanaji wa vifaa vya Zimamoto na Uokozi vilivyo na upungufu mkubwa katika kikosi chetu. Vifaa ambavyo vimepatikana kwa ufadhili ni mtambo wa kujaza upepo (*BA*) *1, pear 60 ordinary fire suit* (nguo za kawaida za kuzimia moto), viatu pear 70, vitanda 15 na *breathing apparatus 20* vifaa vya kupumulia navyo vimepatikana. Vitu hivi wajumbe wanaweza wakaviona kidogo lakini hivi ni vile vifaa ambavyo pale unapotokea moto vifaa hivi wazima moto wanaingia navyo katika sehemu zile za moto.

Serikali ya Ujerumani na Japan imeendelea kutupatia msaada na mafunzo kwa wafanyakazi wetu.

Kifungu cha 82, kamati inashauri katika kukiboresha Kikosi hiki, ni vyema kupatiwa wataalamu wa fani mbalimbali ikiwemo Wakandarasi, Maafisa Habari na Maafisa TEHAMA. Kikosi kipo tayari kuwaajiri wataalamu wa fani mbalimbali wakati fursa za ajira zitakapotokeze. Hata hivyo, kikosi kinaendelea kuwapatia wapiganaji wake taaluma katika fani za Utibabu 2, Rasilimali watu 1, Sheria 1 na Teknolojia ya Habari 1 ndani na nje ya kikosi.

Suala Nam.89, kamati inashauri Serikali za Mitaa kuwapatia elimu watendaji wake wakiwemo Masheha, Madiwani na wafanyakazi wa kawaida ili kuendana na mabadiliko ya sheria na mazingira. Mkoa kwa kushirikiana na Manispaa zake imewapatia mafunzo Masheha, Madiwani na Wafanyakazi kama ilivyoanishwa katika bajeti.

Kifungu cha 91, kamati inashauri Serikali za Mitaa kusimamia vyema utoaji wa huduma za kijamii na kuhakikisha kila mmoja zimemfikia kwa kiwango chenye ubora.

Utekelezaji

Kufuatia kuanza kutekelezwa kwa Sera ya Ugatuzi wa Madaraka, Serikali za Mitaa zinaendelea kushirikiana na sekta ambazo baadhi ya majukumu yake yamegatuliwa kutekeleza mipango ya kutoa huduma kwa wananchi. Huduma hizo ni pamoja na Kilimo, Afya ya Msingi na Elimu ya Msingi.

Mwisho kifungu cha 62 ambacho kiko kwenye kifungu cha 95, kamati imebaini kuwepo kwa baadhi ya Masheha ambao uwezo wao wa kazi umepungua kutokana na ugonjwa na umri mkubwa. Hivyo, kamati inashauri wizara kufanya mabadiliko ya Masheha ambao uwezo wao wa kazi umepungua kutokana na ugonjwa, umri mkubwa au kukosa uadilifu katika utekelezaji wa majukumu yao.

Utekelezaji

Hivi karibuni, Mikoa yote ya Unguja na Pemba imeshafanya uteuzi wa Masheha wapya kujaza nafasi za Shehia zilizokuwa wazi, kwa sababu Masheha waliokuwepo kufariki, kuwa na umri mkubwa, matatizo ya afya na waliokiuka maadili ya kazi. Aidha, Masheha wapya pia wameteuliwa kujaza nafasi za Shehia mpya zilizoanzishwa.

Hitimisho

Mhe. Mwenyekiti, mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa hoja, ushauri na maoni yametokana na ushirikiano wa hali ya juu wa viongozi na wafanyakazi wote wa ofisi yangu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kukushukuru wewe binafsi na Wajumbe wote wa Baraza lako tukufu kwa mashirikiano mnayotupatia katika ofisi yetu. Namshukuru Mwenyekiti

na Wajumbe wa Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum za SMZ kwa ushauri na maelekezo yanayotusaidia sana katika kufanikisha majukumu yetu.

Mhe. Mwenyekiti, aidha, napenda nitumie fursa hii kuwashukuru viongozi na wafanyakazi wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ pamoja na taasisi zake kwa juhudi zao kubwa wanazochukuwa katika utekelezaji wa majukumu tuliyopewa na taifa.

Mhe. Mwenyekiti, ni imani yangu kwamba, wajumbe wamefuatilia kwa makini maelezo niliyoyatoa ambayo yamefafanua utekelezaji wa hoja mbali mbali na ushauri uliotolewa na kamati.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante hoja imeungwa mkono sasa naomba nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum na yeye kuwasilisha ripoti yake.

Mhe. Machano Othman Said (Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum): Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hotuba ya Kamati ya Katiba, Utawala Bora na Idara Maalum kuhusu utekelezaji wa maagizo ya Kamati katika ripoti ya mwaka wa fedha 2016/2017 kwa Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ.

Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehma Mwenye kurehemu kwa kutujaalia uhai na uzima, ambao umetuwezesha kukutana tena leo katika Baraza hili tukufu kwa kutekeleza majukumu yetu ya msingi kwa nchi yetu kiujumla. Ninamuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu azidi kutubariki neema zake ambazo kwa hakika sote ni wahitaji kwake.

Mhe. Mwenyekiti, napenda pia kukushukuru wewe kwa kuliongoza Baraza hili vizuri namuomba Mwenyezi Mungu akuzidishie hekima, busara katika jukumu letu la kutuongoza ili tuweze kuutekeleza vyema wajibu wetu katika chombo hiki muhimu kwa nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile, shukrani za pekee ziende kwa uongozi mzima wa Wizara ya Nchi OR - Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa ushirikiano wao mkubwa wanaotuonesha katika kufanikisha jukumu zito la utekelezaji wa mipango ya serikali kwa ujumla la kuwapatia huduma bora na salama wananchi wote. Aidha, naomba kuchukua nafasi hii kumpongeza Mkuu mpya wa Wilaya ya Magharibi ‘’A’’ Kapteni Khatib Khamis Mwadini ni matarajio yangu kwamba atafanya kazi kwa weledi na uwaminifu ili kuwaletea maendeleo wananchi wa Wilaya hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuchukua fursa hii kuwashukuru sana Wajumbe wa Kamati yetu ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum kwa namna wanavyonipatia mashirikiano makubwa katika kutekeleza majukumu ya kamati hii, ni dhahiri kwamba ushiriki wao ndio mafanikio ya kamati yetu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba sasa kuwatambua wajumbe wanaounda Kamati hii kama ifuatavyo:-

Mhe. Machano Othman Said	Mwenyekiti
Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis	Makamu Mwenyekiti
Mhe. Nadir Abdul – latif Yussuf	Mjumbe
Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Mjumbe
Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa	Mjumbe
Mhe. Ali Khamis Bakari	Mjumbe
Mhe. Suleiman Makame Ali	Mjumbe
Nd. Ali Alawy Ali	Katibu
Nd. Haji Jecha Salum	Katibu

Mhe. Mwenyekiti, kwa mujibu wa kanuni ya *108(14)* ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi Zanzibar, imetoa fursa ya lazima kwa kila kamati kutayarisha ripoti ya mwaka itakayowasilishwa katika kikao cha mwezi wa Februari cha Baraza la Wawakilishi Zanzibar kila mwaka.

Mhe. Mwenyekiti, aidha, kanuni ya *108(15)* ya Kanuni za Baraza, inaelezea kuwa kabla ya kuwasilishwa Barazani utekelezaji wa maagizo hayo, kamati inatakiwa kukaa na wizara husika kujadili utekelezaji huo.

Mhe. Mwenyekiti, kamati kwa kutumia Kanuni ya 106(3) imepewa jukumu la kufuatilia utekelezaji wa maagizo ya kamati yaliyotolewa katika Ripoti ya Kamati ya mwaka uliotangualia. Ambapo kazi hii ilifanywa vyema kwa kipindi hiki kilichopita na bado kamati inazidi kufuatilia utekelezaji wa maagizo hayo kila inapoona inafaa kufanya.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, jumla ya maoni na ushauri 95 yalitolewa katika idara mbali mbali. Ambapo zaidi ya asilimia 75 ya maagizo hayo yalikuwa katika Mamlaka za Mikoa.

Aidha, kamati imepitia, imejadili na kujiridhisha na utekelezaji wa maagizo hayo kwa kipindi hiki ambacho Maagizo yaliyotolewa yanafanyiwa kazi. Kamati inamuomba Mwenyezi Mungu azidi kuwapa nguvu, imani na busara katika kukamilisha majukumu yanayowakabili. Hata hivyo, baadhi ya maagizo au ushauri kwa wizara hii kamati imekubaliana na wizara kuyaandika upya na kuyaweka kiujumla kwa vile yanajirejea rejea kwa taasisi nyingi za wizara hii.

UTEKELEZAJI WA MAAGIZO

Mhe. Mwenyekiti, kamati imeitaka wizara kufuatilia zaidi utekelezaji wa maagizo kwa kutoa maelekezo yafuatayo:-

(i) Kamati inashauri Ofisi ya Mrajis wa Vizazi na Vifo kutoa elimu kwa wananchi kuhusu umuhimu wa kujisajili katika vyeti vya kuzaliwa, vifo, ndoa na talaka.

Mhe. Mwenyekiti, kamati imeelezwa juu ya jitihada nyingi zinazochukuliwa kwa kutolewa elimu kwa wananchi kupitia vyombo mbali mbali vya habari kwenda kujisajili katika vyeti lakini changamoto kubwa iliyopo ni uhaba wa vitendea kazi kama vile magamba ya vyeti na mabuku ya fomu za B1 katika vituo vya kusajilia vyeti.

Mhe. Mwenyekiti, kamati inazidi kusisitiza juu ya kuchukuliwa hatua za kupatiwa vitendea kazi katika Ofisi za Usajili wa Vizazi na Vifo kwa kupatiwa kwa wakati na hususan katika Wilaya za Unguja na Pemba. Vile vile, Kamati inaishauri Ofisi ya Mrajis wa Vizazi na Vifo kuweka bei elekezi kwa vyeti vya ndoa itakayotumika maeneo yote ya Unguja na Pemba.

(ii) Aidha, kamati inashauri serikali kuharakisha ujenzi wa kituo cha Daladala cha Kijangwani. Vile vile, kamati haijaridhika kuwepo kwa kituo cha Daladala mbele ya ofisi kuu ya CCM Kisiwandui mpaka Tobo la pili Michenzani, hivyo Kamati inashauri kuondolewa kwa kituo hicho.

Mhe. Mwenyekiti, kamati inafuatilia kwa umakini utekelezaji wa ushauri huo na inapongeza juhudi za wizara kwa kushirikiana na uongozi wa Mkoa wa Mjini Magharibi kwa kuendelea kuratibu vyema suala hili la upatikanaji wa sehemu ya maegesho ya kisasa ya magari katika mji wetu wa Zanzibar, ambao ndio kivutio kikubwa cha utalii na chanzo cha uchumi wa nchi yetu.

(iii) Kutokana na athari za matukio ya kesi za udhalilishaji na ubakaji, Kamati inashauri serikali na taasisi zinazohusika kusimamia sheria na kuchukua hatua kali katika kudhibiti tatizo hili, ili iwe funzo kwa watendaji na wahalifu wengine wenye kufanya vitendo kama hivi.

Mhe. Mwenyekiti, kamati yetu imeelezwa kwa kina juu ya juhudi zinazochukuliwa na Serikali dhidi ya kukomesha vitendo vya udhalilishaji ikiwa ni pamoja na kuanzishwa kwa Mpango wa Taifa wa Kumaliza Udhalilishaji wa Wanawake na Watoto 2017-2022. Hivyo, Kamati inapongeza juhudi hizi na inaitaka wizara kusimamia kikamilifu Mpango huu ili kufikia malengo yaliyokusudiwa.

(iv) Vile vile, Kamati inashauri kwa Wakuu wa Mabaraza Pemba kuajiri kwa muda wataalamu kwa mikataba kwa mujibu wa mahitaji yao yalivyo kama wanavyofanya wenzao wa Unguja.

Mhe. Mwenyekiti, katika utekelezaji wa ushauri huu, kamati imeelezwa kuwa ushauri huu unatekelezwa kwa kuwa sheria na taratibu zinaruhusu Mamlaka za Serikali za Mitaa kuajiri wataalamu kwa mikataba.

Mhe. Mwenyekiti, kamati inazidi kusisitiza kuwa katika ukusanyaji wa mapato katika Mabaraza ya Miji na Halmshauri zake kuanzishwe mfumo maalum wa ukusanyaji kodi kwa njia ya kielektroniki ili kuziba mianya ya upotevu wa fedha. Aidha, Kamati imeelezwa kuwa kila Halmashauri imeandaliwa fungu maalum ili kuhakikisha wamemudu kukusanya kodi kitaalamu.

Mhe. Mwenyekiti, kamati inazidi kusisitiza fedha za miradi ya maendeleo na zile za mfuko wa Jimbo zitumike vizuri na kukamilisha malengo yaliyokusudiwa kwa kushirikiana na Halmashauri na Mabaraza ya Miji husika. Vile vile, katika kufanikisha hili ni vyema fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo zilizotolewa kwa Mwakilishi ambaye hakufanya marejesho ya matumizi zisitolewe kwa Mwakilishi ambaye hatofanya marejesho kwa fedha ambazo zilitolewa mwaka uliopita. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kamati inatoa pongezi kwa utekelezaji mzuri wa ushauri uliotolewa kuhusu Askari Jamii wa Mji Mkongwe na kufanyiwa kazi. Kamati imeelezwa kwamba Askari Jamii wa Mji Mkongwe mkataba wao walioingia na Manispaa ya Mjini hautaendelea tena kufikia mwishoni mwa mwezi wa Septemba 2017. Kwa bahati nzuri Mhe. Waziri leo ametuthibitishia kwamba tayari mkataba huo umeshafungwa na sasa hivi serikali inatazama mkataba mwengine.

(v) Kamati inashauri serikali kuandaa Bima ya Afya kwa ajili ya wafanyakazi wote wa Idara Maalum ili kuwajengea mazingira mazuri ya utendaji wao wa kazi. Aidha, kamati inaitaka serikali kuanzisha Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa upande wa Idara Maalum za SMZ kwa kuangalia utaratibu unaotumiwa na vikosi au Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mhe. Mwenyekiti, kamati kupitia wizara hii, imeridhika na maelezo yaliyotolewa ya utekelezaji wa ushauri huo kwa kutambua umuhimu wa Bima ya Afya kwa watumishi wake. Kamati imeelezwa kuwa serikali tayari imeanzisha mchakato wa kuanzisha Bima ya Afya kwa watumishi wote wa umma, wakiwemo Watumishi wa Idara Maalum za SMZ kupitia Wizara ya Afya.

Pia, kamati imeelezwa kuwa wizara kupitia Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa kushirikiana na Idara Maalum ya SMZ imeunda Kamati Maalum ili kufuatilia uwezekano wa kuiunganisha Idara Maalum na *ZSSF*.

Kamati inashauri wizara kuzidi kusimamia maeneo yake ya Kambi zote za Idara Maalum kwa kuyapatia maeneo hayo Hatimiliki kwa kushirikiana na Idara ya Upimaji kwa zile kambi ambazo hazijapatiwa na zimekuwa na migogoro ya hapa na pale pamoja na kuvamiwa na wananchi.

HITIMISHO:

Mhe. Mwenyekiti, kiujumla Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum imeridhika sana na utekelezaji wa maagizo iliyoyatoa katika ripoti iliyopita, lakini bado changamoto kubwa ipo katika makaazi ya askari wetu wa Idara Maalum za SMZ, kwani vituo vingi hali zao haziridhishi. Ni imani ya kamati yetu kuwa kupiktia utekelezaji wa bajeti hii na Ilani bora ya Chama cha Mpinduzi, changamoto hii itapatiwa ufumbuzi kwa muda mfupi ili nao kuweza kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi na kwa ubora zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Mwenyekiti wa Kamati kwa uwasilishaji wako. Waheshimiwa Wajumbe mjadala uko wazi na kwa kuanzia tunaanzia na Mhe. Ali Suleiman Ali.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama hapa kuchangia ripoti hii au taarifa ya utekelezaji ya Wizara ya Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ. Lakini pia nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa kutusomea taarifa hii nzuri na niwapongeze Wajumbe wa Kamati wote kwa kazi nzuri waliyoifanya kutuletea mambo mbali mbali ambayo pana haja ya kwamba paungwe mkono ili twende vizuri katika utekelezaji wa kazi zetu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitazungumza kwa ufupi maeneo fulani hasa nikizingatia kwamba taarifa hizi zote ni nzuri na zina mambo mengi yaliyoguswa. Niende ukurasa wa nne nitazungumzia Mkoa wa Mjini Magharibi.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Mhe. Mkuu wa Mkoa wetu wa Mjini Magharibi kwa kazi nzuri anazozifanya na hasa tukizingatia kwamba kazi zake za kuhakikisha kuwa nchi yetu inakuwa katika salama na amani, lakini pia vizazi vyetu ambavyo tunavitegemea viishi au vikue katika hali ya usalama wa maisha yao ya baadae.

Mhe. Mwenyekiti, Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi kwa asilimia mia moja. Mimi namuunga mkono kwa kazi zake anazozifanya na pana haja wananchi wote wenye imani na nchi yetu na vizazi vyetu vya baadae na wao pia wamuunge mkono kwa asilimia mia moja bila ya matatizo. Lakini pia nimpongeze Rais wetu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kumuona kwamba Mkuu wa Mkoa wetu kwa uteuzi wake hakupoteza dira, lakini nimuombe mtendaji wake mkuu Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa kusimamia vyema yale maagizo yote yanayotolewa na kutekelezwa bila ya kuathiri mambo mengine. Mheshimiwa hayo ndio malengo ya utendaji bora katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, tuna matatizo mengi katika nchi yetu, kuna udhalilishaji wa watoto wetu na udhalilishaji uko kwa watoto na wanawake hata kinababa wakati mwengine. Kwa sababu baba anaweza kuwa na safari zake akakutwa na majanga huko usiku katika kutembea akaambiwa hapa utoe kitu ulichokuwanacho au unapigwa panga, hayo yamejitokeza. Kwa hivyo, Mhe. Mkuu wa Mkoa na watendaji wake Wakuu wa Wilaya zote nawapongeza kwa kazi nzuri wanazozifanya. Lakini pia vyombo vya ulinzi na usalama navipongeza kwa shughuli zao wanazofanya bila ya matatizo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kuna utaratibu Mhe. Mkuu wa Mkoa kauanzisha 'Mimi na Wewe'. Maana yake mimi na wewe tukiungana kwa nia njema kufanya maendeleo tutafanya, ya kuondoa maovu tutaondoa, ya kuhakikisha hili lisifanyike halitofanyika. Nampongeza kwa hilo nimeona mifano yake mingi, lakini katika Jimbo la Pangawe, Kijitoupele Skuli Mheshimiwa alishajihisha wananchi. Katika historia nakumbuka mimi wakati huo mdogo Mzee Karume Maisara kule alisema neno moja kubwa sana, alikaa katika uwanja wa Maisara akawa anahutubia akasema: "nataka barabara hii ya Maisara itoke hapa mpaka hospitali watu wang'oe mivinje na mambo mengine ili barabara iwe nzuri".

Zamani tuliambiwa wafungwa au wanafunzi ndio waliokuwa wanalazimishwa kufanya hivyo wakati wa ukoloni, lakini watu kwa ridhaa yao walifanya na barabara nyingi zikapatikana na mambo mengineyo kwa kujitolea. Kwa hivyo, hili la mimi na wewe na mimi ninalichukulia kigezo katika jimbo langu la Kijitoupele, wananchi wangu nitawaelekeza huko kwa mambo mema yanayofaa kama haya. Hongera sana Mhe. Mkuu wa Mkoa na Wakuu wa Wilaya zetu zote katika Mkoa wetu.

Mhe. Mwenyekiti, jengine nitalolichangia katika ukurasa wa 13 mpaka sasa hivi tuseme tu kwamba kuna Manispaa zetu mbili 'A' na 'B '. Manispaa zetu hizi ni mpya nimuombe sana Mhe Waziri mara nyingi nikisimama huwa nasema haya, Manispaa zinataka msaada, zinataa kila kitu ili zifanye kazi kwa ufanisi. Kwa bahati mbaya Manispaa zetu hizi zimekuja katika wakati mgumu hawana nyezo za kufanyia kazi, ingawa kamati imetoa maelekezo yake hapa kwamba kuna mambo yaunganishwe ili faida ipatikane. Kwa mfano, kuna maelezo yalielezwa hapa Mheshimiwa naomba ninukuu kwa ruhusa yako.

Kifungu cha 28 cha kamati kinasema:

"Kamati inashauri kuimarishwa kwa vitendea kazi ili kujenga mazingira bora ya kazi pamoja na kuongeza ufanisi na ubora wa kiutendaji kupitia Mabaraza ya Manispaa".

Mhe. Mwenyekiti, hili ni suala kubwa na suala ambalo lina maudhi sasa hivi, katika maeneo yetu majaa yamekithiri na uzalishaji wa taka mkubwa uko katika Magharibi 'A' na' B'. Niiombe wizara iwafikirie Mayaribi 'A' na 'B' Manispaa zetu ule msaada wanaopata wenzetu mjini basi angalau na wao wawajaalie kama ni ndugu zao. Kwa sababu walikuwa wa eneo moja lakini mabadiliko tu yaliyotokea hawana njia nayo.

Bahati nzuri kuna fedha nyingi wanapata Manispaa ya Mjini zinatoka katika mgongo wa Manispaa "B'. Kwa mfano, Soko la Mwanakwerekwe na Soko la Mboga Mboga Kwa Mchina. Mheshimiwa hii ardhi yote ni mali ya Wilaya ya Magharibi 'B', lakini bahati mbaya kinachozalishwa pale kinakwenda mjini. Nimuombe sana Mhe. Waziri najua kuna taratibu za kisheria lakini wakae wawafikirie wenzao hawa ndio nikaja pale katika huduma za vitendea kazi, basi wanapopata zile fedha watenge fungu maalum la kuwapa wenye ardhi. Kwa sababu hili linawaletea mashaka na manung'uniko na bahati nzuri sisi ndio wa kulisemea tatizo lao hilo ili kuhakikisha kwamba mapato yanapatikana na mambo mengine kwa jumla.

Mhe. Mwenyekiti, niipongeze wizara kwa jumla kwa kazi nzuri wanazofanya Wakuu wa Mikoa wote, Wakuu wa Wilaya zote, Manispaa zetu na Halmashauri mbali mbali kwa kuhakikisha kwamba, umefika wakati sasa hivi wa kujitahidi kupata fedha kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli zao. Lakini pia, Mhe. Mwenyekiti nimpongeze Mhe. Waziri kupiti Serikali yetu kuu kwamba vikosi vyetu vimeangaliwa vizuri safari hii, na vikosi vinahitaji nyenzo kwa asilimia nzuri wamebahatika wamepata kwa hivyo ningechukua ushauri wa Kamati na wizara imejibu iko vizuri katika utekelezaji wake naipongeza. Askari yeyote sawa sawa na mtoto mdogo Mheshimiwa, maana mtoto mdogo

ukimwambia nakuja hapa nakuletea mpira wa kucheza kama hukumpa atalalamika, sasa na askari kwa kuwa na mimi natoka katika nyanja hizo, askari atabakia katika hali ya utoto mpaka atastaafu. Pakitokea pamegawiwa mche wa sabuni mara nyingi hutaka kutoa mfano huo, mmoja kapata mwengine hakupata itakuwa masikitiko, lakini kwa mwelekeo wa sasa hivi vikosi vyetu naamini viko katika mwelekeo mzuri vinalingana kutokana na shughuli zao za kila siku.

Mhe.Mwenyekiti, ombi langu kwa Mhe. Waziri tuwawezeshe uwezo wa makazi yao, makazi yawe mazuri, wapate vitendea kazi vya michezo, waweze kuhisi kwamba niko lakini nafanya kazi zangu baada ya mapumziko. Kwa sababu askari hutaka baada ya mapumziko afanye michezo yake ya kujenga siha.

Mhe. Mwenyekiti, suala kubwa jengine ambalo nitalizungumza hapa kuna wito ulitolewa hapa kamati ilishauri. Magharibi 'A' waliambiwa kwamba kuna matatizo ya udhalilishaji wa watoto wetu na kuna watoto wengine wenye mahitaji maalum walemavu, watoto hawa wanataka kutunzwa na kusaidiwa. Kwa hivyo, niipongeze kamati baada ya kuona hilo kwamba masheha wa sehemu zile waliitwa na wamewekwa pamoja kuhakikisha kwamba wanawalilia sana watoto wetu yatima na walemavu na watoto wanaoishi katika mazingira magumu.

Wito wangu namuomba sana Mhe. Waziri kwa kuwa Magharibi 'A' wamefanya hivyo vizuri na mtu akifanya vizuri msifu na wewe litafutie njia lipate tija kwa wale wengine, ningeomba na Wilaya yetu ya Magharibi 'B' masheha wote waitwe. Katika jimbo langu la Kijitoupele nalilia mama yangu maana yake, wananchi wangu wengi walemavu, watoto walemavu wamo wengi, mayatima wengi na wanaoishi katika mazingira magumu wengi sana. Kwa hivyo, kama wataorodheshwa katika orodha hizi mimi nitashukuru sana. Namuomba Mhe. Waziri kwa kuwa hili lililoelekezwa Magharibi 'A' nalo zuri nawapongeza na mimi nitaiomba wizara kupitia masheha wetu kwa nafasi za Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya wapatiwe fursa masheha wa Wilaya ya Magharibi 'B' na wao waelekezwe ili kuwanusuru watoto wetu ambao ni walemavu na wengine hata skuli hawaendi.

La mwisho Mheshimiwa. Mhe. Waziri katika taarifa hizi zote zilizotokea humu mimi napenda kutoa taarifa ifuatayo. Pamoja na kumsifu Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi tunaomba na Wakuu wengine wa Mikoa wote, juhudi zao tunazithamini lakini suala la udhalilishaji na ubaradhuli ambalo limezagaa katika nchi yetu sasa hivi hivi vita vinavyopiganwa ni vita vikubwa tumsaidia na tuwasaidie wote viongozi wetu tushirikiane ili kulikomesha katika nchi yetu. Ni jambo la aibu Mheshimiwa leo unasikia kuna *birthday* ya mabaradhuli, leo kuna *birthday* ya mashoga. Mheshimiwa hili niache niseme ni hatari katika nchi yetu na aibu. Kwa hivyo, niombe sana Mheshimiwa tuwaunge mkono Wakuu wa Mikoa na vyombo vya usalama vifanye kazi ili kuvikomesha katika nchi yetu visitokee.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo kwa heshima kabisa naiunga mkono taarifa hii ya Wizara ya Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa asilimia mia moja ahsante.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: *Bismillahi Rahmani Rahiim.* Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya ghafla ghafla maana naona sijatajwa. Mimi nitaomba kuchangia taarifa hii ya Wizara ya Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ nikiwa ni mjumbe wa kamati mambo machache na mengine vile vile nitaomba nije nijibiwe japokuwa mjumbe wa kamati.

Mhe. Mwenyekiti, jambo la mwanzo nitaomba kutoa pongezi za dhati kabisa kwa wizara hasa kwa wale wanaofanya kazi vizuri kama Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya wa Unguja na Pemba. Nazungumza hivi kwa sababu tumeshuhudia wanafanya kazi nzuri naamini mambo haya baraka zao zinapita nguvu zao wanapata zaidi kupitia kwa waziri wao na waziri pia namuamini kwa kasi yake anayokwenda nayo na maamuzi yake anavyojiamini katika baadhi ya mambo ya kazi zake.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitatoa mfano, Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi na Wakuu wa Wilaya wote na wengine halikadhalika wanafanya kazi za ziada.

Ningeomba sana mimi mtu anapofanya vizuri nitamwambia kila siku na atakapokuja kuharibu nitakuja kuzungumza vile vile. Lakini Mkuu wa Mkoa wa Mjini na ma- *DC* wake wote pamoja na baadhi ya Mikoa mingine wanafanyakazi za ziada nguvu kubwa na hasa kwenye kukomesha masuala ya madawa ya kulevya, masuala ya mashoga ambayo wameanza kukamata.

Vile vile nampongeza sana Kamanda wa mjini Magharibi kuanza kushughulikia kikamilifu kushirikiana na Mkoa kukamata mashoga wote na ikiwezekana nilizungumza jana wawanyoge hata bila ya sheria ya kupita kama inawezekana wawamalize.

Mhe. Mwenyekiti, tumeona hivi kwamba nashauri Wakuu wa Mikoa wengine waweze na wao kufuata baadhi ya vitu, naamini kila mmoja ana majukumu yake kwa mujibu wa mkoa wake. Lakini kuna vitu kama hivi vya madawa ya kulevya, masuala ya unyanyasa, masuala ya uzalilishaji, masuala haya ya mashoga wanafanya mapati, kuna mashoga hapa Unguja wameshafanya harusi, kuna mashoga wanafanya sherehe za *birthday* na nyumba zao zinajulikana hasa mjini. Mimi ningeomba hata kwenye baadhi misafara kwenda kuvamia mashoga Mkuu wa Mkoa na mimi anialike nihudhurie. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, nazungumza haya kwa sababu mambo yameshakuwa *too march* kwetu ni nchi ndogo lakini tuna sifa mbaya sana diniani kwamba Unguja leo tumekuwa wadhalilishaji wengi, tumekuwa na madawa ya kulevya ndio njia watu wanaharibika, mashoga imekuwa kila kitu *live* sasa hivi wanataka kudai haki. Sasa haki hiyo wataenda kuidai kwenye kaburi haitokuja kudaiwa hapa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitazungumza vile vile kwa *DC* na Mkuu wa Mkoa Kusini Unguja pamoja na Kaskazini Unguja na Pemba. Wanafanyakazi nzuri wako katika mazingira magumu lakini wanajitahidi kupitia wizara husika Waziri wao na Naibu waziri. Kusema la ukweli Kusini kuna matatizo makubwa na hili nampa taarifa Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira. Kuna baadhi ya viongozi Waheshimiwa kazi yao kutapeli wananchi hasa kwenye masuala ya ardhi na mfano mdogo tu tunautoa

Mbunge wa Jimbo la Makunduchi anasifika kwa kutapeli wananchi wa Makundichi kwenye ardhi zao.

Nampongeza sana Mheshimiwa *DC* pamoja na Mkuu wa Mkoa kuweza kutaifisha hivi karibuni viwanja kwa mujibu.....

Mhe. Mwenyekiti: Mhehimiwa Mjumbe nenda kwenye hoja iliyoko mbele yetu usitoke nje ya mada.

Mhe. Nadir Abduk-latif Yuusf Al-Wardy: Mhe. Mwenyekiti, nafikiri ninalolizunguza nimetaja *DC* na hapa kwenye Tawala za Mikoa *DC* anahusika.

Mhe. Mwenyekiti: Nenda kwenye hoja iliyoko mbele yetu ya Mhe. Waziri.

Mhe. Nadir Abduk-latif Yuusf Al-Wardy: Ahsante sana. Mhe. Mwenyekiti, nampongeza tena Mheshimiwa *DC* kwa juhudi zake anazozichukuwa Kusini na Mkuu wa Mkoa wake za kuweza kukamilisha mambo haya na kuweza kudhibiti watu wa aina hii kwa sababu wao wanachotakiwa ni kusimamia Wilaya na Mkoa mambo yote yanayofanyika kumefanyika uhalifu na vile vile niwapongeze kwenye masuala yao yote masuala ya Madawa ya Kulevya wanaovamia na mengine.

Mhe. Mwenyekiti, nitaenda kwenye suala jengine ambalo niliwahi kulizungumza kwenye kamati. Mimi nilidai niletewe vithibitisho vya gari mbili aina ya *fire* zilizonunuliwa na Tawala za Mikao. Lakini hadi hivi leo hazikuletwa vithibitisho katika kamati yetu, mimi ni mjumbe wa kamati yaliletwa majibu matupu kwa njia ya mdomo. Naomba sana niletewe vielelezo ili nijihakikishie nivifanyie utafiti niliridhike navyo kuliko kuletewa majibu kwa maneno. Naomba sana tuje tuletewe vielelezo.

Vile vile Mhe. Mwenyekiti, mimi nitazungumzia miradi ya *parking*. Kusema la ukweli Unguja *parking* ya rahisi shilingi 1000 sasa hivi mjini. Lakini tuangalie tunaowaendesha Unguja au wananchi wetu asilimia 90 ni masikini. Leo tunalipisha mfanyabiashara au mtu yoyote mwenye gari shilingi 1000 baada ya masaa mawili akalipe kwengine alipe 1000 kwa siku mtu atatumia zaidi ya elfu 7000 wakati mshahara wenyewe ukimfanyia hesabu kwa siku sasa hivi umepandishwa na Mhe. Rais shilingi laki tatu ukifanya shilingi elfu saba saba mara thalathini unaweza ukaja kupata lakini mbili na sabini hizo, lakini mbili na sabini mtu analipa kwenye *parking*.

Tunaomba sana wizara ikatafakari kwamba watu wanaowaendesha nchi hii ni masikini ni wanyonge kulipa shilingi 1000 moja kwa muda wa saa moja au masaa mawili ni fedha nyingi sana kwa mujibu wa nchi na hali ya uchumi ilivyo na hali ya watu ilivyo ya maisha yao na hali ya watu ilivyo ya maisha yao na mshahara uliokuwepo. Na tukiendelea hivi Mhe. Rais hata akijitahidi vipi kuongeza mishahara katika nchi hii na sisi ikawa kila mwaka tukawa tunafikiria kuongeza kodi, kufikiria kuongeza vitega uchumi kuingiza mapato serikalini tutafelisha mwenendo mzima na tutamfelisha Mhe. Rais malengo yake ya kufaidisha nchi na kuwaidisha wananchi kwa ujumla. Kila siku kila mwaka serikali, wizara, taasisi zinafikiria kupandisha kodi tu hazifikirii kutafuta mbinu nyengine labda za kibiashara kushusha kutizama hali za wananchi.

Ningeomba sana wizara husika masuala haya yote wafikirie Mhe. Waziri na kuamini na wewe una watu wanyonge una watu wavuvi kama mimi, una watu wanyonge wa kulima, uweze kuwafikiria kwenye masuala kama haya.

Lakini vile vile Mhe. Mwenyekiti, unajua mimi ni Mjumbe wa kamati na hii kamati inakuwa inanifunga wakati mwengine. Sasa mimi nimpongeze tu Mhe. Waziri kwa sababu kila wakati unatakiwa mtu umpe sifa yake, kusema la ukweli mtu haki yake uumpe Mhe. Waziri, Naibu Waziri anafanyakazi vizuri tunaona jitihada zake na naamini anafanyakazi kwa uzalendo na anajiamini kwenye kazi zake. Lakini kama tunavyojua hakuna binaadamu aliekamilika iko siku mimi nitatamgeukia iko siku nitamsifu. Kikao cha leo mimi namsifu kwa sababu anafanyakazi vizuri lakini siku nyengine mkija kuona nimekuja kumsema simuonei ndio kazi zetu zilivyo.

Mhe. Mwenyekiti, nitamalizia kwa kusema kwamba wizara hii ni muhimu kama tulivyoeleza Wakuu wa Mikoa tuwape *support* hasa wanapokata kudhibiti masuala fulani fulani haya ya mienendo tunayoenda nayo na nawaomba wazidi kuendelea kwa kasi kudhibiti masuala ya kulevya kwa sababu ndio yalioshamiri hapa sasa hivi Unguja, masuala haya ya udhalilishaji Mkoa wa Kaskazini Unguja unaongoza kwa Unguja nzima watoto kubakwa na kulawitiwa. Tungeomba sana wafanye jitihda za kutosha ili waweze kukamilisha masuala haya na kuyaondosha kabisa na wale mashoga tusiwasahau mimi hawa ndio nina hamu nao kwa sababu wanaume wazima wanakuja kuwa mashoga haielekei kabisa katika kidunia. Hata Mhe. John Pombe Magufuli kasema hata mbuzi hana akili hiyo. Kusema la ukweli wana-*support* yeye Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wana-*support* Rais wa Zanzibar halipendi na sisi tunalipinga kwa nguvu zote na tunaomba sana Wawakilishi sote masuala haya tuyakemee ili yaweze kupotea rai wetu wananchi wetu tupate heshima kwa mujibu wa tulivyotoka Unguja na historia yetu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi leo sitaki kuchangia sana nai- *support* ripoti hii asilimia mia moja mimi ni Mjumbe wa Kamati nashukuru sana.(*Makofi*)

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi nianze kwanza kwa kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kutoa mchango wangu.

Lakini pia nichukuwe nafasi hii kumshukuru Mhe. Waziri kwa hotuba nzuri aliyoisoma juu ya ripoti yake na maagizo pamoja na kuwapongeza Wajumbe wote wa kamati hii pamoja na Mwenyekiti wao wakiongozwa na Mhe. Machano Othman Said kwa hotuba nzuri aliyoisoma.

Lakini pia niwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Tunguu nikiwa msemaji wao hapa na niahidi nitaendelea kuwa msemaji wao na nitajitahidi ili niweze kuleta utetezi mzuri na kuishauri serikali.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza ripoti ni nzuri maagizo ni mengi na Mhe. Waziri kwa kweli kwa muda mchache huu kwa jinsi ambavyo umeweza kuyazungumza na utekelezaji wake sina budi nikupongeze sana pamoja na kamati kwa nguvu zote.

Moja ningependa nipate ufafanuzi nafikiria kwenye ripoti hazijaja uzuri wanapozungumza suala la kwenye vizazi na vifo, waligusia usajili utakuwa kwa ki-*electronic* ningependa nifahamu zaidi kwamba huu *electronic* wanakusudiwa ni kwa kutumia mkonga au wanatakuwa wanatumia *system* ndani ya *computer* ambayo itaweza kuweka kumbukumbu vizuri kwa siku za mbele.

Lakini pia katika masuala ya ndoa nataka nizungumze masuala ya ndoa ambazo zinafanyika kwa raia watu ni wageni wanakuja Zanzibar kuja kufunga ndoa zao. Mhe. Mwenyekiti, suala la *wedding tourism* ni jambo kubwa sana na duniani kwingi sasa hivi watu wamekuwa wanasafiri ili kuja kufunga ndoa zao kwa ajili hasa ya maeneo yenye vivutio kama visiwa vyenye mandhari nzuri kwa ajili ya utalii na mapumziko.
Ukiangalia kwa Zanzibar sasa tumekuwa tunaongoza kwa upande wa Jamhuri ya Tanzania watu wengi kuja hapa. Sasa ni vizuri tukaanza kuweka takwimu zetu kujua watu ambao wanafunga ndoa Mkoa wa Kaskazini ni kiasi gani wanalipa Mkoa wa Kusini wanakwenda katika maeneo ya Paje, Michamvi na maeneo mengine na kwa upande wa Kaskazini kutoka Nungwi, Kendwa, Pwani Mchangani, Kiwengwa na hao wengi wanahitaji kupata hati. Sasa ni vizuri tukawa na takwim zetu tunazitambua ili kuhakikisha kwamba tunajuwa ni pato gani ambalo linapatikana na hasa hawa raia ambao wanakuja kufunga ndoa zao Zanzibar ili tuweze kujua katika suala hili na utalii wetu tunakwendaje.

Lakini nataka niulize suala la mji wetu hasa katika Mkowa wa Mjini Magharibi na mimi pia nichukuwe nafasi hii kumpongeza Mkuu wa Mkoa pamoja na Baraza la Mji kwa kazi nzuri wanayoifanya kuhakikisha ufasi na mambo mengine yanakuwa.

Lakini pia Mhe. Mwenyekiti, mimshauri Mhe. Waziri pamoja na kamati waweze kujipanga mkakati maalum hasa kupunguza mchanga na vumbi katika maeneo ya barabara ya Darajani, Michenzani pamoja na Rahaleo na barabara ya kwenda Airport na siku hizi zipo gari zimepatikana ambazo zinapita nyakati za usiku zinakuwa zina mafagio zinachukuwa mchanga wote na lile vumbi kuweza kuondoa na gari hizi sio kama ni ghali.

Mimi ningeomba sana Mhe. Waziri kwa kupitia Baraza lake la Mji na Mkuu wa Mkoa ambaye anajipanga kuwa mbunifu kuhakikisha kwamba usafi wetu unaimarika basi wapange mkakati katika nyakati za usiku kuangalia uwezekano wa kupata hizi gari ili kulinda usafi wetu.

Lakini pia nashauri kwenye masuala ya *parking* kufanyiwe mkakati bora wa kisasa ikiwa kama wanazungumza kama kubinafsisha na serikali kupokea kodi yake au mapato kwa kuingia mkataba lakini pia kutumia mashine za kisasa ili mashine hizi ziweze kwenda na mpango mzima wa miji ambayo inayostahiki kuwa na sifa kama hizi na sisi kama mji wetu sasa hivi wa Zanzibar kadiri tunavyokwenda magari yanaongezeka. Kwa hiyo, wanaweza kuangalia kujenga sasa maghorofa ya kuweza kuweka magari kwa ajili ya watu ku-*park* magari yao na kwa bei nafuu ambayo mwananchi anaweza kulipia.

Mhe. Mwenyekiti, sisi katika ripoti ya Mhe. Waziri aliposoma pamoja na Mhe. Mwenyekiti wa kamati husika waliongelea mambo mengi sana. Lakini moja ambalo

nataka niligusie ni suala la utalii. Lakini nataka ninukuu kifungu cha katiba yetu sura ya tano ukisoma kifungu namba 63 inasema kwamba:-

"Kutakuwa na Baraza la kutunga sheria ambalo litajulikana kama Baraza la Wawakilishi lililokuwa na sehemu mbili Rais wa Zanzibar kwa upande mmoja na Wawakilishi kwa upande wa pili".

Niseme kwamba sisi sote tunaongozwa na Katiba hii yetu ya Zanzibar mwaka 1984 kwa kazi zote ambazo sisi tunatakiwa tuzifanye katika kushauri serikali. Sehemu nyengine ni hotuba ya Rais ambayo aliisoma hapa tarehe 5 April 2016 wakati wa uzinduzi Baraza la tisa.

Mhe. Mwenyekiti, ukienda kwenye ukurasa wa 25 anazungumzia suala la utalii na malengo kwenye ukurasa wa 25, 26 ni kwamba tuna malengo ya kuongeza watalii kutoka laki moja elfu thalathini na mbili mwaka 2010 hadi kufikia laki tatu mwaka 2014 hizi ni takwimu za nyuma. Lakini tuna mpango wa kuongeza watalii zaidi kwa mujibu wa ilani kufika laki tano endapo tutafikia 2020.

Mhe. Mwenyekiti, kitabu chengine ambacho kinaniongoza mimi ni Ilani ya Chama cha Mapinduzi juu ya uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015 na imetolewa hii na Halmashauri kuu ya Chama cha Mapinduzi. Ukienda katika ukurasa wa 142 kutoka 41 inasema kuendeleza kuhamasisha sekta binafsi kuanzisha miradi ya ujenzi ya hoteli za kitalii hususan hoteli za daraja la kwanza na kuongeza idadi ya watalii kufikia laki tatu elfu kumi 2014 lakini laki tano kuelekea 2020.

Mhe. Mwenyekiti, nimeona katika moja ya changamoto ambazo zimejitokeza katika Mkoa wa Kaskazini walizungumza suala la Tamasha la *Full Moon* ambalo linafanyika *Kendwa Rocks*. Mhe. Mwenyekiti, pahala penye wengi inawezekana ikawa pana mapungufu lakini mimi niseme tu kwamba mimi nalitambua hili tamasha tangu mwaka 1996 mmiliki wa hili tamasha ni Mzanzibari ni mwana CCM safi ni mbunifu na ukienda katika ukweli tamasha la *Full Moon* litambulikana duniani katika matasha 7 bora dunaini. La saba liko Zadar Croatia, la sita ni Montanita Equador, la tano ni Magnatic Island Australia na nne ni *Zanzibar Tanzania Kendwa Beach*, la tatu ni Doha India Anduna beach, la pili ni Ibitha Spain la kwanza ni Confan chang Thailand inaitwa *bahari hard bin beach*.

Kwa hiyo, mimi nimuombe tu Mhe. Waziri ni mtu mwenye busara hodari na kwa kweli yeye anaunga juhudi za serikali na hasa katika suala la utalii na kuimairisha uchumi wetu. Aangalie uwezekano wapi ambapo panahisi patawezekana kuboresha mimi naamini leo alinijibu suala zuri sana juu ya soko langu la Kaebona Mhe. Haji Omar Kheir ni mzoefu juhudi za Wazanzibari ambao wamekuwa mstari wa mbele katika kuimarisha uchumi wa Zanzibar ajaribu kuangalia pamoja na Mkuu wa Mkoa ambaye anakaimu hivi sasa wa mjini na endapo atakaporudi Mkoa wa Kaskazini Unguja washirikiane kwa pamoja ili kuhamasisha vile vivutio vyote ambavyo ni vya utalii vinaendana uzuri na sisi haturudi nyuma kama Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tunashauri na pale ambapo pana kasoro mimi naamini mmiliki wa hii hoteli ya *Kendwa Rocks* ni mtu ambaye ni mwana CCM

mpenda maendeleo anawafanyakazi zaidi ya 200 mlipaji kodi mzuri na amewegwa juhudi za serikali za utalii kwa wote.

Kwa hiyo, Mhe. Waziri mimi ninachokuomba hili suala limalizike yaani twende nalo na tuweze sasa kuweka mkomo na kuhakikisha kwamba wale Wazanzibari wote wanafanyakazi nzuri tutakuwa tuko nao pamoja na mimi katika hilo nitakuwa nalo na wewe nikiwa mdau ambao naipenda sekta ya utalii ikiwa ni mnyororo wa kujenga uchumi wetu wa Zanzibar.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, nataka niongee pia nikuombe Mhe. Waziri wale wawekezaji ambao waliokuwa wa mwanzo katika eneo la Kendwa wana tatizo la ile barabara ambayo inataka kujumuika katika barabara kuu kuelekea ndani. Kwa hiyo, nimuombe Mhe. Waziri pia na kamati husika katika ripoti yao itakayokuja katika mwaka ujao au mwisho wa mwaka waangalie uwezekano katika hoteli ambazo ziko Kilindi, Amani ya Kendwa, *Kendwa Rocks, Sun Seat* Bangaloo pamoja na barabara ambayo inatoka upande wa *White sand* kuimarisha ile barabara ili na wao wapate unafuu ili tuweze kuhakikisha kwamba miundo mbinu ya Mkoa wa Kaskazini inazidi kuimarika.

Mimi Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka 2005/2010 nilikuwa ni Mwenyekiti wa Jumuiya ya Uwekezaji sekta ya Utalii Zanzibar na katika moja ambalo niliacha zawadi katika Mkao wa Kaskazini ni kituo cha Polisi cha Nungwi ambacho nilishirikiana pamoja na wadau wengi wakaniunga mkono hasa wale ambao walikuwa Wazanzibari pamoja na kampuni ya *RENCO* ambayo ni wamiliki wa Hoteli ya Alagema.

Kwa hiyo, mimi nihakikishe kwamba ushirikishaji wa wawekezaji wote katika Mkoa wa Kaskazini ni muhimu katika kuleta ulinzi na kulinda amani yetu na katika kuhakikisha kwamba ule msemo ambao tunausimamia kwa wote tunakwenda sambamba na wananchi vijijini vyetu wana CCM pamoja na wale wote wapenda maendeleo.

Lakini niseme kuwa unajua Mhe. Mwenyekiti, mwanga wa jua unachukuwa dakika 8 mpaka sekunde 11 kufika katika dunia yetu. Ukiangalia kwamba kuna wengi wanasema kwamba dunia ilikuwa ni *flat* si duara. Kwa hiyo, kule tuna sayari zetu tunaziweka pembeni ya dunia tuna *Mercury, Venus, Earth,* tuna *Mars, Jupiter , Saturns* pamoja na *Uranus* .

Kwa hiyo, ukiangalia jua, jua ni nyota lakini wengi wanafikiria ni jua peke yake lakini jua ni nyota. Lakini katika nyota ambayo ipo karibu na macho ya binaadamu na kama nilivyosema mwanga wa jua unachukuwa dakika 8 na sekunde 11. Kwa hiyo, jua ndio rais wetu tegemeo letu ambaye ndie Mhe. Dokt Ali Mohd Shein Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na sisi sote tunalizunguka hili jua.

Kwa hiyo, kwenye suala la uchumi sisi tutakwenda kwa mujibu wa Rais wetu ndoto yake anayoitaka kuhakikisha kwamba Zanzibar tunafika pahala ambapo panapostahiki. Kwa hiyo, Wakuu wa Mikoa niwaombe Wakuu wa Wilaya wote na viongozi wa Halmashauri wahakikishe wanasoma ilani ya Chama cha Mapinduzi, wanasoma hotuba zote za Mhe. Rais na kuzifahamu hasa katika suala la uchumi. Watambuwe pia katika suala la Mkuza maeneo yaliyotajwa kwenye utalii, biashara na huduma katika suala zima la MKUZA.

Mhe. Mwenyekiti, lakini niseme pia Mhe. Waziri katika hoja ya kuendeleza katika wilaya zetu, Wilaya ya Kati nilikuomba juu ya barabara hizi za Tunguu Mji mpya na Jumbi Mji mpya ambapo viongozi wengi sasa wameanza kuhamia. Naamini kwamba Mkuu wetu wa Mkoa wa Mjini Magharibi pia na yeye ni mtu ambaye anaishi kule na viongozi wengi wapiganaji wetu. Sasa tujitahidi sana katika kuhakikisha kwamba zile barabara zetu za ndani tunaziimarisha pamoja na lile lengo la Tunguu Mji mpya na Jumbi Mji mpya tunaweza kuyaweka sambamba pamoja na dira ya maendeleo ya nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo nimuombe Mhe. Waziri mwenye dhamana kwamba nitaleta maombi yangu rasmi kwa niaba ya jimbo langu anisaidie kupata nguzo za taa ambazo hazitumiki nyengine ziko *Victoria Garden*, ambapo nataka nitumie njia ya ubunifu kutafuta kuboresha taa za Mkoa yetu, pamoja na wilaya na Jimbo langu la Tunguu, ili kuunga mkono juhudi za serikali katika kuhakikisha kwamba wananchi wanapata maendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo na kwa kuzingatia muda, nichukuwe muda huu kukushukuru sana. Mimi naunga mkono hotuba yote ya Mhe. Waziri kwa asilimia mia juu ya mia. Namuomba na yeye pia kwa mawazo yangu yale yote niliyoyazungumza ayabebe na ayafanyie kazi, na Mwenyezi Mungu atakuwa nyuma yake pamoja na sisi Wajumbe wa Baraza wote. Baada ya hapo nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na Wajumbe wa Baraza hili la Wawakilishi kwa kunisikiliza. Naunga mkono hoja ahsanteni sana.

Mhe. Abdalla Ali Kombo: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako kwanza napenda kumpongeza sana mzee wa *speed*, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, kwa kazi zake nzuri.

Mhe. Mwenyekiti, nawaomba na ndugu zangu za Tumbatu msimuache mwana huyu mbebeni mpaka aseme basi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, lakini pia nampongeza Naibu Waziri na maofisa wake wote walioandika hotuba hii. Mji sasa umekuwa mji, ukija ng'ambo kwetu Magogoni, Magomeni sasa hivi shwari kila mtu unamuona na kila mtu anamuona mwenzake, kwa hivyo hakuna haja ya kupapasa tena.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitaanza kuchangia kwenye *ZSSF*. Mhe. Mwenyekiti, suala limekuwa kubwa sana sasa hivi hasa kwa vijana wetu wa vikosi au Idara Malum. Sasa imeandikwa kwenye ripoti, lakini ningemuomba Mhe. Waziri akija tupate ufafanuzi zaidi. Imeandikwa kwamba tunashughulikia, lakini kushughulikia labda mpaka lini, na nani atashughulikia. Kwa sababu kuna neno kwenye ripoti limeandikwa, kuna kamati ya Idara ya SMZ inatafuta uwezekano. Kwa hivyo, hapa kuna hatari kwamba kama uwezekano haupo hii kazi itaachwa. Kwa hivyo, naomba tujitahidi hawa vijana wetu tutizame hatima yao, kama sisi humu ndani.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ni kwamba na yeye mwenyewe aliniahidi kwamba atafanya *follow-up* nani amehusika, bado mji wetu heshima ya ujenzi haipo au nidhamu ya ujenzi

haipo, hasa pembezoni mwa barabara. Tunazungumzia ajali za hawa, sijui niwaite vipi, lakini hawa waendesha vespa wanaitwa sijui T nini, hivyo hivyo. Kwa hivyo, utakuta mita 1.5 au mita haizidi 2.5 mtu anajenga nyumba, haikuwepo zamani ndio inajengwa sasa hivi. Kwa kweli nidhamu inakuwa haipo na nina wasi wasi mtu huyu au mfanyabiashara huyu akianza biashara basi Manispaa inachukua kodi. Sasa hapa ni kwamba tunahalalisha ubovu ama uoza.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri yeye mwenyewe ni shahidi, mimi nakaa Mwanakwerekwe ni Mwakilishi wa Jimbo la Mwanakwerekwe kuna njia ya kwenda amani, sasa hivi biashara imeanza na nina uhakika aidha Manispaa ya Mji ama Manispaa A itakuwa inachukua pesa. Lakini tufahamu tu kwamba tumehalalisha kitu ambacho sicho. Ajali ikitokea tumo, maafa yakitokea sio waziri Mohammed Aboud tu mimi namuita nambari 6 huyo tayari kafika. Lakini ni kwamba chini ya nyumba hii kuna bomba kuu la maji, maeneo haya ndio maeneo yale ambayo maji yanapita yanakwenda Sebleni. Sasa sijui kama wizara yako ama ya ujenzi watu wa *master plan* hao, lakini hiyo ni hatari na Mwanakwerekwe ndio ile ile ndugu zangu masika ikija Rais yuko mbele, Mhe. Mohamed Aboud anafanya *rack*, hii ni hatari. Nadhani tusiwaonee tabu kumwambia mtu hiki kitu hakiwezekani, vyenginevyo inakuwa ni aibu kwetu na inakuwa aibu kwa nchi.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, ambalo ni la kuudhi na ambalo linaondosha haiba ya mji. Siku hizi ukipita mabarabarani pembeni mule kuna zile *used*, aliyeweka baskeli, mafriza, magari ya ajabu ajabu. Sasa hili nawaomba Wakuu wa Manispaa zote, jambo hili linatia aibu. Saa nyengine tujiheshimu na umaskini, isiwe umaskini tena taula yako kufua hufui, vipi, maana yake, unakuja una maji eti umaskini umezidi, hii hatari. Kwa hivyo, Mhe. Waziri ukija, huna haja ya kujibu nadhani umeshasikia.

Mhe. Mwenyekiti, halafu kuna suala hili limeandikwa kwenye ripoti la vijana ambao wamejisalimisha wenyewe, vijana 220 walikuwa wachapa unga, hawa vijana wako wapi na kama wamejisalimisha kweli, je serikali ina mpango gani kwa watu hawa. Kwa sababu kama wametubu wameona hii sio kazi, sasa sisi tunawafanya nini, lakini je kweli wapo, isijekuwa wanataka msaada tu basi.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, la baadae. Sasa hivi mji wetu unazungumzia habari ya Darajani *Corridor*, Michenzani kwamba kutajengwa maduka mazuri tu, wasi wasi wangu ni kwamba je mambo ya *parking* yatakuwaje. Sasa hivi ripoti hii inasema kituo kikubwa cha daladala kitakuwa Kijangwani, isijekuwa yale mambo yetu ya kishamba Mhe. Waziri unayajua, umechukua kigunia chako cha mahindi unakwenda kipandoni, umeshanunua vitu Darajani, umenunua vitu Michenzani unakwenda Kijagwani. Hii nadhani tutakuja kuwakaribisha tena watu wa mikokoteni. Je, tumejipanga vipi na huko tunakokwenda. Maana yake itakuwa maduka hayana maana, wakati mtu kipolo chake anakibeba juu ya kichwa anakwenda kungoja daladala Kijangwani.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, mimi natoka shamba maana yake hata Kiswahili chenyewe kinagonga. Kuna paka mweusi kazi yake kukusanya koa, nadhani tunamfahamu koa. Anakwenda kuchukua anakuja kuweka, anakwenda kuchukua anakuja kuweka hakuna mmoja anayemla. Lakini baadae akija hapana kitu.

Mhe. Mwenyekiti, kuna soko letu la Mwanakwerekwe tumejitahidi likawa safi, sasa tumejisahau tumehamia Fumba kwa matangazo, lakini watu wamerudi barabarani kama kawaida. Sasa isije ikawa ile habari ya Paka kitu kukusanya huku kumbe huku kunaharibika na mwisho wake anakosa mote. Kwa hivyo, naomba tu tusifikie hapo, ikiwa tunatangaza njia kwamba twendeni Fumba, twendeni Fumba. Lakini na Mwanakwerekwe nendeni tizameni Halmashauri, tizameni Manispaa na tizameni wizara, mambo karibu yanakuja yale yale.

Lakini la mwisho Mhe. Mwenyekiti. Bado sio la mwisho. Jambo ambalo ulisema kwamba liko chini ya mikono yako, kuna vijana wale wa KMKM, hili ulisema liko kwenye mikono yako. Sasa sijui umefikia wapi unaweza labda ukatupa ufafanuzi.

Mhe. Mwenyekiti, la mwisho kabisa nakuomba kwenye barabara za ndani wewe ndio muhusika mkuu. Mhe. Waziri tizama kwenye vichochoro vyote vya Unguja na Pemba, lakini usije ukasahau Kusini, kuna barabara bado zina vumbi. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nashukuru na mimi kupata fursa hii. Awali ya yote sina budi kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametujaalia uhai na uzima tukaweza kukutana mahala hapa. Lakini pia nichukuwe fursa hii kuwashukuru na kuwapongeza sana Mhe. Waziri, Naibu Waziri, watendaji wa wizara hii na Wakuu wa Mikoa wetu wote, Wakuu wa Wilaya wote, Wakurugenzi wa Halmashauri wetu wa Halmashauri wote, lakini na wajumbe wa kamati kwa kazi kubwa na nzuri ambayo wameifanya. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka nianze hapa kwenye vizazi na vifo. Mhe. Mwenyekiti, hapa kumetajwa vizazi na vifo lakini bado kuna vyeti vya ndoa na talaka hatuvitilii mkazo navyo ni vitu muhimu sana. Kwa hivyo, ningeomba, ingawa talaka sio jambo tunalolipendekea sana ambalo Mwenyezi Mungu amelichukia sana, lakini lina umuhimu wake linapotokea basi mtu aweze kupewa ile pasi yake ya talaka, kwa sababu isije ikatokea mtu huyo anaolewa mara kumi, kwa sababu hana uthibitisho wa kuwa ameachika. Kwa hivyo, ndoa ni muhimu sana awe na cheti chake lakini na talaka.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika majengo na ofisi za serikali ambazo hazina hati miliki. Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli niseme jambo hili ni la masikitiko sana na sijui uzito wake uko wapi. Mhe. Mwenyekiti, katika vituo vya afya 37 katika Wilaya ya Kati, basi kinaonekana ni kituo kimoja pekee cha Tunguu ndicho chenye hati miliki, hili ni jambo la kusikitisha sana. Lakini katika skuli 81 ambazo katika Mkoa wa Kusini kuna skuli 12 tu ndio zenye hati miliki. Kwa kweli jambo hili bado linahitaji juhudi kubwa za serikali, linahitaji mshikamano mkubwa au kiunganishi kizuri ambacho kitaweza kuyafanya majengo yetu haya yaweze kupata hati. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, katika Mkoa wa Kaskazini kuna skuli 74, lakini skuli 12 tu ndio zenye hati miliki. Kwa hivyo, hii haiko katika mfumo mzuri na jambao hili linasababisha sana kukosa kupatikana hati miliki linasababisha uvamizi wa eneo ambalo limeshatengwa kwa ajili ya shughuli fulani basi likaweza kuvamiwa kwamba haliko katika msingi mzuri wa

kudhibitiwa sehemu hiyo. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba sana kuwe na utaratibu mzuri serikali ifanye kazi katika hali ya mashirikiano ili jambo hili liweze kutatuka kwa haraka, maeneo yanayotengwa basi yaweze kuwa na hati miliki ili yaweze kudhibitiwa vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika suala zima la elimu ambalo mmeeleza hapa kwamba sasa mmeshusha ugatuzi. Sasa mimi Mhe. Mwenyekiti, niombe sana na nilitaka nijuwe sana kuhusu hizi *TC* ambazo sisi ndio tegemeo letu ambalo linaweza kuwalea sana walimu wetu na kupata ufanisi, kupata mafunzo wakaweza kupata ufanisi mzuri juu ya kazi zao. Mimi nilikuwa nataka kujua kwa sababu hapa nyuma niliwahi kuleta hata swali katika Baraza hili, kwamba walimu walitulalamikia kuwa hawaingiziwi fedha katika vituo vyao hivi. Sasa nilitaka kujua tu kwa huu mfumo wa hivi sasa ulivyo, ni vipi vituo hivi vinaweza kupata mafanikio juu ya kuwapatia mafunzo walimu wetu ili waweze kufanyakazi katika ufanisi mkubwa.

Mhe. Mwenyekiti, pia nilitaka kujua kwamba mlisema kuwa kuna upungufu wa walimu 95 katika Mkoa wa Kaskazini Unguja. Nilitaka kujua hivi sasa mmeshaajiri labda wangapi katika kupunguza kasi na kilio chetu hiki ambacho tunacho.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile niende katika Mabaraza haya ya Miji na Manispaa zetu. Pia hapa mmetueleza katika Mabaraza haya kunahitajika sana wataalamu, na ni kweli huwezi kufanya kitu bila ya kuwa na mtaalamu ambaye anakijua vizuri ili tukaweza kufanikiwa vizuri.

Sasa mimi nilitaka kujua labda hatua za awali ambazo zimeshachukuliwa katika kuwapata wataalamu hawa ambao wataweza kuyasaidia Mabaraza yetu ya Miji, lakini hata Manispaa zetu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi mchango wangu ulikuwa sio mkubwa nilitaka kujua hayo. Lakini nasema naiunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja na nawatakia kila la kheri na ufanisi mzuri katika kazi na majukumu yetu ya kila siku, ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Panya Ali Abdalla kwa mchango wako wa kumalizia. Waheshimiwa Wajumbe, naomba nitangazie kwamba wawakilishi kutoka Pemba mara baada ya kuahirisha kikao hiki, mnatangaziwa mubaki hapa na Mhe. Waziri Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, mubaki katika ukumbi huu.

Waheshimiwa Wajumbe, hadi hapa naomba niahirishe kikao hiki hadi saa 11:00 jioni panapomajaaliwa.

(Saa 7:00 mchana kikao kiliahirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11.00 Jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia ripoti hii ya utekelezaji ya Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ.

Mhe. Naibu Spika, awali ya yote nimshukuru sana muwasilishaji wa ripoti hii Mhe. Waziri kwa uwasilishaji wake katika muundo wa bango kitita ambao kwa kweli pamoja na ukubwa lakini umetufanya twende kwa haraka zaidi, lakini vile vile nichukue fursa hii kuweza kuwashukuru na kuwapongeza sana kamati kwa kuweza kuwasilisha na wao ripoti yao, lakini kwa heshima kubwa niwashukuru Wajumbe wote ambao wameweza kuichangia ripoti hii ya utekelezaji.

Mhe. Naibu Spika, mijadala hii ya utekelezaji ilianza tokea ijumaa iliyopita na hii kama sikosei ni Wizara ya nne na kwa kipindi chote hicho kwa kweli nilikuwa sijachangia leo hii nimependa nichangie ripoti hii ya utekelezaji katika Wizara hii, nilikuwa sijachangia kwa sababu Mhe. Naibu Spika, huu ni utaratibu mpya ambao Baraza umeanzisha kwa hivyo nilikuwa najifunza mijadala mitatu ambayo imepita. Mhe. Naibu Spika, utaratibu huu ni utaratibu mmoja mzuri sana kwa hivyo nilipongeze sana Baraza la Wawakilishi hususan watendaji kwa kuweza kubuni utaratibu huu wa Wizara kuwasilisha ripoti za utekelezaji baada ya maoni au ushauri wa kamati na naomba utaratibu huu uendelee.

Mhe. Naibu Spika, utaratibu huu unaongeza ufanisi unaongeza uwajibikaji, lakini vile vile kamati inapata kusimamia vizuri sana matumizi ya fedha za umma ambazo zinapitishwa katika vikao vya bajeti, nimeridhika sana na majibu ya utekelezaji wa Mawaziri ambao wamewasilisha hapa kwa kweli wamejitahidi kwa sababu ni mfumo mpya hata ukiangalia ule uandishi au ile *format* ya uwasilishaji inatofautiana kwa sababu ni kitu kipya, lakini ningependa sana wawe na *format* inayofanana hapo mwakani.

Mhe. Naibu Spika, wasiwasi wangu ni mmoja tu katika utaratibu huu kwamba majibu ambayo yametolewa katika Wizara karibu zote ambazo zimewasilisha ni majibu ambayo kamili na ukamilifu wake wakati mwengine baadhi ya wajumbe walikuwa wanatia wasiwasi. Kwa hivyo mimi kwa maoni yangu kwamba kile ambacho Mawaziri wanakiwasilisha kwetu basi kiwe ni halisi kwa sababu wajumbe watapaswa kuhoji, licha ya kuhoji ya kwamba hii sasa ripoti hii inakuwa ni *reference* kwa kamati pale ambapo itafuata utekelezaji kujiridhisha, sasa iwapo kama kuna hoja ambazo sio halisi maana yake Wizara inayohusika itapaswa kuweza kujibu pale ambapo kamati imegundua imekuwa sivyo na ripoti ya utekelezaji. Kwa hivyo niwaombe sana Mawaziri na wao kuweza kujiridhisha na majibu ya utekelezaji katika taasisi zao ili kuweza na kuleta taarifa ambazo kwa hapa nazo zitakuwa za uhakika zaidi.

Mhe. Naibu Spika, sasa nielekee katika ripiti hii ndani hapa mimi nilikuwa nataka kuelewa katika ukurasa wa tatu kwenye hoja ya saba, Kamati ilishauri Serikali kuharakisha ujenzi wa Kituo kiku cha daladala cha Kijwangwani, ujenzi wa kituo hichi umezungumziwa zamani na juzi juzi nilipita kuna kifusi ambacho karibu mwezi mmoja na nusu kipo, sasa mimi nilitaka kujua tu kwamba ujenzi wa kituo kile ni lini hasa wananchi wategemee. Kama michoro yake tayari au bado lakini wananchi wanakihitaji sana kwa sababu msongomano wa dala dala katika eneo la Michenzani imekuwa ni kero kubwa kwa wananchi.

Lakini vile vile Mhe. Waziri atakapokuja basi aweze kutupa utaratibu kwa sababu wananchi wana wasiwasi kutakuwa na utaratibu gani mtu anayetoka Mwera anataka kufika Darajani, daladala inamfikisha Kijangwani kwanza halafu abadilishe au vipi, mtu anatoka Pemba kashuka meli ana mizigo yake afuate dala dala Kijangwani au Darajani, sasa ni vyema sana ingawa kituo hakijajengwa lakini utaratibu huu wananchi wanaudadisi sana kwa pale sehemu ambayo imekaa.

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo nije katika ukurasa wa 4 katika hoja ya 10 katika Mkoa wa Mjini Magharibi. Nichukue fursa hii kwanza kuweza kuwapongeza watendaji wa Mkoa wa Mjini Magharibi hususan Mkuu wa Mkoa mwenyewe kwa umahiri na ushujaaa wake katika kusimamia majukumu yake, kubwa zaidi katika utekelezaji wa kupiga vita suala zima la madawa ya kulevya na kero nyengine ambazo zinachangia vitendo ambavyo vinakwenda kinyume na maadili ya Zanzibar. Tuna haki ya kumpongeza na Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Mjimi Mgharibi kwa juhudi anazozichukua lakini vile vile kwa kuanzisha ile program ya mimi na wewe kwa kweli inaonesha program ile ikiendelea basi tutapiga hatua kubwa sana ya maendeleo.

Mhe. Naibu Spika, katika suala la madawa ya kulevya katika uperesheni ambazo zinafanyika mimi naziunga mkono sana kwa sababu tuna maeneo mengi, tuna vikundi vingi vya vijana ambavyo wanajishughulisha na uuzaji au utumiaji wa madawa ya kulevya, kwa hivyo naipongeza sana Serikali ya Mkoa pamoja na mikoa mingine kwa juhudi ambazo wanazichukua katika kuona tatizo hili linaondoka. Mhe Naibu Spika, niombe tu kwamba vikundi hivi ambavyo vinashughulikia uperesheni hizi wakati mwengine inatumia nguvu za ziada na unaweza ukasema kwamba pengine wanachukua sheria mikononi, inatokea wakati mwengine wanapopiga *ambush* inawezekana wakaingiza waliomo na wasiokuwemo, sasa jambo hili wakati mwengine linaweza likapoteza imani kwa wale ambao hawakuhusika na suala hili. Niombe sana tu kwamba vijana wetu hawa ambao wanashughulikia na operesheni hizi basi wawe makini katika kuona kwamba wale wanaohusika tu ndio ambao wanawashughulikia, na suala la vipigo wakati mwengine linaweza likawa linachangia katika kuwafanya vijana wetu hawa baada ya kurekebishika lakini kuwa masugu zaidi.

Mhe. Naibu Spika, niseme hili kwa sababu kuna tukio ambalo limetokea ambalo linalalamikiwa sana na wananchi ambalo limetokea katika jimbo langu la Magomeni, kijana ambae anapita kuelekea msikitini akakumbwa na dharuba hii na ikapelekea mguu wake kuvunjika na hivi sasa kwa kweli imebidi kuweza kutumia gharama kubwa wakati yeye hakuhusika katika suala la namna hii, lakini baya zaidi wahusika wale wakachukuliwa na kwenda kutupwa sehemu ya mbali.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa umebakiza dakika tatu.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Kwa hivyo hali ile inapelekea kwamba sheria zile baada ya vijana wale kuwapeleka katika vituo inakuwa imekiukwa, kwa hivyo niombe sana wale vijana wanaokumbwa na matatizo haya basi wapelekwe katika vituo vinavyohusika kisheria ili waweze kufunguliwa mashitaka kwa makosa ambayo wamekutwa nayo.

Mhe. Naibu Spika, sasa nije katika suala zima la Mikoa na Wilaya hapa kuna suala hili la vijana wa mabaraza ya vijana, imeelezwa hapa kwamba tayari baadhi ya vijana wameanza kujishughulisha na uzalishaji baada ya kupatiwa elimu, ambao hivi sasa wanajishulisha na ushoni, kilimo, uzalishaji sabuni na kadhalika. Ningependa tu Mhe. Waziri atakapokuja atwambie ni mabaraza ya Wilaya gani ambayo yameweza kupata fursa hii ili na sisi tuweze kujiridhisha kwa sababu ni jambo zuri lakini utelelezaji wake, lakini vile vile suala la masoko liko vipi kwa sababu vijana wengi wanasikitika hata wakiwa na miradi maana yake masoko yanakuwa ni magumu kwao.

Mwisho nimalizie na suala zima la Bodi za elimu Mkoa wa Kusini, kamati ilishauri juhudi za pamoja zifanyike kati ya wazazi na walimu na uongozi wa Mkoa kuinyanyua sekta ya elimu, hapa Mkoa umesema kwamba kwa kupitia bodi za elimu na kamati za skuli husika tumeendeleza kuelimisha jamii. Mhe. Naibu Spika, najiuliza kwamba hizo bodi za elimu bado zipo, kwa sababu bodi za elimu zilikuwepo nakumbuka katika kipindi kama sio cha Mhe. Haroun alipokuwa Waziri wa Elimu zilikuwa na uhai lakini hivi sasa naona uhai wake ni mdogo, kwa hivyo nilikuwa nataka kuelewa kwamba bodi hizi na zipo kisheria na zinafanya kazi vipi.

Kwa mfano kwa tatizo la elimu Wilaya na Mkoa wa Kusini inaonekana kwamba mazingira ya kujifunza katika Wilaya ya Kusini yawe mazuri zaidi kuliko wilaya nyengine, hakuna mikondo miwili ambayo wanafunzi katika kujifunza mkondo ni mmoja tu lakini hata idadi ya wanafunzi katika darasa inakuwa ni ndogo. Lakini la kushangaza maendeleo ya elimu yanashuka siku hadi siku mpaka takwimu za mwaka jana Wilaya ya Kusini Kiwilaya katika Mitihani ya Form II basi ni ya 11 na ya mwisho. Sasa sijui kama hizi bodi za elimu zipo na zinafanya kazi gani na keshokutwa ni mtihani, kwa hivyo atueleze bodi ya elimu ya Wilaya ya Kusini ipo na inafanya kazi zipi hivi tukiona kwamba maendeleo yanadidimia kila siku.

Lakini juzi tu kuna taarifa kwamba Skuli ya Ukongoroni au Charawe katika mitihani ya darasa la 4 darasa lina wanafunzi 19 lakini ni miongoni mwa skuli 10 zilizofanya vibaya….

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa muda wako umekwisha.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Sasa Mhe. Naibu Spika, akija Mhe. Waziri atuwekee wazi juu ya hili na baada ya hayo nishukuru sana kwa nafasi uliyonipa naunga mkono hoja, asilimia mia kwa mia katika ripoti hii. Ahsante sana Mheshimiwa.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe kazi tuliyonayo mbeleni ni kubwa kuna taarifa nyengine ambayo tunatakiwa tuipokee leo tuimalize leo, sasa nina wachangiaji wengine watano, kwa hivyo nina hakika kwamba kama tutaendelea kuchangia kwa watu hawa watano ina maana hapa tunaweza tukaongeza muda usiku huu wa leo. Kwa hivyo ningewaomba sana watakaochangia atakuwa Mhe. Raza, na nitampa bahati Mhe. Bahati Khamis Kombo wa Chaani waliobakia walete kwa maandishi.

Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammediali: Mhe. Naibu Spika, Waheshimiwa Wajumbe wenzangu awali ya yote napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, pamoja na wazee na wenzangu woote kwa dua zao na neema zao pamoja na wazee wangu nasema hujafa hujaumbika. Mhe. Naibu Spika, nishukuru vile vile Baraza lako kwa kunipa mashirikiano mazuri katika kipindi ambacho Mwenyezi Mungu kila binaadam atampa mitihani, lakini mwisho Mwenyezi Mungu anatwambia wape habari nzuri wanaosubiri.

Mhe. Naibu Spika, awali ya yote nishukuru Wizara inayohusika na Tawala za Mikoa kuanzia Waziri, watendaji wake, Katibu Mkuu, viongozi katika Wizara, watendaji wakurugenzi pamoja na Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Baraza la Manispaa, Madiwani wote kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kuteleza ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Mhe. Naibu Spika, mimi nilikuwa na mawili tu katika kutoa mchango wangu ninachosema kwamba ukiona moyoni mdomo utasema, mimi nilikuwa makini sana katika kusikiliza hoja za wenzangu mbali mbali niwashukuru kila mmoja ana uhuru wa kusema na nchi yetu kila mmoja ana uhuru wa kuabudu, lakini niseme tu kwamba tumekaribisha vitega uchumi vya utalii na moja katika njia yetu ya kujipatia mapato. Lakini yote katika utalii utamaduni wa Zanzibar nafikiri tuwe tunaelewa.Tumepokea kwa Mtume Muhammad (S.A.W.) anaposema kwamba hata nendeni China nendeni kachukueni yale mazuri yale mengine ambayo sio utamaduni wetu tuyawache. Sasa hili suala la utamaduni wa kuleta vitu ambavyo vinaweza kugusa wananchi katika suala la utalii nafikiri Wizara zinazohusika za Vikosi pamoja na Wakuu wa Wilaya na Wizara ya Utalii ikawa makini sana, nasema Zanzibar ni suala ambalo *we are cosmopolitan* lakini lazima tutizame mazingira ya wananchi wetu.

Kwa sababu vitu hivi hata huko nje vinakuwa na *holl* maalum haziwi za mitaani wala hazikeri wananchi, sasa uzuri wa jambo lazima tuwe makini na sisi sote kwamba tuna vizazi vijavyo vinakuja, wajukuu wetu, watoto wetu ambao watakuja kuturithi tutizame utamaduni mkubwa. Kweli utalii tunautaka lakini kuna vitu hivi ambavyo vinakuja unasema kwamba mifano unatoa nje, lakini tuna utamaduni na Mtume ameshatwambia sasa mimi utalii tunaukubali tunaupokea moja katika ilani ya chama. Lakini suala hili ambalo linaleta vitu vya *pool* lazima tutizame mazingira ya wananchi kwamba hili jambo linakuwa na *holl* maalum, lakini leo unaingia katika vitu Mkoa mzima wa Kaskazini au sehemu kubwa wananchi na watoto wetu ule utamaduni au kero inakuwa inawapata sasa lazima tuwe makini, tuwe na hekima, busara, usikivu mimi Mhe. Waziri nakuomba sana hili suala la kupata kipaumbele sauti ya wananchi lipewe kipaumbele katika mazingira yetu yote ya utalii au mengi ambayo tunataka kufanya zitizamwe sehemu zote mbili.

Mhe. Naibu Spika, mimi naona bado Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Masheha ni vizuri kukaa kwa pamoja kutizama *when we have a problem, where to find the solution and then what we say what is next,* lakini kuliko kuingia na vitu ambavyo vitaweza kutuharibia utamaduni wetu. Mimi nasisitiza kwamba mambo kama haya lazima viongozi wakae kitako tutizame kuna vitu ambavyo vitagusa wananchi. Basi mimi naona bora mambo mengine tuwe tunavumilia.

Mhe. Naibu Spika, hata hili suala la Mahoteli ambazo za Makuti, hapa Waziri anajitahidi sana katika vikosi, tunahitajia magari mengi lakini nataka wakae Mawaziri wanaohusika. Hivi hoteli za mabanda ya makuti nafikiri yamepitwa na wakati. Mabanda ya makuti yakiingia moto wakati huo utalalamika utasema bwana zima moto iko wapi, na nyenzo ya zima moto ni ukusanyaji wa mapato.

Naomba Serikali ya Mapinguzi ya Zanzibar tutizame kwamba haya mahoteli ya makuti naona yatatugharimu sana, ardhi yetu ni mali, kuna watu duniani wapo tayari kuja kuweka *investment* ambayo itaweza kusaidia. Mimi naona Wizara zinazohusika, Wizara ya Utalii, Mheshimiwa kaka yangu maalim Rashid na Waziri wakae walione, hilo la kwanza.

Mhe. Naibu Spika, jengine nakuja suala la mapato ya *parking* hizi. Hivi Manispaa, Wakurugenzi wote, nataka niseme kwa kuwambia Wazanzibari kwa kweli katika mambo ambayo kodi iko ndogo sana katika Afrika Mashariki na ya Kati na Tanzania Bara basi ni Zanzibar. Rais ametupa upendeleo maalum sana kwa wananchi wote na wafanyabiashara. Sasa tusisingizie leo *parking* Sh. 1000/= una gari ya milioni 20 sasa *you can afford twenty millions, ten million,* halafu elfu moja mimi naona bado ni kidogo. Sasa tujenge utamaduni Wazanzibari wote wa kulipa kodi, nafikiri ni jambo zuri sana. Wazanzibari na wafanyabiashara tuwe na utamaduni wa kulipa kodi.

Mhe. Naibu Spika, katika suala la mazingira yote nasema bado Manispaa bado sehemu zote zinazohusika suala la *parking car* litizamwe. Kama leo Mheshimiwa ukenda Mau pale watu wanakwenda Mabenki kutoa milioni 20, 50, hakuna mtu anayekwenda kutoa 5,000/- utakuta magari yamepangwa kuanzia Madema mpaka barabara ya pili, kwanza wanasababisha ajali. Lakini kila mmoja kaona pale hakuna *parking*.

Mimi natoa wito kwa Baraza la Manispaa kila sehemu wanapaona waweke *parking* ili tuweze kupata mapato. Lakini mapato hayo yatumike pahala ambapo yamekusudiwa. Kwa sababu sisi tutarejea hapa tutasema barabara hii Mhe. Waziri ulituahidi Halmashauri itatengeneza barabara fedha hakuna, kwa sababu kila tunachokipata ndicho tunachokitumia. Mimi nafikiri niombe bado Baraza la Manispaa nataka nihakikishe kwamba lazima tuwe na utamaduni wa kulipa, tubadilike lakini Baraza hizi zote za Manispaa wana uwezo wa kukusanya fedha nyingi sana.

Mhe. Naibu Spika, Dar-es-Salaam tu hapo ukisimama pale pale askari anakutolea risiti yako 30,000/= hapa tunakuja kupiga kelele, Wizara ya Mawasiliano, Utalii, watasema barabara zao ndani mbovu, Halmashauri, sasa mimi nafikiri kuwepo na utaratibu maalum wa kuweza kujifunza.

Mhe. Naibu Spika, mimi juzi nilikuwepo Dubai na ndugu yangu Almasi na Ruba Mkubwa, Wallahi, Bilahi, Talahi, Dubai pale kulikuwa *Deira Red Light*, nilikuwa na wenzangu kama 27 basi tulipoona hamna magari tulikata tu, basi ile kukata tu kulikuwa kuna maaskari ambao wamevaa unifomu zao za kawaida nilikuwepo na mimi, tulikumbwa sote tukawekwa sehemu moja, tukaambiwa haya toweni vitambulisho. Tukachukuliwa tukapelekwa Polisi kwa bahati mimi nikatoa kitambulisho changu, kilichonisaidia kile kitambulisho changu wakanambia sawa tunakuheshimu lakini kesho uwende *Deira Police Station* ukalipe dirham 300, umekata tu. Sio kama wenzetu, lazima kuwepo utaratibu wa sheria.

Lakini mfanyabiashara kama kina Raza tutaweka gari njiani tunaweka foleni kubwa tuwekeni utamaduni wa kulipa elfu 50, laki kila mmoja ataweka akili yake sawa. Mapato yapo mengi nchi hii, ukitaka kumchinja nyani usimtizame uso wake. Hayo ndiyo yaliyonifika mimi Dubai wale wengine wote wakachukuliwa sio kama Serikali ya Dubai lakini leo utaratibu wa sheria. Lakini leo tizama magari yote ukenda Marikiti pale kila mmoja kaweka gari yake ina thamani ya milioni thamanini ile gari. Sasa nafikiri Mhe. Waziri kama kuna utaratibu wa sheria tupitisheni sheria humu gari ikisimama sehemu yeyote awe Raza awe Pandu awe Jecha Shilingi 50,000/=. Haya ndiyo yatasaidia barabara za ndani.

Mhe. Naibu Spika, Rais wetu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohammed Shein ni msikivu ana hekma ana busara na naishukuru serikali nzima kwa utamaduni tuliokuwa nao, lakini bado tuwe na utamaduni wa kukusanya mapato.

Kwa haya machache Mhe. Naibu Spika, niishukuru na naiunga mkono Wizara nzima kwa asilimia mia kwa niaba ya wananchi wangu wa jimbo wa Jimbo la Uzini, lakini bado tuwe na utamaduni wa kulipa. Manispaa waanze mikakati yao ya kuweza kukusanya kila sehemu, waweke utaratibu wa kuweza kupata fedha. Ahsante sana.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, kuhusu utaratibu.

Mhe. Naibu Spika: Kuhusu utaratibu.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: 63, Kanuni 147 kutenga kando kanuni, sijui niisome Mhe. Naibu Spika, au ...

Mhe. Naibu Spika: Unataka nini nambie unachokitaka.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Tunachojadili hapa ni Wizara muhimu kwa wananchi na kila kitu ...

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Jaku Hashim, nimeshatoa maamuzi kwamba mchangiaji wa mwisho atakuwa Mhe. Bahati Khamis Kombo, sitaki ulalamishi, tunaendelea. Mimi nafanyakazi kutokana na muda nilionao, nafanya kazi kutokana *order paper* niliyonayo. Nimesema wale waliobakia, kuna wengine watano wamebakia usifanye mazungumzo yakawa marefu tukapoteza muda. Wachangiaji watano waliobakia walete kwa maandishi, maandishi yako yatafika, mawazo yako yatafika kwa Mhe. Waziri hata ukiandika kwenye

karatasi. Lakini kama una majadiliano zaidi ya hayo mimi sasa hivi sitaki kusikia kwa sababu mimi nakwenda kwa *order paper* niliyonayo na muda ambao nimepewa. Mhe. Jaku Hashim kaa tunataka tuendelee. Mhe. Bahati.

Mhe. Bahati Khamis Kombo: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kwa kunipa fursa hii ya kuweza kuchangia machache laasiri hii. Kwanza kabisa nichukue fursa hii ya kumpongeza Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi pamoja na Kamanda wake Pamoja na Mkuu wa Wilaya wake kwa juhudi kubwa wanazozichukua kupambana na vitendo viovu ambavyo hata leo nimemsikia akizungumza asubuhi kwamba tayari jana wamekamatwa watu ambao wana vitendo viovu. Pia niendelee kumpongeza sana Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba kwa kupambana na magendo ya karafuu.

Mhe. Naibu Spika, niendelee moja kwa moja katika ukurasa wa 7 katika maoni Nam 12. Hapa nimeona kwamba Kamati imeshauri kuendelezwa kwa Mabaraza ya Vijana ili kuwezesha vijana kupambana na mazingira yanayowazunguka kifikra na kiuchumi ili kuachana na mawazo potofu ambayo kikwazo cha maendeleo. Hili ni jambo zuri sana na mimi nawaunga mkono sana Kamati hii kwa ushauri huo ambao wameutoa.

Mhe. Naibu Spika, nimetaka kujua tu kwa sababu hapa pana maneno yanasema katika utekeleza Mabaraza ya vijana yameanza kujishughulisha na uzalishaji baada ya kupatiwa elimu. Mabaraza hayo yameanza kufanya shughuli za ushoni, kilimo, uzalishaji wa sabuni, dawa za kusafishia vyoo, vigae, shampuu, mafuta ya mgando, siki na shughuli za ufugaji. Hapa nilitaka kujua kama ni Wilaya gani ambayo tayari mabaraza haya wameshafaidika na mambo haya.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea kidogo mbele Mabaraza ya Miji Kamati inashauri kuwa Wakuu wa Mabaraza ya Miji Pemba waajiri kwa muda wataalamu kwa mikataba kwa mujibu wa mahitaji yao yalivyo kama wanavyofanya Unguja.

Mhe. Naibu Spika, mimi ningeshauri ni vyema wakaajiri moja kwa moja na sio wa muda kwa sababu tukiendelea kila siku kutafuta wataalamu wa muda kwa kweli baadaye itakuwa ni kikwazo, lakini ni vizuri tukapata wataalamu ambao kuwa ni wa kudumu.

Mhe. Naibu Spika, nikenda mbele kidogo katika ukurasa 11 Kamati inashauri mabaraza kuanzisha mfumo wa uajiri kwa njia ya mkataba, hii itasaidia sana kuziba maendeleo ambayo kuna upungufu wa wataalamu. Hapa Mhe. Waziri naomba atakapokuja atwambie kwamba hapa kuziba maendeleo au kuziba mapengo ambayo kuna upungufu wa wataalamu.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea mbele katika ukurasa Nam. 12 Kamati imeona kuwa Mabaraza ya Miji Pemba yameshindwa kukusanya kodi zake vizuri kutokana na kutoshirikisha Mahakama. Tuseme kwamba Mahakama ina majukumu mengi sana. Mahakama kwa kweli tunaibebesha mzigo mkubwa sana. Wakati huu tulionao sasa hivi ni vyema kwamba Mabaraza ya Mji yote yakapatiwa Mahakama zao na vile vile yakapatiwa askari wao maalum, ili kuondosha tatizo hili la kutokushirikiana vizuri baina ya Mahakama zetu na Mabaraza ya Mji yaliyoko Pemba.

Mhe. Naibu Spika, katika kifungu hicho hicho namba 28 niende moja kwa moja katika utekelezaji. Mabaraza ya Mji yamechukua hatua ya kuzungumza na uongozi wa Mahakama ili kujua changamoto zinazowakabili taasisi hiyo na kuzichukulia hatua ya utatuzi na mabadiliko yameanza kuonekana kwa upande wa Baraza la Mji Mkoani, jumla ya kesi 62 zimeshashughulikiwa na kupatiwa ufumbuzi.

Mhe. Naibu Spika, kwa uzoefu wangu ambao kuwa ninaoujua katika Baraza letu la Mji Mkoani pana tatizo na hizi kesi ni nyingi. Hapa sasa nilitaka kujua kwamba kesi hizi zimepatiwa ufumbuzi hao ambao wanaohusika wamepelekwa Mahakamani au wamepatiwa ufumbuzi wa kunyamaza kimya na halikuwa lolote na wala chochote.

Mhe. Naibu Spika, sasa hivi tunakwenda na wakati na wakati tunaokwenda hatwendi kwa ajili ya kuficha mtu ni lazima tufanye kazi kwa uwazi ili tuendelee kuleta maendeleo katika Mabaraza yetu ya Mji. Namuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa atuweleze kwamba hizo hatua ambazo zimechukuliwa na ni adhabu gani ambazo wamepewa.

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako nakushukuru sana, ahsante sana na mimi naunga mkono ripoti hii kwa asilimia 95 tano namuomba Mhe. Waziri atakapokuja kunipa majibu *Inshallah* tutakuwa pamoja.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana nakushukuru Mhe. Bahati sasa tumpishe Mhe. Waziri Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ. Karibu Mheshimiwa.

Mhe. Waziri Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika, kwanza nataka nikushukuru sana kwa kunipa ruhusa ya kuweza kuja kutoa ufafanuzi kwa baadhi ya mambo machache sana ambayo Waheshimiwa Wajumbe wamepata nafasi ya kujadili na kuchangia utekelezaji wa maagizo, ushauri na maoni ambayo yalitolewa na Kamati ya Katiba, Utawala Bora na Idara Maalum za SMZ.

Mheshimiwa Wajume waliochangia kwa kusema ni Wajumbe 9 nao ni:

1) Mhe. Machano Othman Said - Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum.
2) Mhe. Ali Suleima Ali
3) Mhe. Nadir Abul-latif Yussuf Al-Wardy
4) Mhe. Simai Mohammed Said
5) Mhe. Abdalla Ali Kombo
6) Mhe. Panya Ali Abdalla
7) Mhe. Rashid Makame Shamsi
8) Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali
9) Mhe. Bahati Khamis Faki

Waliochangia kwa maandishi ni:

1) Mhe. Ussi Yahya Haji
2) Mhe. Masoud Abrahman Masoud
3) Mhe. Mtumwa Peya Mbarouk
4) Mhe. Miraji Hamis Mussa
5) Mhe. Suleiman Sarahan Said
6) Mhe. Said Soud Said
7) Mhe. Hamza Hassan Juma

Hao ndio Waheshimiwa waliochangia nataka nichukue fursa hii kuwapongeza wote walioichangia taarifa hii ya utekelezaji ya maagizo ambayo tumepewa na Kamati.

Mhe. Naibu Spika, nataka nizingatie maelekezo ambayo umenipa, kwamba kwanza nataka niwaambie Waheshimiwa Wawakilishi tulichofanya serikali kupitia Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum ni kuja kuleta taarifa ya utekelezaji ambayo tumeagizwa na Baraza hili la Wawakilishi kupitia Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi kwa mujibu wa kanuni. Nisingefikiria kama ingezuka mijadala mipya kwa sababu nilichofanya ni kuja kutekeleza wajibu na kutimiza matakwa ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Naibu Spika, yapo mambo ambayo Waheshimiwa Wajumbe wameyaleta naona hizi ni kama hoja mpya amazo sidhani kama zitakuwa zinaenda sambamba na utaratibu huo ambao Mhe. Rashid Shamsi ameuweleza kwamba ni utaratibu mzuri na sisi kama serikali tunasema kwamba utaratibu huu ni mzuri na uendelee kwa sababu unatuweka sana katika uwajibikaji wa serikali. Niwaombe Waheshimiwa Wajumbe yale maoni yao yate ambayo wameyatoa na sitopata nafasi ya kuweza kuyatolea ufafanuzi wajuwe kwamba haya ni sehemu ya mambo ambayo tutakwenda kuyapatia ufumbuzi na hatimaye tupo tayari kuweza kuyaeleza. Lakini kutokana muda mambo mengine nayaona ni mapya kabisa yaliyojitokeza.

Mhe. Naibu Spika, maoni yote ambayo tunamshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati kwa kuendelea kushirikiana na sisi pamoja na Kamati nzima pamoja na Wajumbe wote wa Kamati kwa ushauri ambao wametupa na ripoti hii kabla ya kuja hapa tulipitisha kwenye kamati yake na bahati nzuri wametupa baraka wa kuileta mbele ya Baraza hili Tukufu na yote ambayo wametushauri tumeweza kuyafanyika kazi na yake ambayo wametushauri katika kamati kwasababu tuko pamoja tutaendelea kukumbushana na kuweza kuyatolea ufafanuzi.

Mchangiaji wa pili Mhe. Ali Suleiman Ali alipongeza na hasa hasa alimpongeza Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Mjini lakini kwa jumla aliwapongeza na wakuu wa Mikoa na Wilaya nyengine na jambo hili limefanywa sana na waheshimiwa takribani wote waliopata nafasi ya kupongeza kwa hiyo nazipokea pongezi hizi kwa niaba yao, vile vile amepongezwa sana Mhe. Rais mwenyewe amezikia pongezi na mimi niwapongeze waheshimiwa wajumbe kwa kuwapongeza au kwa kutupongeza sote.

Limezingumzwa suala la kuwasaidia Mabaraza ya Manispaa ya Magharibi 'A' na Magharibi 'B' kuhusu vifaa, Ofisi yangu inayo mkakati na tayari imeshatengeneza *program* kwa ajili ya kuweza kuyasaidia Mabaraza haya ya Mji kwa utaratibu wa

mgawanyo wa mali na madeni katika Mabaraza ya Mji matatu Mabaraza ya Manispaa ili kuona kwamba tunaondoka na hili na tatizo la Mabaraza ya Manispaa ya Magharibi 'A' na Magharibi 'B', hasa kwenye utaratibu wa kuwapatia magari uko mpango huo utakapokamilika basi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kupita Kamati yetu ya Katiba, Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum mtaweza kupata taarifa lakini tunao mpango wa kuyasaidia Mabaraza hayo.

Amezungumzia pia suala la hili limezunguzwa na baadhi ya Waheshimiwa wengine suala la utambuzi la watu wenye ulemavu jukumu hili pia wapewe Masheha wa Mabaraza au Wilaya ya Magharibi 'A' na Wilaya ya Magharibi 'B', ninachotaka kusema kwamba mpango huu ulikuwa kwa nchi nzima, Masheha wote wamepewa taaluma hii na wamepewa taarifa hii ili kuwatambua watoto wenye ulemavu ili Serikali iweze kupanga Mipango ya kuweza kuwapatia haki za msingi.

Mchangia wa tatu alikuwa Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf ambaye naye ametupongeza na pongezi tunazipokea na ni kweli yeye ni mjumbe wetu wa kamati lakini tunatambua wakati wa kujadili taarifa hii yeye alikuwa safarini kikazi tunambua hivyo na ameunga mkono mambo ambayo yamezungumzwa na kamati na hata kumalizia kwake ameunga mkono sana.

Amezungumzia sana suala la mashoga na wengineo, nia ya Serikali ni kukomesha uovu ndani ya nchi yetu. *(Makofi)*Kwa hivyo Serikali inashukuru sana kwa maoni na ushauri ambao tunapewa na wajumbe wa Baraza hili la Wawakilishi juu ya kupambana na uovu. Serikali kwa kupitia Mkoa wa Mjini lakini na Mikoa Mengine itaendelea na makakati huu ili kuhakikisha maovu hayaendelei ndani ya nchi yetu.

Alizungumzia pia matatizo ya ardhi na waheshimiwa wengine wamezingumza kwa kweli Serikali kupitia Mikoa na Wilaya tuna mikakati maalum wa kupambana na matatizo haya na kwa wale viongozi ambao wanajuhusisha na mambo haya basi wito ulishatolewa na Mhe. Rais kwamba tuachane na tabia hii kwa sababu wakati wa kuchuka hatua hatoheshimika mkubwa kwa ukubwa wake kwa sababu ya maovu anayoyafanya, nakushukuru sana Mhe. Narid kwa kutumbusha na kuwakumbusha wahusika wote.

Mhe. Nadir pia alizungumzia mchango wake ambao aliutoka kwenye bajeti ya wizara hii au ofisi wakati wa mjadala kuhusu vielelezo vya magari ya *fire*, nataka nimthibitishe kwamba vielelezo hivi tulitakiwa tuviwasilishe kwenye Kamati ya Bajeti ya Baraza la Wawakilishi na ofisi yangu ilichukuwa hatua ya kuzikabidhi ili kamati ya bajeti, iwe Balozi wa kuweza kuliarifu Baraza juu ya vielelezo vile na hatukudharau lakini kwa sababu yeye ni mjumbe wa kamati vile vile hatua shaka wala tatizo vilelezo hivi kuweza kuviwasilisha kwenye Kamati ya katiba kama alivyosema yeye mwenyewe.

Swali la kodi na wajumbe wengine wamelichangia hili na nadhani nikimjibu Mhe. Nadir na waheshimiwa wengine nitakuwa nimetoa ufafanuzi. Suala la kodi ni kweli kama unavyoelewa kwenye bajeti iliyopita Serikali haikupandisha kodi ya namna yoyote ile isipokuwa iliweka mfumo na kuweka ufafanuzi juu ya zile kodi. Kwa upande wetu Serikali za Mitaa maana nakusudia Mabaraza ya Manispaa pamoja na Mabaraza ya Mji na Halmshauri tulichofanya sisi ni kuainisha aina ya huduma ambazo sisi tunatoza ada

na hizo ziko kwa mujibu wa sheria na kanuni ambazo tumezitunga na tuna hakika ada hizi hazitawakwaza wananchi kwa sababu ada hizi tunapoziweka tunakubaliana kwa mujibu wa sheria ya fedha za umma na sheria yetu namba 7 ya mwaka 2014 ya Serikali za Mitaa tunakubaiwa na Waziri husika wa Fedha ili kuona kwamba hatuleti muingiliano na kupandisha kodi kiholela.

Kwa hivyo nimtoe hofu Mwakilishi wa Wananchi wa Chaani kuhusu suala hili kwani Taasisi zetu kwanza ni taasisi ambazo zinatoa huduma hazifanyi biashara kwa hivyo hata ada tunazotoa na kwa ajili ya kutoa zile huduma kwa hivyo naomba waheshimiwa wajumbe waelewe hilo na hatutofanya kwa kuwakandamiza wananchi wanyonge bali tunafanya kwa maslahi ya wananchi wetu.

Mhe. Simai Mohammed Said alizungumzia suala la mfumo wa usajili kuingia katika mfumo wa *electronic* na akataka kujua tunaingia tu kwenye *computerize* au mkonga kama nilivyosema juzi tunaingia katika mfumo mpya wa usajili wa matukio ya kijamii. Hivyo tutatumia *facilities* ya mkonga uliopo katika kuimarisha *database* ambayo itaunganishwa na *database* nyengine. Kwa hivyo kama nilivyosema juzi ni kwamba tunatarajia mwisho wa kikao hiki tutasoma sheria kwa mara ya kwanza ya Taasisi hii ya Usajili na hatimaye wajumbe mtapata nafasi ya kuja kuusajili ule mswaada mtaona ndani yake tunakusudia kufanya nini, kitu muhimu stahamala tutasoma kwa mara kwanza na baraza lijalo tutakuja na sheria mtaijadili hapa na hatimaye mtaipitisha ili Serikali tuweze kuifanyia kazi.

Lakini pia alizungumzia suala la ndoa za wageni kwa mfano watalii wanapokuja na watu wengine wanaoamua kuja kufungua ndoa hapa Zanzibar. Kwa mujibu wa sheria ya usajili wa matukukio ya kijamii ndoa inasajiliwa pale pahala ambao inafungwa kwa hivyo, sheria yetu inalitambua hilo na sheria itakayotungwa baadae italitambua hilo na tutaimarisha zaidi mfumo ili kuhakikisha hakuna ndoa itakayofungwa bila ya kusajiwa hapa Zanzibar hata kama waliofunga ni wageni na ni kweli nakubaliana naye kwmaba hizi zitaingiza fedha katika mfuko mkuu wa hazina.

Ushauri wake wa kupungunza mchanga nadhani tunaukubali alisema pia jambo hili katika mchango wake wakati wa bajeti na tuko mikakati ya kuweza kuufanyia kazi suala la maegesho limezungumzwa na wajumbe wengi akiwemo yeye Mhe. Raza na wengineo kwamba hili jambo kama nilivyosema katika utekelezaji wetu kama tunalitengenezea utaratibu na sasa hivi tuko katika hatua ya mbali sana, tumepeleka taratibu na mikataba na namna ya kuweza kulifanya kwa kushirikana na wahusika wengine wa binafsi ili tuweze kukusanya suala la mapato yanayotokana na maegesho kwa kutumia njia ya *electronic* jambo hili tumefika mbali na pale itakapokuwa tayari waheshimiwa tutakuja kulieleza.

Amezungumzia suala la kuongozwa na Katiba nakubali kwamba nchi yetu inaongozwa na Katiba vile vile dira yetu inaongozwa na *program* maalum ya utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapianduzi lakini hotuba ya Kiongozi wetu Mkuu hasa kuhusu Sekta ya Utalii. Nataka nimthibitishe kwamba katika ile sera ya utalii kwa wote sisi Ofisi ya Rais, Tawala la Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum tumepewa maeneo maalum ya kuitekeleza sera hii ya utalii kwa wote.

Kwanza kuhakisha nchi iko salama na wageni wanaokuja wanakuja salama na wanaondoka salama. Lakini la pili kuhakikisha kwamba miji yote ya Zanzibar inakuwa safi ili iwe ni kivutio cha watalii. Lakini vile vile, amezungumzia suala la matamasha ambayo yanafanyika hatuna tatizo na tamasha lolote lile na tunayaunga mkono isipokuwa Serikali inachotaka kuhakikisha kwamba matamasha yale yanafuata utamaduni na silka za wazanzibari ili yasije yakaleta mkanganyiko katika kuharibu utamaduni wa wanzanzibari. Kwa sababu utamaduni wa wazanzibari na silka za wazanzibari ni sehemu ya kuimarisha huo utalii kwa wote ndani ya nchi hii ya Zanzibar.

Matatizo ya barabara ya Kendwa nadhani ameleta kama ushauri na sisi kama ofisi tutakaa na wawekezaji tuone tunashirikiana nao vipi ili kuona tunashughulika na barabara hii kupitia halmashauri zetu wewe uwe balozi wa kuweza kuwambia wawekezaji kwamba wawe tayari kuzungumza na Viongozi wa Halmashauri na Mikoa kwa ajili ya kulifanikisha hili lakini sisi tunalipokea na hatua matatizo nalo.

Mhe. Abdalla Ali Kombo Mwakilishi wa Wananchi Mwanakwerekwe kila siku anakuja na mpya leo amekuja na paka mweusi anayetafuta kowa watu wa mjini wanaita konokono lakini ni kowa na mimi huwa nafatilia sana ile misamiati yake ili nijue maana yake halisi ni nini. Namshukuru sana Mhe. Abdalla amezungumzia sana suala la kwamba mji umekuwa mji na mimi nataka nikubaliane naye na *Inshaallah*, tutaendelea kushirikiana ili mji uwe mji na ameona juhudi zetu za kujenga barabara ile kutoka kwa Mabata hadi Kijitoupele. Nataka niwaarifu Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwamba Serikali imeamua ndani ya kipindi hiki na mkandarasi yule kama kuondoka tuhakikishe na ile barabara iliyomo ndani ya Ilani ya Uchaguzi nayo tunaijenga kwa hiyo kwa wale wanasema kwamba Wilaya ya Magharibi 'A' na 'B' hakuna barabara zote ziko mjini tumeanza kushughulika nazo.

Amezingumzia suala la ZSSF na vijana wetu wa Idara Maalum kama nilivyosema suala hili Serikali imelifanyia kazi na tumeunda timu ya wataalamu kati ya *Management* ya *ZSSF* na *Management* ya Idara Maalum za SMZ ili kuona jambo hili tunali-*fast track* ili liweze kutekelezeka na wao ni sehemu wa kufaidika na mfuko huu wa Hifadhi ya Jamii kwa hiyo Mheshimiwa namuomba asiwe na wasiwasi.

Nidhamu ya ujenzi ushauri tunaupokea na tunaendelea kuufanyia kazi na pale pahala ambalo amepasema Mwanakwerekwe watu waliojenga katika njia za maji kwa kweli kuna mradi wa ZUSP II ambao utatoa maji kutoka pale bonde la Mwanakwerekwe kuunganisha Sebleni na maeneo mengine ya Kwa Binti Amran tutahakikisha nyumba zote zilizopo katika maeneo ya njia za maji kama tulivyofanya katika maeneo ya Jang'ombe na kwengineko tunawalipa fidia kwa wale ambao wamepata vibali halali na tunazivunja ili kuondosha kadhia hii ya kutuama kwa maji na kuepukana lilie tatizo la kila mwaka kuwapa watu msaada kwa ajili ya mafuruko ambayo yanatokea.

Kwa hiyo nyumba zote zilizojengwa bila ya mpango tutaangalia tutafanya tathmini kama wapo ambao Serikali tumewapa *permit* sisi wenyewe basi tutaangalia kwa mujibu wa sheria ziliopo ili tuweze kuwafidia, lakini kwa wale ambao wamejenga kiholela Serikali itachukua eneo lake na kuweza kufanyia maendeleo ambayo Serikali inataka kuyafanya.

Vifaa chakavu ni kweli katika mji wetu ukitembea barabarani utakutia vifaa vingi chakavu ambavyo vinatoka nje lakini Serikali iliwahi kuleta sheria ya vitu hivi na sisi tunaangalia kwa umakini na tunaliwekea utaratibu wa kuweza ya kuzitumia kanuni tulizo nazo kuona kwamba vifaa vile chakavu havizagai ovyo barabarani kama mtu anafanya biashara ya vitu vile chakavu basi awe na sehemu maalum ambayo anaweza akahifadhi bila kuharibu mandhari ya mji kwa hivyo nakubaliana naye.

Tuna mpango gani wa usafiri wa Kijangwani na hili pia amelisema Mhe. Shamsi pahala kwanza ambapo pamewekwa kifusi ni pahala pa muda ambapo kituo kile kilichopo Michenzani mpaka CCM tobo la pili kinahamia pale kwamba gari zote zinazotoka nje ya mji zitafikia pale na pale patakawa na *route* nyengine ambayo inatoka Kijangwani kuja huku mjini kwa hivyo lile tatizo ulosema la kubeba pakacha au kipolo kwa mtu anotoka Pemba anotoka wapi halikuwepo, kwa sababu zitakuwepo gari ambazo zinafika mjini na kuweza kutoa huduma mpaka pale Kijangwani na pale Kijangwani zitakuwepo gari ambazo zinakwenda katika maeneo mengi.

Waheshimiwa wajumbe nyote mmetembea duniani, dunia nzima inakuwa na pahala maalum *stand* ambayo magari yanayotoka nje ya mji yanafika hapo na pale yanapofikia kunakuwa na *route* nyengine ya magari ambayo yanaingia ndani ya mji na sisi tutafanya hivyo na lini kituo kitakuwa tayari. Kituo cha *temporary* si muda mrefu kitakuwa tayari lakini kile kituo kikuu cha daladala kinategemea pale Mpango Mkuu wa *Master Plan* ya Mji utapokuwa ushakuwa tayari ndipo utapojenga sasa kituo cha kudumu, kile tunachofanya sasa ni cha muda tuu. Kwa hivyo niwatoe wasiwasi waheshimiwa wajumbe kwamba hakutokuwa na usumbufu wowote kuhusu suala hilo.

Kuhusu soko la Mwanakwerekwe ni kwamba ni lazima tuhakikishe mazingira ya soko lile yanakuwa vizuri na linaatumika kama lilivyokusidiwa na vurumai inaondoka na mimi nimefahamu tusiache mbachao kwa msala upitao. Najua kwamba sasa hivi tunajishughulisha zaidi na suala la kutoa huduma katika maeneo ya Fumba, lakini bila kusahau eneo na Mwanakwereke kwa wakati mmoja.

Kuhusu vijana wa KMKM vipi nataka niwathibitishie kwamba jambo hili tayari limemaliza na hivi karibuni ufumbuzi wao utapatikana na kwa sababu mnawasiliana nao watakupeni taarifa nzuri na siyo taarifa mbaya. Ahsanteni sana.

Mhe. Panya pongezi tunazipokea majengo ambayo hayana hati tumeeleza kwa urefu sana katika utekelezaji wetu na namna jinsi gani tunavyochukua hatua kwa hivyo muendelee kutuvumilia ili zile hatua zilizobakia tuweze kuzichukuwa.

Walimu wangapi wameajiriwa kwa hivi sasa sina *data* za walimu wangapi lakini yapo mafanikio ya kupunguza ule ukubwa wa ukosefu wa walimu ambao ulikuwa umetokea katika Wilaya zetu mbali mbali. Hatua za kuwapata wataalamu nazo nimezieleza kwa urefu sana kwa sababu ya muda naomba mridhike.

Mhe. Rashid Makame Shamsi mengine nimeyajibu lakini ametuasa kwamba vile vikundi

vya operesheni vinapofanya kazi yao viangalie waliokuwa ndio na waliokuwa sio. Mimi nisihi tu kwamba raia wema waondoke katika yale magenge ambayo tunayadhani kwamba ni magenge ya uhalifu. Unapojiingiza katika magenge yale wanapokuja watu wa operesheni hawachaguwi huyu Haji Omar, huyu Makame Shamsi na wewe watakuingiza kundini. Kwa hivyo, ni vizuri tutambue hivyo kwamba watu wa vyombo wanapofanya kazi zao wakishapewa *direction* kwamba pahala fulani pana magenge ya uhalifu, jaribu sana hapo pahala kupaepuka, vyenginevyo watakapokuja hawachaguwi sura, wanachukua tu baadae watakapofikishwa kwenye vyombo vya sheria ndio itajuuikana kwamba huyu ndiye au siye. Kwa hvyo, hili kama limefanyika kwa athari zile ambazo mheshimiwa umezisema ni bahati mbaya, nadhani sio malengo hasa ya serikali yetu katika kufanya hivi, lakini wito wangu ni huo.

Suala la kituo cha daladala umetwambia kwamba serikali tuwe na *format* moja ya uwasilishaji wa ripoti. Nadhani serikali tutakaa tuone na kubwa zaidi umeona kwamba wengine wameleta kwa njia ya bango kitita, wengine wameleta kwa njia ya utaratibu ule wa kawaida wa maandishi. Nadhani hilo ni wazo zuri ambalo serikali tutakaa tuweze kulifanyia kazi.

Umetoa pongezi kwa programu ya mimi na wewe, tunakushukuru. Wilaya gani kuhusu Mabaraza ya Vijana. Sisi kama tulivyosema kwamba tuko katika ugatuzi, sekta zote ambazo zina maafisa wake Wilayani tunapotoa programu tunaitoa kwa Wilaya zote. Sasa suala la nani amefanya na nani hajafanya hilo litategemea kile kitengo chetu cha ufatiaji na tathmini kuona yupi ametimiza hili jambo kwa asilimia ngapi. Na hili limeulizwa na wajumbe wengi lakini kimsingi programu hii inatakiwa itekelezwe kwa Wilaya zote za Unguja na Pemba.

Mhe. Mohammed Raza Daramsi namshukuru sana kwa mchango wake na sote kama alivyosema tumeweza kumuombea Mungu katika kadhia yake ile, mwanadamu Mwenyezi Mungu anakukumbuka na akikukumbuka basi vile vile ana uwezo wa kukuponyesha, na tunamshukuru Mwenyezi Mungu Mhe. Raza amekwenda salama na amerudi salama na leo tumeungana nae na Mwenyezi Mungu ataendelea kumpa afya njema ili tuweze kushirikiana nae. Amelizungumzia suala la kuzingatia maadili ya Wazanzibari na silka nadhani nimeshalitolea ufafanuzi sina haja tena ya kulizungumza kwa mara nyengine. Ametuomba serikali kupitia upya na kuangalia ujenzi wa aina wa hoteli za kitalii za makuti zinazojengwa ndani ya nchi yetu kama bado utaratibu huu unaendelea uendelee au laa. Jambo hili serikali kwa jumla tumeshaanza kulizingatia na leo umetukumbusha basi tutaendelea kulifanyia kazi ili tuweze kuweka hoteli ambazo zina hadhi ya kuja wageni wenye heshima.

Mhe. Naibu Spika, suala la maegesho nalo nimesema kwa hiyo nadhani majibu yangu ni yale yale.

Mhe. Bahati Khamis Kombo na yeye alizungumzia mkakati kuhusu Mabaraza ya Vijana nishatoa ufafanuzi sina haja ya kurejea. Mashirikiano kuhusu Mahakama na Mabaraza kesi 62 zimehukumiwa na zimepatiwa ufumbuzi, na sio 62 zimehukumiwa chache. Kwa hiyo, zile kesi tulizoziripoti katika Baraza la Mji la Mkoani zimepatiwa ufumbuzi baada ya mashirikiano kati yetu sisi na Mahakama Kuu ya Zanzibar. Kwa kuweka utaratibu

mzuri wa mfumo wa kufungua Mahakama za Mabaraza lakini vile vile kwa zile kesi ambazo zinakwenda kwenye Mahakama za Wilaya nazo kuweza kupatiwa ufumbuzi wa haraka.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kwisha kusema hayo yapo maoni mengine ambayo yametolewa kwa maandishi, Waheshimiwa Wajumbe wajue tu kwamba yale yote ambayo wameyaleta kwa maandishi yale ya ushauri tunayapokea na yale ya kuyafanyia kazi tutayafanyia kazi na sote tutaridhika baada ya sisi kukutana na kamati na kuyaripoti yale ambayo tutakuwa tumeyachukua hapa.

Baada ya kwisha kusema hayo Mhe. Naibu Spika, na Waheshimiwa Wajumbe niwashukuru na naomba kutoa hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri, Waheshimiwa Wajumbe naomba sasa tukubali kama tumeipokea taarifa ya Mhe. Waziri kwa hivyo tutanyoosha mikono waheshimiwa naomba tukubali kwamba tumeipokea, wanaokubali. Ahsanteni sana.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

HOJA ZA SERIKALI

Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji – Ripoti ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Ardhi na Mawasiliano kwa Mwaka 2016/2017

Mhe. Waziri Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha Taarifa ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Ardhi na Mawasiliano ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar kwa mwaka wa 2016/2017.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuchukua nafasi hii kukushukuru wewe kwa kunipatia fursa hii adhimu ya kuwasilisha utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya Ardhi na Mawasiliano ya Baraza lako tukufu kama ambavyo walitupatia wakati walipokuwa wanafanya kazi za kamati katika wizara yetu kwa lengo la kuimarisha utendaji na kuleta ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya wizara.

Mhe. Naibu Spika, napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi na Mawasiliano Mhe. Hamza Hassan Juma, Mwakilishi wa Jimbo la Shaurimoyo, Makamu Mwenyekiti wa Kamati, Mhe. Suleiman Sarahan Said, Mwakilishi wa Jimbo la Chake-Chake pamoja na wajumbe wote wa kamati hiyo kwa ushauri, maelekezo na mashirikiano waliyotupatia muda wote wakati wakitekeleza majukumu yao kwa lengo la kuimarisha kazi zetu za kila siku. Ni imani yangu kuwa ushauri na maelezo yao waliyotupatia yamesaidia sana katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya wizara yetu kwa ufanisi zaidi.

Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji inaendelea kusimamia utekelezaji wa majukumu yake kwa kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo (*Vision 2020).* Mkakati kwa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini MKUZA III, ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi mwaka 2015/2020, Sera ya Taifa ya Usafiri Zanzibar 2008, Sera ya TEHAMA, Sera ya Taifa ya Nyumba na Mpango Mkuu wa Usafiri Zanzibar (*Transport Master Plan* ya 2009) pamoja na sera nyenginezo zinazohusiana na shughuli hizo. Katika kutekeleza majukumu hayo kwa ufanisi wizara imeyagawa katika sekta kuu nne. Sekta ya Ujenzi, Sekta ya Makaazi, Sekta ya Mawasiliano na Sekta ya Usafirishaji.

Mhe. Naibu Spika, Kamati ya Ardhi na Mawasiliano chini ya Mwenyekiti wake Mhe. Hamza Hassan Juma ilipata fursa ya kupitia sekta zote nne kwa Unguja na Pemba kwa lengo la kukagua na kupokea taarifa ya utekelezaji wa bajeti kutoka katika taasisi mbali mbali za wizara yetu. Wakati Kamati ya Ardhi na Mawasiliano ya Baraza la Wawakilishi ikikagua kazi mbali mbali za wizara pamoja na kupokea taarifa za utekelezaji wa bajeti, Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji ilipokea maagizo mbali mbali, ushauri mbali mbali kutoka kwa kamati hiyo kwa lengo la kuimarisha utendaji na kuleta ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya wizara.

Mhe. Naibu Spika, baada ya wizara yetu kupokea maagizo mbali mbali kutoka kwa Kamati ya Ardhi na Mawasiliano kwa lengo la kuleta ufanisi katika kutekeleza majukumu ya wizara, hatua za utekelezaji wa maagizo hayo ni kama ifuatavyo:-

Maagizo

Agizo Nam.1. Kamati inaiushauri sekta hii kuhakikisha inasimamia kwa ukaribu zaidi miradi yote mikubwa ya wizara hii ili kuokoa fedha za wananchi.

Utekelezaji

Tayari wizara kupitia Idara ya Mipango, Sera na Utafiti imewatayarisha watendaji wake wote katika kuhakikisha kwamba miradi yote mikubwa na midogo iliyo ndani ya wizara pamoja na taasisi zake inasimamiwa kikamilifu kwa pamoja na wizara yetu.

Agizo Nam.2. Kamati inaitaka sekta hii kuhakikisha na kusimamia katika bajeti ya mwaka bodi zote zilizomo kwenye wizara hii zinazotegemea fedha kwa ajili ya kufanya shughuli zao kama sheria zinavyotaka.

Utekelezaji

Mhe. Naibu Spika, wizara katika bajeti ya mwaka huu wa fedha 2017/2018 imezipatia bajeti bodi tatu zimetengezewa bajeti zilizomo chini ya wizara hii ambazo awali hazikuwa na bajeti wala chanzo cha kupata mapato ya kuendesha shughuli zao. Bodi hizo ni bodi ya Usafiri Barabarani, Bodi ya Usimamizi na Utunzaji wa Nyumba na Bodi ya Kudhibiti Kodi za Nyumba. Bodi nyengine mbili Bodi ya Wakandarasi na Bodi ya Usajili wa Usanifu zitaendelea kujiendesha kutokana na mapato yao ya ndani.

Agizo Nam.3. Kamati inaiomba wizara kwa kushirikiana na Shirika la Nyumba kuanza kuzifanyia matengenezo nyumba ambazo zinaweza kutengenezeka na baadae kujiongezea mapato.

Utekelezaji
Shirika la Nyumba Zanzibar tayari limeandaa mpango mkubwa wa kuzifanyia matengenezo nyumba zake. Mpango huo umehusisha matengenezo ya muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu na unategemewa kuanza kutekelezwa ndani ya mwaka huu wa fedha 2017/2018.

Agizo Nam.4. Kamati inalitaka shirika kufanya uhakiki na kuzitambua nyumba zake zote na kuziorodhesha katika daftari la mali za shirika *Fixed Assert Register*. Kazi za kuzifanyia uhakiki kuzitambua na kuziorodhesha nyumba zake katika daftari la mali za serikali inaendelea, na zoezi hilo limegawika katika maeneo manne. Nayo ni nyumba za maendeleo, nyumba za Mji Mkongwe, nyumba kongwe katika maeneo mbali mbali na nyumba za vijijini.

Agizo Nam.5. Kamati inaliomba Shirika kutafuta hatimiliki za nyumba zake haraka iwezekanavyo, kuondokana na hali ya udanganyifu kwa baadhi ya wamiliki wa nyumba hizo. Kazi ya kuzitafuta hatimiliki nyumba za serikali inakwenda sambamba na zoezi la kuzitambua na kuziorodhesha miliki zake katika daftari la Shirika. Baada ya hapo nyumba hizo zitafanyiwa tathmini ili ziorodheshwe pamoja na thamani zake.

Agizo Nam.6. Vile vile katika agizo hili kamati inaishauri Shirika kutenga bajeti maalum kuongeza bajeti na kuwa bega kwa bega na mdhamini wa majengo Pemba ili kuhakikisha *Pilot Project* yake ya usafi inafanikiwa.

Utekelezaji

Mhe. Naibu Spika, Shirika la Nyumba liko bega kwa bega na mdhamini wa Shirika hilo Pemba, ambapo ya kuzifanyia usafi nyumba za Madungu zinaendelea na kuzifanyia matengenezo yote yanayohitajika kwa nyumba hizo.

Agizo Nam.7. Kamati inaiomba wizara ihakikishe inatunga Kanuni haraka ili kusaidia utekelezaji wa Sheria Nam.6 ya 2014. Hali ambayo hupelekea ugumu kwa upande wa Shirika katika kutekeleza majukumu yake.

Utekelezaji

Shirika linaendelea na utungaji kanuni na sheria husika.

Agizo Nam.8. Kamati inaitaka Bodi ya Nyumba ifanye kazi zake kama sheria inavyoagiza au mwenyekiti ajiuzulu kwa kushindwa kazi aliyopewa pamoja na wajumbe wake.

Utekelezaji

Bodi na *Management* ya Sherika imelipokea agizo hilo na imeahidi kuongeza kasi katika utekelezaji wa majukumu yake.

Agizo Nam.9. Kamati inalishauri Shirika la Nyumba kutafuta aidha wabia au taasisi za kifedha kushirikiana nazo ili kuweza kuwawezesha wananchi waweze kuwakopesha au kuwajengea nyumba kwa njia ya mkopo nafuu kama wanavyofanya wenzetu Tanzania Bara.

Utekelezaji

Shirika tayari limeanza mazungumzo na wawekezaji na taasisi mbali mbali za fedha ili kupata mikopo au kuwa na ubia katika miradi mikubwa ya ujenzi wa nyumba za Shirika letu la Nyumba.

Agizo Nam.10. Mamlaka ya Hifadhi na Uendeshaji wa Mji Mkongwe ishirikishwe kikamilifu wakati wa kuandaa na kutekeleza miradi ya ujenzi huo ili kuepusha hasara na usumbufu mkubwa wakati wa utekelezaji wa miradi hasa ya ujenzi wa ndani ya hifadhi hiyo. Kamati inazishauri taasisi mbali mbali kabla ya kuamua utekelezaji wa miradi ya ujenzi katika eneo la Hifadhi ya Mji Mkongwe lazima kwanza ipelekwe kwenye kamati ya wataalamu wa mamlaka ya Mji Mkongwe ili kutoa miongozo yenye kufaa.

Utekelezaji

Ushauri umepokelewa…

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Waziri wajumbe wanalalamika kidogo wanasema sauti yako iko chini sana, kwa hvyo tunakuomba uzidishe sauti kidogo.

Mhe. Waziri Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Samahani mheshimiwa, samahani sana Mhe. Naibu Spika, sisi wengine tumeumbwa warefu kidogo kwa hivyo nilikuwa nafanya utaratibu unaofaa.

Mhe. Naibu Spika, katika utekelezaji ushauri umepokelewa na *Management* ya Mamlaka ya Hifadhi na Uendeshaji wa Mji Mkongwe unaandaa mpango maalum wa kutoa taaluma kwa wamiliki wote wa nyumba na majengo mbali mbali yaliyo katika eneo la hifadhi ya Mji Mkongwe.

Agizo Nam.11. Kamati inaishauri Mamlaka ya Mji Mkongwe kwenda *UNESCO* kwa ajili ya kukwamua muongozo wa ukarabati wa jengo la Beit-el-Ajaib ili kuweza kujengwa na watalii waweze kuja kuangalia na kufanya tafiti zao.

Utekelezaji

UNESCO na *ICOMOS* wameandikiwa barua ya tarehe 14/08/2017 kuwaomba wataalamu wao waje Zanzibar kwa ajili ya kutoa ushauri na maoni yao kuhusu mradi wa *Darajani Corridor* na miradi mengine ikiwemo *House of wonders*, Beit-el-Ajaib. *UNESCO* ilijibu kuwa watakuja wataalamu hao mwisho wa mwezi uliopita 2017 na yatafanyika

mazungumzo na miradi yote ya Mji Mkongwe itazungumzwa kwenye mikutano hiyo. Napenda kuchukua fursa hii Mhe. Naibu Spika, kulitaarifu Baraza lako tukufu kwamba ujumbe huo wa *UNESCO* sasa hivi uko nchini na mazungumzo mbali mbali yanaendelea.

Agizo Nam. 12. Kamati inazitaka taasisi zote zinazomiliki majengo katika maeneo ya Mji Mkongwe kufuata ushauri wa kitaalamu kutoka Mamlaka hiyo pamoja na kuitekeleza miongozo hiyo hasa katika kukarabati majengo hayo ili kuepusha kupata hasara ya kuanguka kwa majengo hayo, jambo ambalo taifa hupoteza rasilimali watu pamoja na mali zao.

Utekelezaji

Ushauri wa Kamati umepokelewa na unafanyiwa kazi sambamba na kutoa elimu kwa wamiliki wote wa nyumba na majengo mbali mbali ya eneo hilo juu ya sheria, kanuni na taratibu juu ya hifadhi ya Mji Mkongwe.

Agizo Nam.13. Kamati haikuridhishwa hata kidogo na mazingira ya jengo la Ofisi ya Idara hiyo na kuitaka wizara kulipatia ufumbuzi wa haraka iwezekanavyo suala hilo.

Utekelezaji

Idara ya Usafiri wa Leseni baada ya kuliona tatizo hilo imewasiliana na wakala wa majengo ya serikali kufanya uchambuzi yakinifu na kutoa michoro itakayoongoza marekebisho ya jengo hilo kama ilivyochukuliwa hatua za kuzirekebisha sehemu nyengine za majengo hayo katika mwaka uliomalizika mwaka wa fedha 2016/2017.

Agizo Nam.14. Kamati inashauri idara ifanye mpango wa kuanzisha skuli ya udereva wa viongozi wa serikali.

Utekelezaji

Kwa mujibu wa kifungu Nam. 8 cha Sheria Nam. 7 ya mwaka 2003 (*Road Transport Act)*, idara inatakiwa kusimamia unazishwaji wa skuli ya udereva kuwasajili walimu wa skuli na walimu wa udereva na kuandaa mitaala ya mafunzo hayo na sio kuanzishwa skuli za udereva.

Agizo Nam. 15. Kamati inaomba idara ifanye ukaguzi wa mara kwa mara kwa vyombo vyote vya moto vya barabarani pamoja na madereva ili kuisaidia serikali katika kupunguza idadi ya ajali za barabarani.

Utekelezaji

Ushauri umechukuliwa na utafanyiwa kazi.

Agizo Nam. 16. Kamati inaomba wizara kupitia idara kufikiria kuanzishwa utaratibu wa ulipaji wa faini za papo kwa papo kwa kulitumia Jeshi la Polisi kama wakala wa kutekeleza suala hilo kama inavyofanyika huko Tanzania Bara.

Utekelezaji

Kanuni tayari imeshaandaliwa na hivi karibuni utaratibu huo utaanza. Wizara hivi sasa inaandaa waraka ambao utawasilishwa serikalini mwezi wa Oktoba wa kuomba utekelezaji wa kanuni hizo kwa jamii.

Agizo Nam. 17. Kamati inaitaka serikali pamoja na wizara husika kupitia idara kuangalia uwezekano wa kukataza usafiri wa bodaboda ama kutoa leseni na kuwatambua madereva wa bodaboda hizo, ili kuepusha mlolongo wa malalamiko kuhusiana na usafisi hasa wa usafiri huo wakati wa usiku.

Utekelezaji

Suala hilo limefanyiwa kazi kwa kuitisha kikao cha wadau kuangalia vipengele vya sheria ili kupata maoni ya pamoja baina ya pande zote husika.

Agizo Nam. 18. Kwa kuwa harakati na mahitaji ya ujenzi na utunzaji wa barabara yanaongezeka kwa kasi mjini na vijijini, ni vyema wizara ikaagiza zana nyengine mpya za kisasa ili kwenda sambamba na mahitaji ya wakati huu.

Utekelezaji

Agizo limepokelewa na kwa mwaka huu wa fedha wizara imetenga Shilingi Bilioni Tano ili kuanza ununuzi wa baadhi ya vifaa kama vile gari la kutandaza lami (*Paver*) na gari la lami ya maji (*bitumen sprayer*) na mtambo wa kupkia lami (*Asphalt Plant*) pamoja na ununuzi wa lami (*bitumen*) tani 1,700.

Agizo Nam.19. Kamati inaiomba serikali iongeze bajeti ya idara hii kutokana na majukumu yake inayopangiwa ili yaweze kutekelezeka.

Utekelezaji

Agizo limepokelewa na kwa mwaka huu wa fedha serikali imetenga Shilingi Bilioni Tano kwa ununuzi wa vifaa mbali mbali kama tulivyosema na Hazina, pamoja na Shilingi Bilioni Tisa zimetengwa na Hazina kutoka Mfuko wa Barabara za kufanyia kazi za matengenezo barabara mbali mbali kwa Unguja na Pemba.

Agizo Nam. 20. Kamati imeitaka Bodi ya Mfuko wa Barabara kuacha urasimu usio na msingi wakati wa ujenzi wa barabara, kwani husababisha ucheleweshwaji wa ukamilishaji wa ujenzi wa barabara na kusababisha kazi nyengine kukwama au kutojengwa kwa wakati.

Utekelezaji

Agizo limepokelewa na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji itawasilisha kwenye vikao vya Mfuko wa Barabara kwa kuwa wizara hii ni mjumbe wa Mfuko huo ambao kiutawala uko chini ya Wizara ya Fedha na Mipango.

Agizo Nam. 21. Kamati inaitaka idara hii kuwasiliana na Afisi ya Rais Ikulu ili kufuatilia ahadi zote za Mhe. Rais majimboni na kuzitekeleza, kwa lengo la kuondoa malalamiko ya *passport plant* pamoja na ununuzi wa lami.

Mhe. Naibu Spika, hapo nataka nirejee kidogo. Afisi tumetakiwa kuwasiliana na ofisi ya Mhe. Rais Ikulu, ili kufuatilia ahadi zote za Mhe. Rais pamoja na kuzitekeleza kwa lengo la kuondoa malalamiko ya muda mrefu kuhusu utekelezaji wa ahadi hizo, ingawa kwa upande wa Pemba ahadi hizo hutekelezwa kwa haraka sana tofauti na hapa Unguja.

Utekelezaji

Agizo linafanyiwa kazi pamoja na kujumlisha maagizo aliyotoa Mhe. Rais katika ziara aliyoifanya hivi karibuni Agosti mwaka 2017 katika wilaya zote 12 za Zanzibar ili kuandaa mpango kazi wa utekelezaji wa maagizo haya.

Agizo Nam. 22. Kamati inaiomba wizara ifanye mpango wa kuwaingiza katika Mfuko wa Bima ya Afya wafanyakazi wake, kwa vile wamekuwa wakifanya kazi katika mazingira magumu na hatarishi kwa afya zao.

Utekelezaji

Mfuko wa Bima ya Afya haujaanzishwa rasmi hapa Zanzibar na Wizara ya Afya inaendelea na maandalizi ya kuanzishwa kwake. Hata hivyo, baadhi ya wafanyakazi kwa hiari zao wamejiunga na Mfuko wa Bima ya Afya ya Tanzania. Wizara inaendelea kulifuatilia kwa ukaribu sana suala hilo.

Agizo Nam. 23. Kamati inaishauri idara izidi kutoa taaluma kwa wananchi juu ya matumizi bora ya barabara pamoja na kuheshimu alama zilizomo barabarani ili ziendelee kudumu kwa muda mrefu zaidi.

Utekelezaji

Agizo hili ni endelevu na linaendelea kufanyiwa kazi. Katika mwaka huu wa fedha bajeti maalum imetengwa ili kuiendeleza kazi hiyo ya kutoka taaluma kupitia vyombo vya habari na vipeperushi pamoja na makongamano mbali mbali.

Agizo Nam. 24. Kamati inaitaka idara iwasilishe au iwasiliane na Manispaa na Halmashauri husika ili kuhakikisha kwamba suala la usafiri wa barabarani linasimamiwa ipasavyo.

Utekelezaji

Lengo la wizara ni kulihamisha suala hili kupelekwa Wiara ya Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ ili kupitia Halmashauri zao kulisimamia suala hili kwa Halmashauri zote za Unguja na Pemba ikiwa ni sehemu ya mpango wa ugatuzi. Hatua za utekelezaji bado zinaendelea.

Agizo Nam. 25. Kamati inaitaka serikali kupitia Idara ya *UUB* kuwalipa fidia wananchi walioko pembezoni mwa barabara kwa Wete-Chake Chake ili waanze kuhamisha majengo yao pamoja na vipando vyao, kwani fedha hizo tayari tumezitenga kwenye bajeti hii tuliyonayo ili wakati wa ujenzi utakapoanza isije kuleta usumbufu kwa wananchi.

Utekelezaji

Wizara imeanza kufanya tathmini upya ndani ya robo ya pili ya mwaka 2017/2018 yaani Oktoba - Disemba kwa barabara hiyo kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango, Uhakiki Mali na mkandarasi (*MECCO*) na Idara ya Mawasiliano kwa kuainisha maeneo yaliyopo ili tujue mkonga uko maeneo gani na wengineo kwa ajili ya kutekeleza agizo hili ndani ya mwaka huu wa fedha 2017/2018.

Agizo Nam. 26. Kamati inaitaka serikali kupitia idara hii kufanya kila jitihada kuepuka kuukata mkonga wa mawasiliano wa taifa ili kuepuka hasara kwa serikali.

Utekelezaji

Agizo limepokelewa na linafanyiwa kazi, changamoto kubwa itayojitokeza katika ujenzi wa barabara ya Bububu - Mkokotoni sehemu inayoanzia Mfenesini hadi Mahonda na kwa Pemba barabara ya Wete kuelekea Chake Chake kwa sehemu inayoanzia Wete (Limbani) hadi Mzambarauni. Wizara inaangalia uwezekano wa kuzidisha upande mmoja barabara hiyo ili kuunusuru mkonga wa mawasiliano usipate athari wakati wa ujenzi.

Agizo Nam. 27. Kamati inaiomba serikali pamoja na wizara kupitia shirika ifanye juhudi ya kuyapima na kuyafuatilia hatimiliki maeneo yote ya bandarini na minara ya kuongozea vyombo vya usafiri wa majini.

Utekelezaji

Baada ya kupatikana kwa hati za maeneo ya Mkokotoni, Kigomasha na Mpigaduri, Shirika la Bandari kupitia wizara linaendelea kuyafuatilia maeneo mengine ikiwa ni pamoja na maeneo yote yanayosimamiwa na taasisi za wizara hii baada ya kuwaandikia barua Wizara ya Ardhi, kumbukumbu Nam. MOICT/M120/C.1/VOL ya tarehe 10 Januari, 2017 na barua nyengine ya tarehe 7 Agosti, 2017 ya kumbukumbu Nam. MOICT/M.70/1/VOL.1/78.

Agizo Nam. 28. Kamati inalitaka Shirika la Bandari kushirikiana na *TRA* kutafuta mashine ya *X-Ray* kuweza kukagua mizigo kwa uhakika hapo bandarini.

Utekelezaji

Baada ya kununua mashine mbili za *X-Ray* ambazo hivi sasa zimeanza kutumika katika mwaka huu wa fedha, shirika linategemea kununua mashine nyengine mbili kwa ajili ya bandari ya Mkoani na Ukumbi wa *VIP* wa Bandari ya Malindi kwa hapa Unguja.

Agizo Nam. 29. Kamati pia inaipongeza wizara kwa kupitia Shirika la Bandari, lakini ni vyema mafunzo ya ziada wakapatiwa wanaotumia vyombo hivi ili kuweza kuishi na vitumike kwa muda mrefu. Tunashukuru kwa pongezi hizo na tunatekeleza hilo agizo kwa kuhakikisha kwamba agizo limepokelewa na linafanyiwa kazi na Shirika la Bandari kwa kubadilishana uzoefu na wafanyakazi wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege ili kupata uzoefu zaidi.

Agizo Nam. 30. Kuhusu suala la ujenzi wa bandari ya Wete, Pemba kamati inaipongeza serikali kwa wazo la kushirikiana na mwekezaji binafsi kuijenga bandari hiyo, lakini inataka serikali kuhakikisha yeyote atakaetaka kuwekeza kwenye ujenzi huo ni lazima adhibiti na matumizi ya bandari yasimamiwe na Shirika la Bandari.

Utekelezaji

Agizo limepokelewa na kuhusu ujenzi wa gati nyengine Wete unaendelea. Katika mwezi wa Julai, 2017 Shirika la Bandari limekutana na uongozi wa *Azam Marine* hapa Zanzibar *and Zanzibar Fast Ferries* kwa kukubaliana mambo ya msingi juu ya namna ya kuendeleza uwekezaji huo. Ni mategemeo ya wizara kwamba kazi hiyo inaweza kuanza mwanzoni mwa mwaka wa 2018.

Agizo Nam. 31. Kamati inaiomba serikali pamoja na wizara kuangalia uwezekano wa kutafuta meli nyengine ya abiria na mizigo, ambayo itaendana na mahitaji ya hivi sasa ya kubeba mizigo na abiria ili kukabiliana vyema na soko katika sekta ya usafiri wa majini.

Utekelezaji

Agizo limepokelewa na majadiliano bado yanaendelea na kwa mwaka huu wa fedha serikali itaanza kwa kujenga meli moja ya mafuta kwa kuchukua nafasi ya Mt. Ukombozi ambayo inatumika hivi sasa.

Agizo Nam. 32. Kamati pia inaomba serikali kwa kushirikiana na wizara pamoja na shirika iangalie uwezekano wa kutafuta meli nyengine ya mafuta.

Utekelezaji

Serikali imeanza matayarisho ya ununuzi wa meli hiyo ambapo kwa mwaka huu wa fedha wizara imetenga shilingi 18 bilioni kwenye bajeti kwa ajili ya hatua za awali za ununuzi wa meli hiyo na majadiliano bado yanaendelea.

Agizo Nam.33. Kamati inaendelea kulishauri shirika liangalie uwezekano wa kuanzishwa safari zaidi katika Bandari za Tanga, Mtwara na Comoro kwa usafirishaji wa abiria na mizigo ikiwemo saruji.

Utekelezaji

Wizara kupitia Shirika la Meli imepokea na kuanza kufanyia kazi agizo hilo. Aidha, kwa hivi sasa shirika pamoja na kutoa huduma za usafiri baina ya visiwa vya Unguja na Pemba imeanzishwa safari za kwenda Comoro ambapo ndani ya mwaka wa fedha uliokwisha tayari safari mbili zimefanyika. Aidha, kwa upande wa Mombasa tayari shirika limeshafanya safari moja.

Agizo Nam. 34. Kamati imepokea maamuzi ya serikali kuiuza Meli ya MV. Maendeleo na kununua meli nyengine, lakini kamati inatoa angalizo mapema kuwa meli itakayonunuliwa izingatie mahitaji ya abiria na wafanyabiashara.

Utekelezaji

Angalizo limepokelewa na mahitaji ya abiria na wafanyabiashara yamezingatiwa na kamati ya serikali inayosimamia ujenzi wa meli mpya za serikali kutokana na uzoefu uliopatikana katika changamoto za uendeshaji wa Meli ya MV. Mapinduzi II. Utafiti huo wa muundo wa meli mpya ya abiria na mizigo bado unaendelea kufanywa pamoja na kujaribu kuepuka au kuziondosha kabisa changamoto zilizoikabili MV. Mapinduzi II kwa hivi sasa.

Agizo Nam. 35. Kamati inaomba mamlaka ihakikishe kwamba inatoa ushauri wa kutosha kwa mamlaka zinazohusika ili mikataba ya kimataifa ya usajili wa meli iweze kuridhiwa Bungeni.

Utekelezaji

Kufuatia ziara ya Kamati ya Baraza la Wawakilishi katika Taasisi za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeamuliwa kuundwa kwa kamati ya watendaji washughulikie suala hilo. Kamati hiyo inasubiri majina ya wajumbe wake kutoka Serikali ya Muungano wa Tanzania ili kazi hiyo ianze mara moja.

Agizo Nam. 36. Kamati inaiomba Mamlaka ya Usafiri Baharini ihakikishe kwamba inalisimamia kikamilifu suala la ulanguzi wa tiketi pamoja na tiketi za mikonni, kwani linachangia kwa kiasi kikubwa vyombo vya usafiri kupakia abiria kuliko uwezo walionao.

Utekelezaji

Wizara kupitia Mamlaka ya Usafiri Baharini imeshafanyia kazi suala hilo ikiwemo kuwasajli na kuwapatia leseni kwa kampuni zote zinazouza tiketi na kuhakikisha zinatumia *electronic ticket* na kutoa elimu kupitia vyombo vya habari kwenye televisheni na redio kuhusiana na masuala ya tiketi za magendo.

Agizo Nam. 37. Kamati inaiagiza Mamlaka ya Usafiri Baharini kusimamisha haraka iwezekanavyo kampuni ya *Philtex* kutoa huduma za usajili wa meli kinyume na utaratibu na sheria za nchi. Hali ambayo imeipelekea kuikosesha mapato serikali.

Utekelezaji

Wizara imepeleka suala hili kwa Mhe. Mwanasheria Mkuu wa serikali yetu kwa kulifanyia kazi zaidi kisheria suala hilo.

Agizo Nam. 38. Kamati inaiomba serikali pamoja na wizara kuishirikisha kikamilifu mamlaka ya Viwanja vya Ndege katika hatua zote za uendelezaji wa jengo la *Terminal II*.

Utekelezaji

Wizara imeshaunda kamati ya watendaji ambayo imewashirikisha wajumbe kutoka Idara ya Mipango ikiwemo Mkurugenzi wa Idara na Mratibu wa Mradi na wajumbe watatu kutoka Mamlaka ya Viwanja vya Ndege, wakiwemo Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege, Mkurugenzi Mipango na Mkurugenzi Ufundi wa Mamlaka hiyo. Tayari kamati ya watendaji imeshaanza kazi za ufuatiliaji wa uendelezaji wa jengo la *Terminal II*.

Agizo Nam. 39. Kamati inaiomba serikali pamoja na Wizara ya Fedha na Mipango kwa ujumla kuharakisha uwekaji wa *transformer* katika kiwanja cha ndege Pemba ili huduma zitakazotolewa ziwe za uhakika na endelevu.

Utekelezaji

Uwekaji wa *transformer* imeshawekwa na Shirika la Umeme katika Kiwanja cha Ndege cha Pemba chini ya Wizara ya Ardhi tokea tarehe 1 Aprili, 2017.

Agizo Nam. 40. Kamati inaishauri serikali na wizara kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege kuharakisha unununzi wa kifaa cha kuongozea ndege kinaitwa *ILS (Instrument Landing System)* katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume IA, hali ambayo haitaongeza pato la taifa kupitia sekta hii ya usafiri wa anga.

Utekelezaji

TCAA ya Tanzania upande wa Muungano tayari imepanga kwenye bajeti yao ya mwaka huu 2017/18 kuweka mtambo huo wa *Instrumental and System* kwenye Uwanja wa Ndege wa Abeid Aman Karume wa *International Airport* na timu ya mwanzo ya ufundi kutoka *TCAA* imeshatembelea uwanja huo na kuonana na mamlaka ya *Zanzibar Airport Authority* kwa utambuzi.

Agizo 41. Kamati inaiomba wizara kwa kushirikiana na Mamlaka kuendelea na ukarabati wa jengo la sehemu ya kushukuia na kuondokea abiria wakati wa safari zao ili kupunguza hali ya msongamano ambayo hupelekea upotevu wa mizigo kwa baadhi ya siku hususan ukizingatia siku ya Jumatano.

Utekelezaji:

Waraka wa uboreshaji wa jengo umeshawasilishwa Serikalini kwenye Baraza la Mapinduzi na imeundwa kamati maalum ya Baraza la Mapinduzi inayoongozwa na Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar wakiwemo watendaji wakuu wa serikali pamoja na uongozi wa ZAA.

Aidha serikali kupitia Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji itatenga fedha maalum za kununua vifaa vya kuimarisha utoaji wa huduma kwenye jengo hilo.

Agizo 42. Kamati inaiomba serikali na wizara kuweza kutafuta njia mbadala ya kuwapatia mamlaka ya Viwanja vya Ndege Kikosi cha Zima moto cha kudumu.

Utekelezaji

Wizara inaanda waraka huu na hoja hiyo kwa kuiwasisha serikalini kwenye Baraza la Mapinduzi kwa suala la kutizama uwezekano wa kuwa na kikosi cha Zima moto. Vikosi hivyo, vya viwanja vya ndege viendeshwe na Mamlaka husika.

Agizo 43. Kamati inaiomba serikali kwa kushirikiana na wizara kuendelea kuimairisha miundo mbinu ya mawasiliano ili kuweza kuwa na uwezo mkubwa na hivyo kuweza kubeba habari picha na hata *data* ili kufikia maendeleo undelevu ya dunia.

Utekelezaji

Utekelezaji wa agizo hilo umeanza kwa kuanzisha mfumo wa *E-Health* pamoja na kuanza maandalizi wa *E-Education, E-Taxation* na *E-Tourism*, na kwa upande mwengine serikali inaendela na mpango wa kuimarisha huduma za matumizi wa Mkonga wa Taifa ili kukidhi mahitaji haya.

Agizo 44. Kamati inaiomba serikali kwa kushirikiana na wizara kwa ujumla washirikiane wadau wote kabla ya kuanza kutekeleza miradi inayojipangia husasan katika masuala mazima ya mawasiliano.

Utekelezaji

Agizo lilipokelea na vikao vya Wadau mbali mbali inaandaliwa kwa madhumuni haya.

Agizo 45. Kamati inaomba makampuni kuunganisha haraka iwezekanavyo wajiunganishe kwenye mkonga wa taifa ili kupata njia mbadala ambayo itabeba mzigo mkubwa wa mawasiliano.

Utekelezaji

Agizo limepokelewa na limeshaanza kufanyiwa kazi kwa kuanza kuimarisha usimamizi wa matumizi ya mkonga chini ya Taasisi za Serikali ili kutoa fursa kubwa kwa kampuni nyengine kujiunga na mkonga huo katika matumizi yao.

Agizo 46. Kamati inaomba makampuni ya simu za mkononi kufikiria kuweka huduma ya free *WI-FI* katika maeneo ya wazi kama vile Hospitali Kuu ya Mnazi Mmoja, Forodhani, Michenzani na maeneo mengine yanayofanana na hayo ili kuzidi kuwasaidia wananchi kufaidika na huduma ya *WI-FI.*

Utekelezaji

Agizo limepokelewa na linafanyiwa kazi utekelezaji wake utaanza baada ya kukamilika mfumo mpya wa usimamizi wa matumizi ya Mkonga pamoja na kuyashirikisha makampuni mengine katika utowaji wa huduma hizi.

Agizo 47. Kamati inaiomba serikali ifanye juhudi za kuhakikisha kwamba inaweka utaratibu wa kutatua kero ya kutotambulika kwa vibali vya Taasisi za Zanzibar kwa wakuu wa taasisi hizo ambazo si za Muungano kuweka utaratibu unaoeleweka ili wananchi waweze kupata huduma za kiposta bila ya usumbufu wowote.

Utekelezaji

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeanza majadiliano na watendaji wa sekta husika kutoka Serikali ya Muungano ya Tanzania kupitia vikao vyao vya kutatua kero za

Muungano. Tayari vikao vitatu vya watendaji kwa pande zote mbili zimeshafanyika na kupeana kazi za ufuatiliaji.

Agizo 48. Kamati inaishauri serikali kwa kushirikiana na makampuni kutoa elimu kwa watumiaji wa huduma hizi pamoja na Taasisi za Serikali ni ya umuhimu kwa kuzitumia huduma hizo ipasavyo.

Utekelezaji

Agizo limepokelewa na wizara na imewasiliana na TCRA ili Kamati kusaidia katika utoaji wa huduma hizo.

Mwisho:

Mhe. Naibu Spika, kwa kumalizia nachukua fursa hii tena kukushukuru wewe kwa kunipatia fursa hii. Aidha nawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Ardhi na Mawasiliano pamoja na Wajumbe wote wa Baraza lako tukufu kwa kunivumilia kwa kunisikiliza kwa umakini wakati nikiwasilisha taarifa hii. Naomba Wajumbe wote waipokee taarifa hii.*(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha na naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sasa tunaendelea sasa tumpishe Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi na Mawasiliano.

Mhe. Suleiman Sarahan Said (Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi na Mawasiliano): Nashukuru sana Mhe. Naibu Spika, Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Mawasiliano kuhusu Ripoti ya Utekelezaji maagizo ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kwa Mwaka 2016/2017.

Mhe. Naibu Spika, Awali ya yote, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Subhanahu wataala, Aliejaa utukufu, ambaye ametujaalia uzima na afya njema na kutuwezesha kukutana hapa siku ya leo tukiwa ndani ya Baraza lako tukufu, tukitekeleza majukumu yetu mbali mbali na kutumikia wananchi wetu ambapo leo tunawasilisha mbele yako Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati kwa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kwa mwaka 2016/2017.

Mhe. Naibu Spika, Sitatenda haki ikiwa sijamshukuru na kumpongeza Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji, pamoja na watendaji wote wa Wizara hii kwa mashirikiano yao ya dhati kwa Kamati wakati wote tulipokuwa tukipitia na kujadili maagizo hayo.

Mhe. Naibu Spika, Baada ya maelezo hayo sasa naomba niwasilishe kwako Ripoti ya Utekelezaji wa maagizo ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji ambapo jumla ya maagizo 48 yaliwasishwa kama ifuatavyo:

Mhe. Naibu Spika, Katika moja ya agizo lililotolewa na Kamati kwa Wizara ya Ujenzi, Agizo nambari 2, Mawasiliano na Usafirishaji kwamba ifikapo mwaka wa fedha 2017/2018 Bodi ya *Condominium* iwe tayari imeshatengewa fungu kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yao.

Mhe. Naibu Spika, cha kusikitisha Bodi hii ilianzishwa kwa mujibu wa Sheria ya *Condominium Act No. 10, 2010,* Bodi ambayo hadi sasa nawasilisha hotuba hii ya utekelezaji wa maagizo haijawahi kufanya kazi hata siku moja.

Mhe. Naibu Spika, Kamati inashukuru kwamba kwenye bajeti hii kuwa wametengewa fungu maalum katika bajeti ya wizara lakini bado hadi leo bodi hii haijaanza kazi zake, kutokana na mustakabali huo kamati yangu inaitaka bodi hii ifanye kazi zake mara moja kwani kuchelewa kufanya kazi kunaikosesha Serikali mapato ambayo yangelipatikana kupitia ada za majengo mbalimbali ya Serikali.

Mhe. Naibu Spika, Pamoja na hayo, kuna baadhi ya nyumba za ghorofa ambazo wapangaji wake wanamiliki sehemu tu ya majengo hayo jambo ambalo linaleta

usumbufu wa kuzifanyia matengenezo nyumba moja moja na baadhi ya wakubwa kukataa kulipa kodi ya matengenezo za nyumba hizo.

Mhe. Naibu Spika, Agizo nambari 7, Utekelezaji wa agizo hilo haujakamilika kwa kuwa Shirirka bado linaendelea na Utungaji wa Kanuni ambayo itasaidia kurahisisha utekelezaji wa kazi za Shirika. Kutokana na kutotekelezwa ipasavyo agizo hilo Kamati bado inaiomba Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Nyumba kuharakisha kukamilika kwa Kanuni hiyo ili kuipa nguvu Sheria husika kuweza kutekelezeka kama ilivyokusudiwa. Kushindwa kufanya hivyo ni kuikosesha mapato Serikali yatokanayo na Kodi za Nyumba za Serikali pamoja na za wawekezaji binafsi katika sekta hii.

Mhe. Naibu Spika, Agizo nambari 11, Utekelezaji pia wa agizo hilo haujakamilika kwakuwa wataalamu kutoka UNESCO wanatarajiwa kuja tarehe 30/9/2017 hadi tarehe 3/10/2017 ambapo mazungumzo ya miradi yote ya Mji Mkongwe yatafanyika. Aidha, Kamati inaendelea kusisitiza kuharakishwa kutekelezwa kwa mradi wa Beit –el Ajaib.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa, waheshimiwa punguzeni minongono sauti zimekuja juu sana.

Mhe. Suleiman Sarahan Said (Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi na Mawasiliano): Mhe. Naibu Spika, Agizo nambari 13, Utekelezaji wa Agizo hili pia haujakamilika kwakuwa kilichofanyika ni kurekebisho madogo madogo tu ya Idara kwavile hakukuwa na fedha zilizotengwa kwa kazi hiyo wakati kamati ilipotoa maelekezo. Aidha, kamati inashauri wizara kukaa pamoja na Idara ya Leseni kuandaa tena mpango wa muda mrefu wa kulikarabati jengo la idara ya usafiri na Leseni ili lisiendelee kuharibika hasa nyakati za mvua.

Mhe. Naibu Spika, Agizo nambari 14, Agizo hili halijakamilika utekelezaji wake kwa kuwa hadi sasa idara haina mitaala na pia imeshindwa kuandaa mitaala ya mafunzo ya udereva. Aidha, Kamati imeshauri kutoa mtaalam maalum kwa Madereva wote wanaoendesha viongozi wa Serikali katika vyuo vyetu vilivyopo Zanzibar na sio kwenda Tanzania bara.

Mhe. Naibu Spika, Agizo nambari 15, Agizo hili nalo halijafanyiwa kazi kwa kuwa hadi sasa idara imeshindwa kufanya ukaguzi wa mara kwa mara kwa vyombo vya moto vya barabarani pamoja na madereva.

Mhe. Naibu Spika, Agizo nambari 16, Agizo hili halikamilika utekelezaji wake kwa kuwa kanuni bado ipo katika hatua za kusubiri kuwasilishwa Serikalini. Kutokana na jibu hilo Kamati inaishauri Wizara kwa kushirikiana na Idara ya Usafiri wa Leseni kuharakisha utekelezaji wa Kanuni hiyo ili kuweza kurahisisha kazi za Idara hiyo.

Mhe. Naibu Spika, Agizo nambari 17, kwa kuwa usafiri wa bodaboda umeanza kushamiri hapa Zanzibar, Kamati inaitaka Idara kuweza kutoa leseni maalum za kusafirisha abiria ili kuweza kuwadhibiti kwa kulinda usalama wa abiria na kuepusha ajali kwani hivi sasa wanapakia abiria bila ya kuwa na leseni ya kuwapakilia abiria jambo ambalo iwapo itatokezea ajali hakuna sheria au kanuni ilioruhusu kubeba abiria. Lakini pia zikitokea leseni za bodaboda itakuwa ni rahisi kuweza kumtambua mmiliki wa chombo iwapo kitatumika kwa vitendo viovu ikiwemo uhalifu au magendo.

Mhe. Naibu Spika, Agizo nambari 25, Kamati imefanya jitihada za kwenda Tanzania Bara kuonana na Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango ya Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania ili kujua nini tatizo la kukwamishwa upatikanaji wa fedha za kumalizia barabara hii. Wakati nusu ya pesa zipo tayari kutoka “BADEA” tatizo ni nusu ya pesa zilizobakia kutoka SAUDI FUND, wakati pesa zipo za Serikali ya Saudia lakini

hadi leo haijatoka ruhusa ya kupatikana kutoka kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango wa Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mhe. Naibu Spika, Agizo nambari 27, Utekelezaji wa Agizo hili bado unasuwa suwa hali ambayo inapelekea Kamati kutofurahishwa hata kidogo kuona kwamba hadi leo Bandari zote pamoja na Minara ya kuongozea Meli kwa upande wa Unguja na Pemba kukosa Hati Miliki za maeneo hayo.

Mhe. Naibu Spika, Chakushangaza maeneo ambayo yamekosa hatimiliki ni maeneo yanayoingiza pato la Nchi yetu. Je? Hatuoni kuwa tunaikosesha Serikali kuingiza mapato kiukamilifu kupitia vianzio hivyo.

Mhe. Naibu Spika, Kutokana na hili Kamati inaitaka Wizara ya Ujenzi, Mawasilisano na Usafirishaji kukaa pamoja na Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira kuweza kulitafutia ufumbuzi suala hili kabla ya kumaliza bajeti ya 2017/2018.

Mhe. Naibu Spika, Agizo nambari 38, Pamoja na Kamati kufika Tanzania Bara kwa nia ya kukutana na Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango kupata Usahihi wa tatizo hili, kwa sababu anazozijua yeye mwenyewe Katibu huyo alishindwa kutenga muda wa kukutana na Kamati.

Mhe. Naibu Spika, Kusema kweli kamati haikufurahishwa na kadhia hii kwa kuwa ni miaka tisa sasa ukamilishaji wa jengo la *Terminal II* haujaleta sura hali ambayo inapelekea kurudisha nyuma maendeleo ya Nchi ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, Naomba tena napenda kuwashukuru na kuwapongeza tena viongozi na watendaji wa Wizara hii kwa juhudi wanazochukua katika kutekeleza kazi zao pamoja na ushirikiano wao kwa Kamati hii. Aidha, nawashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa kunisikiliza kwa makini na utulivu wa hali ya juu wakati wote nilipokuwa nikiwasilisha.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa naheshimu michango na mapendekezo pamoja na ushirikiano kikamilifu naomba niwataje kwa majina Waheshimiwa Wajumbe na makatibu wa Kamati hii ya Ardhi na Mawasiliano ya Baraza la Wawakilishi kama ifuatavyo:-

Mhe. Hamza Hassan Juma	Mwenyekiti
Mhe. Suleiman Sarahan Said	Makamu Mwenyekiti
Mhe. Nassor Salim Ali	Mjumbe
Mhe. Said Omar Said	Mjumbe
Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali	Mjumbe
Mhe. Khadija Omar Kibano	Mjumbe
Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Mjumbe
Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil	Mjumbe
Ndugu Fatma Omar Ali	Katibu
Ndugu Mwanaisha Mohammed Kheri	Katibu

Naomba kuwasilisha.

Mhe. Naibu Spika, naomba dakika tano kidogo niweze kuchangia neno moja kama utaniruhusu.

Mhe. Naibu Spika: Ninakupa dakika tatu.

Mhe. Suleiman Sarahan Said (Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi na Mawasiliano): Mhe. Naibu Spika, nataka nitoe shukurani za dhati kwa wizara nzima ya Mawasiliano na Usafirishaji kuanzia Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na

Wakurugenzi wote wa Uwanja wa Ndege, Bandari pamoja na Nyumba, Shirika la Meli na wote wanaohusika kwa kutupa ushirikiano mkubwa katika kazi zetu tunazozifanya.
Lakini Mhe. Naibu Spika, pamoja na jambo hili mimi niungane nao katika kutafafutia changamoto matatizo ambayo mengi yalikuwa yametukabili katika wizara hii ikiwemo barabara ya Chake/Wete ambayo ni hatua ambazo tunafatilia mpaka Tanzania Bara tukiwa na ushirikiano wa karibu sana wa wizara hii Waziri na Naibu Waziri na Makatibu Wakuu wote.
Lakini vile vile tuko na mashirikiano mazuri kwa barabara ya Ole Kengeja. Lakini pia niwapongeze sana kwamba sasa hivi Bandari yetu ya Zanzibar ina mashine za kukagulia mizigo bila ya kufunguliwa. Kwa hivyo, niwapongeze sana wizara hii kwa kufanya changamoto za haraka haraka ili kuweza hivyo.
Lakini pia niwashukuru kwa kujitahidi katika kunasua matatizo ya Meli ya MV. Mapinduzi. Mheshimiwa pamoja na kwamba kuna maneno maneno ya meli lakini Mheshimiwa ile meli ni ya kisasa na ni ya *computerize* vizuri sana, lakini matatizo madogo madogo yakitokezea ni matatizo ya kiufundi. Lakini ni meli ambayo kwa kweli ni ya Kitalii si ya kupakia mabungo na kuku lakini Mhe. Rais ametupenda sana kutupa meli kama ile.

Lakini pia Mheshimiwa nataka niwapongeze sana Ofisi ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Ofisi ya Ujenzi na Uchukuzi wa Mawasiliano ya Jamhuri ya Tanzania katika kutupa mashirikiano katika kutoa changamoto nyingi ambazo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikiwemo madeni ya *ATCL* pamoja na SUMATRA, *ZMA* pamoja na kutafutia changamoto za *DANOUS*.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, hilo lilikuwa niweze kuangalia. Lakini pia niiishauri wizara katika haraka haraka Bodi ya *Condominium* ifanye kazi zake kwa haraka ili kusaidia kupatikana kwa mapato.

Lakini pia nataka nisema kwamba kitu kimoja naiomba Wizara ya Ardhi kwa haraka wajitahidi kwa kuwasaidia au kuwapa hatimiliki katika minara yetu ya kuongozea ndege pamoja na bandari zetu, hili ni mashirika ya serikali kwa hivyo ningeomba sana.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Suleiman Sarahan. Sasa Waheshimiwa Wajumbe, nina wachangiaji watano na kama nilivyosema mwanzo kwamba kazi hii tunatakiwa tuimalize leo. Kwa hivyo, nawaomba wana wale wachangiaji wote ambao watachangia, basi nitawapa dakika kumi kumi, na itatubidi baadae tuongeze muda kwa ajili ya kumalizia kazi hii.

Kwa hivyo, nawaomba sana mambo ya kurudia rudia na pongezi nyingi, hizo mzikatekate ili muende kwenye hoja ambayo itaweza kujibiwa na Mhe. Waziri. Kwa hivyo, naanza na Mhe. Simai Mohamed Said, baada ya hapo atafuatia na Mhe. Suleiman Makame Ali, na ajitayarishe Mhe. Jaku Hashim Ayoub.

Mhe. Simai Mohamed Said: Ahsante Mhe. Naibu Spika, na mimi kwa kuheshimu kiti chako juu ya suala la muda nitajitahidi kutumia dakika tano, ili na wenzangu wazidi

kupata muda na wao pia waweze kutoa mawazo yao na kuweza kuishauri serikali. Kwa hivyo, naomba uniruhusu niende kwenye mchango wangu moja kwa moja.

Mhe. Naibu Spika, jambo la kwanza nilikuwa nashauri kwa wizara husika tupatiwe elimu au masomo au tupigwe msasa juu ya suala zima la sera ya taifa juu ya suala zima la usafiri, kwa sababu wengine inaelekea ufahamu wetu bado ni mdogo. Kwa hivyo, sio vibaya ikawa tunakwenda sambamba baina ya serikali na sisi Wajumbe wa Baraza. Lakini leo pia nataka niseme kitu kikubwa juu ya Bandari ya Mpigaduri na mawazo yangu ambayo niliyokuwa nayasema kuhusiana na Bandari ya Bumbwini.

Mhe. Naibu Spika, mimi ni mjumbe wa Kamati ya Bajeti na nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa busara za Mwenyekiti wetu pamoja na wizara husika tulipelekwa pale Mpigaduri Maruhubi tukaonana na wataalamu kutoka Bandari, na kwa kweli maswali yangu yote ambayo nilikuwa nayauliza juu ya Mpigaduri na masuala mazima juu ya kima cha maji na upepo kwa upande wa Bumbwini. Kwa hivyo, nimepata ufafanuzi mzuri. Mimi kuanzia leo nitakuwa mpigadebe wa Bandari ya Mpigaduri.

Mhe. Naibu Spika, pia nimeona juu ya suala zima la vifaa ambavyo vinataka kununuliwa na imepangwa katika bajeti ya mwaka 2017 kuelekea 2018, ambapo serikali imesema itanunua mashine za *Paver* ambayo sagasaga mawe, *Bitumen Sprayer* na *Asphalt Plant* mtambo mpya.

Mhe. Naibu Spika, nimuombe sana waziri mtambo uliokuwa unatumika sasa hivi, ni mtambo ambao umedumu kwa miaka mingi sana. Kwa hivyo, atuhakikishie wakati tender itakapoanza mfumo mzima wa kununua hivi vifaa basi uwe ni endelevu, tupate mashine nzuri na mimi naamini Mhe. Waziri wetu Balozi Ali Karume ana uzoefu mzuri na utaalamu wa kupata mashine za kisasa ambazo zitaweza kudumu na kukidhi haja, ili na yeye pia aweke historia katika nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, jengine juzi nilizungumza suala la meli ambazo zinazoegesha. Mimi Mhe. Naibu Spika, napata kidogo ukakasi kuwa naona meli zinapaki katika Bahari ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini baina ya eneo la Bagamoyo au Saadani kwa kuelekea upande wa visiwa vyetu vya Unguja. Huwa najiuliza je, hizi meli zinatambulika kwa upande wa Bandari yetu ya Zanzibar na kama kuna malipo wanalipa Zanzibar au katika Bandari yetu ya Dar es Salaam au ndani ya Jamhuri ya Muundano.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, ningeshauri wizara husika ijiridhishe nipate maelezo na kama tupo sawa, basi naamini tunakwenda sambamba. Lakini pia alizungumza katika moja ya maagizo juu ya suala zima la ununuzi wa *ILS* ambayo ni *Instrumental Landing System* kwa ajili ya *Airport* yetu ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, mimi nashauri juu ya ununuzi wa mashine hii, umakini unahitajika tupate kitu cha kisasa *tender* zitakapopatikana ziende kwa mujibu wa sheria zetu za nchi, na usimamiwe moja kwa moja mradi na Mwanasheria wetu Mkuu ahakikishe haya yote yanafanyika bila ya ubadhirifu na hakuna upendeleo katika Makampuni ambayo yatasimamia katika vifaa kama hivi ambavyo ni muhimu kwa taifa letu.

Pia Mhe. Naibu Spika, nishauri katika ujenzi mzima wa *terminal II* ambao umezungumziwa. Kamati yetu ya bajeti ilipokwenda kutembelea pale, tuligundua vitu viwili kimoja ni cha muhimu. Nimpongeze sana Naibu Katibu Mkuu ambaye alikuwepo kwa niaba ya Katibu Mkuu, walikuja siku ile tukakaa nao na tukawauliza maswali. Lakini eneo la Kaskazini ambapo ndege kubwa zitakuwa zinaingia katika zile *Tubes au Air Bridge,* lakini kwa chini katika sehemu ya *arrivals*, wakifika pale wageni sehemu ni ndogo sana. Kwa hivyo, kwa mkono wa kulia ambapo panatarajiwa kujengwa *VIP* kwa ajili ya wageni mashuhuri, basi ikiwezekana mshauri elekezi au huyo *consultant* ambaye atatumika wabadilishe.

Mhe. Naibu Spika, hayo ni mawazo yangu, kwa sababu eneo halitoshi na kama patakuwa na ndege mbili kubwa zitaingia kwa wakati mmoja, basi pana hatari kwamba wageni watakuwa wako nje kwa upande ule wakisubiri kabla ya kuingia kutambulikana pamoja na *immigration* zetu. Kwa hivyo, waangalie ni jinsi gani wanaweza kuiondosha ile *VIP* na kubadilisha pale ule mfumo mzima katika ile sehemu ya *arrival* kwa upande wa Kaskazini juu ya *Terminal II*.

Mhe. Naibu Spika, pia amezungumza Makamu Mwenyekiti wa Kamati husika na niwapongeze juu ya suala la *Condominium Act* Kwa kweli na mimi naungana nao juu ya masikitiko yao. Suala la *Condominium Act* linahitaji lifanyiwe kazi kwa haraka na viongozi wote pamoja na *ZIPA* na wizara zote zinazohusika waanze utaratibu, kwa sababu hili jambo lilianzishwa kwa nia njema ili tuweze kuendeleza nchi yetu.

Jengine Mhe. Naibu Spika, ni suala la Mshauri Elekezi juu ya barabara ya Uzi, kutoka Unguja Ukuu hii ya baharini ambapo kwenye mikoko kuelekea mpaka Uzi pale juu. Natumai kwamba mshauri tayari atakuwa keshapatikana, sijapata kusikia kwenye ripoti. Lakini nakumbuka Mhe. Waziri wakati anayazungumza alisema hili jambo litaanza mwaka huu, sasa sijui tunatarajia lini, kama ni mwaka huu au katika mwaka wa fedha mpaka kuelekea mwaka 2018.

Mhe. Naibu Spika, nimalizie kwa kusema kitu chengine ni juu ya suala zima la mkonga. Mhe. Naibu Spika, fununu nilizozipata ni kwamba mkataba wa serikali na Kampuni ya Zantel umevunja, na kwamba sasa wana mpango mkuu wa kusimamia suala zima la mkonga na matumizi yake chini ya wizara. Suala hili naunga mkono litaongeza mapato ya serikali na wananchi, Wazanzibari na wawekezaji wote wataendelea kupata huduma bora.

Mhe. Naibu Spika, jengine ambalo nataka niligusie dogo, kwa sababu nimelizungumza na nitakuja kulichangia katika kamati nyengine inayohusika na utalii na kazi. Kuhusu barabara ya Fuoni kuelekea Tunguu, nina wasiwasi fedha ambazo zilizotengwa au zinazotafutwa, pamoja na dola milioni 58 zilizotengwa kwa ajili ya mradi wa *Terminal II*, zinazohusiana na kima cha chini ambapo hawa *unskilled* na *skill labour* watatumika. Karibu matumizi ya shilingi 25,000 na 30,000.

Mhe. Naibu Spika, wakati tunaandaa bajeti yetu na matumizi ya ujenzi mzima zilikuwa sheria tofauti na ambapo sasa hivi itahitajika serikali kulipa kwa ajili ya vibarua. Kwa hivyo, nashauri sana wizara ianze kujipanga kuangalia kwamba haya yote yataanza

kukidhi na mradi huu hautakuja kukwama, ambapo pia ni azma ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kukamilisha katika ahadi zake kuelekea mwaka 2020, na hasa katika ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo machache niliyozunguza kwa ajili ya muda, naunga mkono hoja kwa asilimia mia juu ya mia. Nakushukuru sana kwa nafasi uliyonipa, ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mhe. Mjumbe. Mchangiaji anayefuata ni Mhe. Suleiman Makame Ali, ajitayarishe Mhe. Jaku Hashim Ayoub na baadae atafuata Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf. Naomba waheshimiwa muda.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Mhe. Naibu Spika, mimi sitokuwa na muda mkubwa sana kama kawaida yangu unavyonijua.

Mhe. Naibu Spika, mimi niende moja kwa moja katika ukurasa wa 9, kamati inaitaka serikali kwa kupitia Idara ya *UUB*, kuhusu masuala ya utengenezaji wa barabara ya Wete/Chake Chake ambayo imepitia Ziwani barabara ile.

Mhe. Naibu Spika, mimi niiombe Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji chini ya Mhe. Waziri mahiri komredi Mhe. Balozi Karume, kwamba mpango huu wa tathmini ya wale ambao watahusika kwenye masuala ya kupisha ujenzi walipwe kwa wakati unapofika, isijekuwa tena bado huyu hajaondoa nini, bado huyu hajaondoa nini ili kurahisisha kazi zile za ujenzi wa barabara kwenda haraka sana.

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo niende kwenye suala la bandari. Hapa kwenye ukurasa wa 10 Kamati inaiomba serikali pamoja na wizara kwa kupitia shirika zifanye juhudi kuhusu masuala ya bandari.

Mhe. Naibu Spika, nadhani mara nyingi tunazungumzia masuala ya bandari. Kama kule Pemba Wesha kuna bandari ile ya Wesha, bandari ile ni nzuri sana na imetengenezwa kwa ajili ya kuingiza mapato katika nchi yetu hii. Lakini Mhe. Naibu Spika, bandari ile niseme kwamba kuna msongomano mkubwa sana Mkoani ambapo kwamba kule Mkoani ni sehemu ya kupitia abiria. Lakini leo bandari kama ile ya Wesha imekaa tu.

Kwa hivyo, mimi ningemuomba sana Mhe. Waziri akafanya mpango wa kuongeza kina cha maji katika bandari ile ya Wesha, ili kwamba zile meli za mizigo zinazokwenda kule kushusha saruji na mambo mengine ziweze kufika pale. Kwa sababu ukiwaangalia wafanyabiashara wengi walioko Pemba wako Chake Chake, kwa hivyo Chake Chake na Wesha ni karibu sana. Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri na wizara yake walifikirie sana suala hili, walichukuwe na walifanyie kazi.

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo niende kwenye suala la meli, kwamba kamati imeitaka wizara kwa kupitia serikali kuhakikisha kwamba imepatikana meli nyengine ya abiria. Mhe. Naibu Spika, kwanza niipongeze sana Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar, chini ya uongozi mzuri na mahiri wa Mhe. Rais Dk. Ali Mohammed Shein. Alitufanyia

suala hili ili kuona kwamba Meli hii ya Mapinduzi itakuwa ni mkombozi wa wanyonge hususan wanaotoka Pemba kuja Unguja na wanaotoka Unguja kwenda Pemba.

Lakini Mhe. Naibu Spika, cha kushangaza meli hii niseme sijui ni changa la macho au sijui niseme nini ili iweze kufahamika. Kila siku meli hii utasikia mlango haufunguki, kesho utasikia meli oil ni mbovu, sijui kesho utasikia sijui meli ina tatizo gani. Mhe. Naibu Spika, mimi nataka nijui hii meli tatizo lake ni nini, hata kwamba meli ile mpya hata miaka mitatu haijafika kwamba leo utasikia imeharibika nini na kesho imeharibika nini.

Mhe. Naibu Spika, kama unavyojua sisi Wapemba au sisi Wazanzibari wengi hatuna uwezo wa kupanda ndege tunategemea meli. Lakini sasa leo Mhe. Naibu Spika meli hii ambayo tunaitilia tamaa, lakini tukiiona meli hii kila siku inatengenezwa tengenezwa na mkondo wa Nungwi kama tunavyoujua, basi tunakata tamaa kusema kweli.

Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri na hili suala la kamati lichukuliwe kwenye serikali na lifanyiwe kazi, na nina imani kutokana na uongozi mzuri wa Mhe Rais, basi ni kwamba meli nyengine itapatikana, lakini wale watakaoteuliwa kwenda kutafuta ile meli basi watafute chombo ambacho ni cha uhakika, kizima na chenye umadhubuti mzuri zaidi. Sio kwamba waondoke hapa na koba la mapesa, wakifika kule wachukuwe chombo watakacho wao watuletee hapa. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, zile ni pesa za wananchi, wavuja jasho, wanyonge wa Zanzibar. Kwa hivyo, naomba sana wizara hii pamoja na viongozi watakaoteuliwa kwenda kutafuta vyombo hivyo, watafute vyombo ambavyo wajuwe hivi ni vyombo vya uhakika. Mhe. Naibu Spika, lengo ni kupiga hatua za kimaendeleo ili kutekeleza ilani ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo niende kwenye suala hapo hapo la barabara. Mhe. Naibu Spika, leo asubuhi hapa tumemsikia Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji akizungumzia suala la bodaboda. Mhe. Naibu Spika, na yeye Mhe. Naibu Waziri alikiri siku moja humu kusema kwamba wale vijana wa bodaboda ndio ajira yao, na ni kweli Mhe. Naibu Spika, mara nyingi tunapiga kelele hapa kwamba vijana Zanzibar ajira hakuna, wasitegemee serikali wajiajiri wenyewe. Leo Mhe. Naibu Spika, mtu keshakopa kanunua pikipiki, kama kuna sheria basi watungiwe wale ili waweze kujiendesha, kwa nini kule Bara waweze kufanya vile sisi hapa Zanzibar nchi ndogo hii mtu anaweza kuvunja sheria, kama atavunja sheria barabara basi hafiki Nungwi keshakamatwa. Kule Pemba kila pahala kuna geti, basi mtu avunje sheria asikamatwe Mhe. Naibu Spika. *(Makofi)*

Kwa hivyo, mimi naomba sana suala hili, kama ni sheria basi watungiwe wale vijana wa bodaboda, ili kupunguza wimbi la vijana huko mitaani kwa sababu tunapiga kelele kila siku hapa, kwamba vijana wanapiga mapanga sijui wanafanya nini, basi ni hao hao Mhe. Naibu Spika, akikuona wewe na simu ya kupangusa ataitaka, lakini sasa kazi hana atafanya nini atakupiga panga ni kweli.

Kwa hivyo, naomba Mhe. Naibu Spika, hii walichukuwe Mhe. Waziri na waweze kuwatungia sheria hawa vijana, kwa sababu ndio tegemeo letu, kesho kutwa mwaka 2020 tunawataka vijana au tunawategemea vijana nikiwemo na mimi tunawakusanya katika viwanja mbali mbali ili kuwaomba kura zao Mhe. Naibu Spika. Sasa leo tukisema kwamba tuwazuwie kuendesha bodaboda basi tuwatungieni sheria ambazo kwamba tukijua hizi sheria wakizikiuka basi mtu hafiki Makunduchi, hafiki Mkokotoni akamatwe kwa sababu Zanzibar ni ndogo. Lakini leo ukisema kwamba wale vijana wasiendeshe kwa sababu hawana sheria basi tutakuwa tunawaonea. Hiyo kusema kweli itakuwa tunawaonea, hiyo itakuwa kusema kweli hatukuwatendea haki.

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo niende kwenye suala hilo hilo la barabara na Mhe. Naibu Waziri nilimsikia asubuhi vile vile akizungumza kuhusu suala la barabara hususan madaraja. Mhe. Naibu Spika, barabara nyingi zikijengwa madaraja kusema kweli hayatanuliwi. Kama lile daraja la Pondeani pale Mhe. Naibu Spika, alilolizungumza asubuhi Mhe. Naibu Waziri, alisema kwamba daraja lile ni zuri sana.

Kwa hivyo, naiomba kamati Mhe. Suleiman Sarahan alilisemea hili kwa sababu yeye ni mjumbe wa kamati na analiona. Mhe. Naibu Spika, kusema kweli daraja lile la kwendea kule Pondeani ukipita pale ni roho mkononi, pale kila siku mimi husema kwamba daraja hili iko siku mtu atakuja kubakia pale pale na gari yeke, kwa sababu lile daraja ni bovu. Kwa hivyo, naomba sana Mhe. Waziri uhakikishe kwamba madaraja ambayo ni mabovu yote yaweze kufanyiwa ukarabati na yatanuliwe, ili tuweze kupishana kwa nafasi katika barabara.

Pia Mhe. Naibu Spika niiombe vile vile wizara kwenye masuala haya ya barabara kwamba zinapotengenezwa zile barabara basi zitengenezwe zenye viwango na zenye kudumu kwa muda mrefu, sio kutengeneza barabara leo kesho ikawa na mashimo kama bao la soo. Mhe. Naibu Spika, naunga mkono hoja hii asilimia mia kwa mia.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante nakushukuru Mhe. Suleiman na ninakupongeza kwa *speed* yako, una *speed* kubwa sana ya kuzungumza. Waheshimiwa Wajumbe, sasa hivi anayefuata ni Mhe. Jaku Hashim Ayoub, Mhe. Jaku nakuomba sana ujali muda, halafu baadae atafuata Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf na ajitayarishe Mhe. Ali Suleiman Shihata.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, nimeanza saa 1:17 na bila ya kupoteza muda nije kwenye ukurasa wa 3, Mhe. Waziri naomba unisikilize kwa makini hapa. Katika bodi ulizotaja umetaja bodi 4 hapa, bodi hizo ni Bodi ya Usafiri, Bodi ya Usimamizi, Bodi ya Nyumba na Bodi ya Wakandarasi.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri nilikueleza unachagua wajumbe hawana sifa, Bodi ya Wakandarasi ya Usajili Wasanifu kuna mjumbe mule mmoja umemteua hana sifa, anatakiwa awe na digirii, umemchukua mtu mmoja sijui kwa sifa gani, tumemuona kajenga basi ujenzi wake utafikiri spoki ya baskeli imesimama jengo lake, halafu unakwenda kumpa sifa hizo ndani ni kitu cha kusikitisha. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, bila kupoteza muda hapo hapo kwenye kifungu namba 4, kamati inalitaka shirika la nyumba kufanya uhakiki wa kuzitambua nyumba zake zote na kuziorodhesha katika daftari la mali. Utekelezaji, kazi za kuzifanyia uhakiki wa kuzitambua na kuziorodhesha nyumba zake katika daftari na mali, shirika linaendelea na zoezi hilo limegawika katika maeneo manne.

Nyumba za Maendeleo, nini maana yake. Lengo ni kuwakomboa wanyonge, lakini kila siku nyumba zile zinapandishwa bei na hizi nyumba kazijenga marehemu baba yako, utakuwa humfanyii haki. Ni Rais ambaye kafanya kazi kubwa ya kuwakomboa wanyonge wa nchi hii, kila siku nyumba zinapandishwa bei na kuzitengeneza zinakushindeni, hii sio haki, lengo halijapatikana. Lengo ni kumkomboa mnyonge katika nyumba zile. Shilingi laki mbili, laki tatu, laki tano inaangaliwa na vyumba, na kutengeneza inawashinda, hata yale makaro kuyasimamia yanakushindeni. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nisipoteze muda nije katika ukurasa wa 4, kuhusu bodi ya *management* ya shirika imelipokea agizo hilo na imeahidi kuongeza katika kasi ya utekelezaji wa majukumu yake. Nimeomba wenyeviti, liangalieni hata Mwenyekiti wa Shirika la Meli na yeye liangalieni.

Mhe. Naibu Spika, nije kwenye ukurasa wa 5 kuhusu *Darajani Corridor*. Niliuliza hapa kipi kinachokuja mwanzo katika uchoraji na ramani. Leo tumevunja Darajani, tumevunja Kijangwani mwaka unakwenda zake, tumewadhulumu wanyonge muda huu wote hakuna tunachokifanya,imekuwa hadithi kama uwanja wa ndege. Kama hatujawa tayari na mipango hii tusifanye hichi kitu, hali ya maisha ni ngumu. Ile subira kuwa yavuta heri, sasa hivi sijui anavuta sigireti au vipi. Hali ni nzito, tumevunja maduka pale Darajani tumepoteza pesa ngapi, wafanyakazi wangapi, leseni ngapi, umeme na kila aina maana yake, kipi kinakuja mwanzo kabla ya ujenzi, ramani au michoro. Mhe. Naibu Spika, nafikiri imefika. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nije katika ukurasa wa 6, 12 Maagizo, Utekelezaji. Ushauri wa Kamati tumeupokea na tunaufanyia kazi sambamba na kutoa elimu kwa wamiliki wote wa nyumba na majengo mbali mbali.

Mhe. Naibu Spika, hapa pana majumba mengi karibu mabovu na naomba kuyataja Mhe. Waziri yafuatilie, Wizara ya Kilimo ya zamani nyuma *People Palace* hebu kaliangalie lile jengo likoje miaka mingapi Serikali imechukua hatua gani mpaka muda huu, jengo la Wizara ya Kilimo la zamani nyuma *People Palace*, Jumba la Katiba na Sheria la zamani Wizara au Serikali imchukua hatua gani mejengo yale, nyumba ya kulelea watoto hivi sasa salama Mhe. Shadya kahamisha watoto wale kawajengea nyumba ya kileo Mazizini nimpongeze sana Mhe. Shadya Karume, mnyonge mnyongeni haki yake tumpeni.

Tuangalie nyumba ya *People Palace* jumba la historia la kifalme mna vitu vya thamani watalii wanaingia mle ndani, mna gari mle ndani mna vitu vya maajabu ajabu maana yake linashinda linaanza kuvuja halafu huku tunaangalia kupiga kelele mambo mengine kuna nyumba kuna mikopo hatuwezi, tukarabati hizo tulizokuwa nazo kwanza.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kutoa hapo nije namba 18 niipongeze sana Kamati hii ikiongozwa na Mwenyekiti Makini Mhe. Hamza Hassan Juma, agizo limepokea kwa mwaka huu Wizara imetenga bilioni tano, hapa alisema kama kuna watu wanaostahiki sifa *UUB* chini ya uongozi wa Ali Tahir huyu jamaa hana jumamosi, hana jumapili, hana sikukuu saa moja ukienda utamkuta kwenye kazi si msifu, jimboni kwangu hajanisaidia barabara lakini anafanya kazi kilillahi. Hana mvua wala vitendea kazi hana hivyo hivyo anaunga pechi anatia huku anafanya kazi tumeangalia Michenzani pale, tumeangalia njia ya Unguja Ukuu ni watu wa kupongeza sana tunapiga kelele lakini bajeti yao ni ndogo.

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo kwa haraka haraka bila ya kupoteza muda nije shirika la Bandari nae nimpongeze Mkurugenzi wa Bandari kazi aliyofanya sisi sote tumeona usiku mchana makontena pale mizigo inafika mpaka wengine tunalipa *penalty* pale kwa kuchelewa, kazi kubwa wamefanya na meli hazikai sana.

Mhe. Naibu Spika, nije ukurasa wa 11 Mhe. Suleiman kazungumza hapa Kamati inaiomba Serikali pamoja na Wizara kuangalia uwezekano wa kutafuta meli nyengine, mimi naomba isitafutwe meli nyengine tutengeneze hii iliyokuwepo kwanza tuliyonunua mpya, si tumenunua mpya na haifanyi kazi tutengeneze hii kwanza hizo pesa tulizopata.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hapo nije kwenye ukurasa wa 13 Kamati inaiomba Serikali pamoja na Wizara kushiriki kikamilifu Mamlaka ya Viwanja vya ndege hatua zote za uendelezaji wa jengo hili, Mheshimiwa hapa tuna matatizo na sijui tunalipa riba kiasi gani kwa uwanja wa ndege ule, uwanja *terminal* nafikiri sasa hivi kuna mabuku mle ndani kuna manyoka ndani hakuna kinachoendelea. Lakini AG hapa kidogo tusaidie pana mkataba mwengine umetoka juzi *tender* lakini sheria zimefuatwa pana msokotano hapa taratibu zote zimefuatwa Uwanja wa Ndege mtu kashajaza *tender* na kashashinda lakini sasa anataka kusokotwa.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hapo nije na kuangalia majumba yale ya Michenzani, majumba yale nilikuwa nikisema narudia kwa mara ya pili, majumba yale kodi zinakodishwa kiholela, lengo la aliyejenga nyumba zile hafanyiwi haki, kwa nini Serikali isiandae kujenga nyumba nyengine mpya ili tukapandisha kodi. Leo kodi zinapanda kila siku baada ya muda huu baada ya muda huu, baada ya hichi baada ya hichi.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo naomba nisipoteze muda sana.

Mhe. Nadir Abdullatif Yussuf Al-Wardy: *Bismillahi Rahmani Rahim* muda wangu utaisha saa 1.45 nakushukuru Mhe. Naibu Spika, mimi nitaomba nianze na machache kuchangia ripoti hii ya Wizara ya Mawasiliano na Ujenzi, kwanza ningeanza kutaka kuja kujibiwa suala la mashine za *X Ray* mbili zilizonunuliwa na Wizara hii ni shilingi ngapi mmezinunua mashine hizi, *guarantee* yake miaka mingapi na *brand* yake ni ipi.

Lakini suala langu la pili nataka kujua zile nyumba tulizozungumza watendaji wenu wa Wizara yenu waliowatepeli watu kwenye majenzi waliowauzia nyumba wakawatafutia njia nyengine wakawanyang'anya mmefikia wapi, mmewachukulia hatua gani na wale waliotapeliwa umewafidia nini hadi hivi leo.

Mhe. Naibu Spika, jengine nyumba ya Beit el Ajaib, *Old fort* Ngome Kongwe na *Museum Palace* ni lini majumba yale mtayafanyia *renovation* kwa sababu ni ngome ya utalii na ndio kivutio tunachoringia Zanzibar, yatafanyiwa *full renovation* mna *plan* gani na lini mnatarajia kuyamaliza kuyafanyia marekebisho na hasa Beit el Ajaib kimekwama nini hadi hivi leo wakati jumba lile halitaki kubomolewa linatakiwa kufanyiwa *Renovation.*

Jambo jengine Mhe. Naibu Spika, suala la mafuta petrol na Diesel Zanzibar bei tunayouziwa ni kubwa sana ningependa kujua Serikali ina-*charge* shilingi ngapi kodi kwenye masuala ya mafuta, kwa sababu ukiangalia *barrel* moja ni dola 50 lakini cha ajabu hapa Zanzibar sasa hivi lita moja ni shilingi elfu mbili, je wanatumia vigezo gani mpaka mafuta kufikia shilingi elfu mbili Zanzibar na wananchi kuumia. Kwa sababu nchi kama hii elfu mbili ni pesa nyingi sana kwa lita moja.

Lakini nakwenda mbio mbio kwa sababu nina mambo mengi nazungumzia *Red light za traffic light,* watu wanazifanya zile *red light* kama ni zao wao wanaziwasha na kuzifunga, tunachotaka kujua je wamewatayarisha mapolisi vipi katika *area* zile watu wanavyovunja sheria kuvuka zile *traffic Light* bila kufikia ile *time* ya *green light* kuweza kuwafukuza na kuwakamata mbele na kuwachukulia hatua, kwa sababu *traffic light* zimekuwa hazifuatwi kabisa. Mna taratibu gani za kuweka *traffic light* sehemu nyengine muhimu za Zanzibar zilizokuwa *business area* kama Magomeni na sehemu nyenginezo mpaka hivi leo *traffic light* hakuna, pale Mtoni sehemu inayosababisha ajali kila siku *traffic light* hakuna wakati vile vitu havitakiwi fedha nyingi. Ni lini mna utaratibu wa kufunga *traffic light* katika sehemu kila muhimu ya barabara.

Mhe. Naibu Spika, mimi ningezungumzia madaraja, madaraja Zanzibar yanaua kila siku madaraja hamutii *sign* hayana alama yoyote nchi hii ya kitalii sisi ni Wazanzibari tutajua sehemu gani kuna daraja lakini wageni hawatofahamu, wageni kila siku wanakufa. Uzembe unasababishwa na Wizara yenu husika. Ni lini madaraja yale mtayajenga kwa kupita gari mbili na kuweka *sign* pamoja na kuweka alama za barabarani sehemu zote Unguja na Pemba.

Mhe. Naibu Spika, jambo jengine taa za barabarani njia ya *Airport* hili nafikiri litamuhusu Mhe. Waziri wa Wizara ya Nchi Afisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara maalum za SMZ na Wizara husika ya Mawasiliano, barabara ya *Airport* hadi hivi leo hakuna taa hata moja kuanzia *Airport* mpaka mwisho wakati ile ndio *International*. Mtu yoyote anayekuja kiongozi katika nchi hii anapita njia ya *Airport* haiwaki taa ni aibu tumeanza kuweka Magomeni, Daraja Bovu lakini *Airport* sehemu muhimu barabara taa hakuna. Ni lini sasa mna utaratibu wa kuweka taa katika njia ya *Airport.*

Mhe. Naibu Spika, mimi nakwenda kwenye karatasi nyengine ningependa kujua *Airport* kwenye mashine za *Parking* ni nani aliyekabidhiwa eneo lile baada ya kutolewa aliyekuwepo na kumepita *tender* kampuni ngapi zimeshiriki na makubaliano yepi yamefanyika baina ya nyinyi Wizara na mtu ambae anaendesha.

Jambo jengine Mhe. Naibu Spika, Mji Mkongwe ningependa kuzungumzia kwamba hata nyumba zikiporomoka basi wajaribu kuzijenga kama zilivyokuwa mwanzo wasijenge kwa muundo mpya kuharibu mandhari ya Mji Mkongwe Zanzibar, huu ushauri wangu ningeomba sana Wizara ifikiria kujenga treni kuanzia Mjini hadi Nungwi, Mjini hadi Makunduchi pamoja na mjini, kwa sababu Unguja ni ndogo sana gharama yake sio kubwa ya hivyo waweke hata *treni ya lower Speed, medium size* sio lazima ya *high Speed* waweke treni kama ilivyokuwa wakati wa asili, watu hawataki kupanda gari wapande treni mambo yaendelee Mheshimiwa huo ni ushauri tu.

Mhe. Naibu Spika, ningependa kuzungumzia sehemu ya *Airport* sehemu za kupeleka mizigo na kuingia na kutoka, kuna watu wanaumwa na migongo wamefanyiwa *operation* watu wazima hawawezi kubeba mizigo, kwa nini Wizara hadi hivi leo hawajaweka kitengo maalum cha mtu anayetaka kubebewa mizigo akaweza kulipia halafu akabebewa mizigo mpaka nje au akafipitishiwa mpaka ndani matokeo yake wanalazimishwa kubeba mizigo wenyewe, kutia kwenye *Screen* na kushusha mnawavunja migongo watu wazima, hakuna nidhamu watu hawamuonei huruma. Ni lini Wizara sasa itaweka utaratibu wa kuweza watu kubebewa mizigo watapolipia.

Mhe. Naibu Spika, suala jengine ni lini sasa hii *Airport* iliyokuwa na mashaka kila siku itakwisha, kwa sababu *Airport* ile imekaa kama iliyosomewa Halbadiri kila siku haishi, tunataka tujue mkataba mpya mlioingia mmeingia na kampuni gani au ngapi, shilingi ngapi za Fedha ambazo mmeziomba ambazo Serikali inatakiwa kulipa na kwa miaka mingapi na lini itakwisha *Airport* ile. Kwa sababu Mhe. Rais mlimuahidi tokea miaka ya nyuma kwamba mtamkabidhi mpaka hivi leo hamjamkabidhi na sio kosa lake kosa lenu nyinyi, sikulaumuni mliokuwepo sasa hivi wapya lakini waliopita wote nawalaumu kwa sababu ngoma imechelewa.

Mhe. Naibu Spika, nataka kuja kujua *fire* mbili zilizonunuliwa na Wizara ya Mawasiliano bilioni 3,600,000,000/= zimenunuliwa kwa kupitia *tender* gani kampuni ngapi zimeshiriki ku-*bill tender fire* zile na nchi gani mmenunua. Kwa nini Wizara haijafikiria kununua *fire* za bei afadhali wakapata nyingi wakenda kununua *fire* mbili kwa bilioni 3,600,000,000/= ambazo hazina hata ngazi za kupanda ghorofa zaidi ya mashine ya *Propera* uki-*pull* inasukuma maji. Kuna *Fire* mbili za Mawasiliano na Vikosi nazungumza za Mawasiliano tunataka vielelezo.

Mhe. Naibu Spika, nataka kufahamu Wizara husika barabara yaani utafikiri Mwendawazimu aliyekuwa na mapechi, imenyesha mvua Unguja nzima barabara zina mashimo kwa utapeli unaofanyika. Barabara zinazojengwa Unguja zote ziko chini ya kiwango na cha kushangaza kila barabara kilomita moja inasemekana zaidi ya bilioni moja, tunataka kujua kila barabara tani ngapi ya uzito inachukua na mmekuwa na *guarantee* ya miaka mingapi mnapompa mjenzi anayejenga, na shilingi ngapi mnalipa kumlipa mtu kwa kila kilomita moja.

Mhe. Naibu Spika, suala la daladala tungeomba Wizara husika iwatilie mashine za *Speed limit* kwa sababu wenye daladala ni wendawazimu wengi wao wanaua raia kwa shilingi mia mbili na mia tatu, wawekewe *speed limit* ambayo haitozidi *speed* sitini kwa daladala

na wale wanaopeleka wageni *private hire* wawatilie *speed limit* isiyozidi *Speed* 80 kama mtu ana haraka aondoke masaa kabla ili apeleke wageni kwa njia ya utaratibu wenzetu wote duniani wanadhibitiwa na *speed limit*, nashangaa mpaka hivi leo sisi watu wanauliwa raia wetu kwa shilingi mia mbili au mia tatu daladala zinafukuzana wanashindwa ku-*control.*

Lakini vile vile Mhe. Naibu Spika, nimeona hapa kwamba kuna agizo wametenga bilioni 5 kwa ajili ya kununua magari ya UBB, ningeomba gari hizi zijekuwa ziwe gari yale mambo ya nyuma yaliyofanyika kutaka *percent* tuachane nayo tununueni gari kabila nzuri, gari za uhakika mambo yaende. Mambo yale ya kutaka watu tena wafaidike tununue vitu vibovu hatuendelei baada ya miaka miwili mambo yameharibika hatutaki kuyaona.

Mhe. Naibu Spika, hili buku kubwa na hasa Wizara hii nzito kweli, hapa tukiangalia kumeandikwa kwamba kuna mkandarasi *MECCO,* mimi nazungumza kila siku kampuni ya *MECCO* iko peke yake dunia hii. Hebu tuelezeni wanao-*bid* kampuni ni wangapi isitoshe huyu *MECCO guarantee* yake vipi kwenye ujenzi wa barabara, au kuna watu wazito ndio wanae mkononi ndio maana hii *MECCO* kila siku inaingia humu ndani. Mhe. Naibu Spika, imefika hatua sasa ya kutumbua sisi Wawakilishi kabla ya kufika kwa Mhe. Rais, kwa sababu naona Mhe. Rais sasa tunamuonea huruma yuko peke yake muaminifu lakini kazungukwa na madudu.

Mhe. Naibu Spika, mimi nataka kuzungumzia jengine hapa kuna suala hili la MV. Mapinduzi II lakini kuna meli inataka kuletwa nyengine ambayo imetengwa bilioni 18, tunataka kujua meli hii itagharimu shilingi ngapi kwenye Wizara hii na je pesa hizi mtalipa *cash* au pia mtakopa. Mhe. Naibu Spika, mimi nimpongeze Mhe. Waziri husika namuamini, Naibu Waziri, waweze kuangalia hali iko vipi chama huko nje kinasemwa vibaya kwa watu wachache wanaoharibu Serikali hii na hawa ndio tunaotaka kuwashughulikia.

Mhe. Naibu Spika, mimi sina mengi haya ndio mambo machache niliyozungumza leo nasubiri siku za mbele, nasubiri majibu yangu nakushukuru sana, namshukuru Mwenyezi Mungu nampongeza Rais wangu Dk. Ali Mohammed Shein ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Nadir nitasema kama nilivyosema jana kwa kuwa tunachangia utekelezaji wa Maagizo kuna baadhi ya mambo ambayo umeyazungumza hayamo ndani ya utekelezaji wa maagizo, kwa hivyo tutawapa nafasi Waheshimiwa Mawaziri hayo kuyajibu baadae, yatajibiwa yale tu ambayo yamo katika utekelezaji wa maagizo ya Kamati.

Mhe. Ali Suleima Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama hapa na kuchangia ripiti hii ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji. Mhe. Naibu Spika, nimpongeze Mhe. Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri ambazo wanafanya kuhakikisha kwamba tunakwenda vizuri ndio hali halisi ya usafirishaji katika nchi yetu.

Lakini mimi nitakuwa na machache sana Mheshimiwa kwanza niipongeze *UUB* kwa kazi zake nzuri wanazofanya Mhe. Naibu Spika, hasa tukizingatia ujenzi wa barabara ambazo wanazijenga. Pili niipongeze Serikali kwa kuhakikisha kwamba barabara zetu zinajengwa kwa haraka katika maeneo mbali mbali ya nchi yetu, mimi nitoe rai tu au niishauri Wizara kupitia *UUB* umefika wakati tuangalie ujenzi wa barabara umekuwa gharama kubwa sana lakini kiwango kinachojengwa kinaweza kuwa sahihi au pana mapungufu mimi si mtaalam. Lakini nasema pana usahihi barabara zinakufa upesi kwa kutokujengewa kinga baada ya ujenzi wa barabara nzima pembeni zinaachwa zikija mvua zinayayuka au zinayeyushwa na mvua na kuleta uharibifu wa haraka.

Naishauri Wizara wakati umefika kuzijengea barabara kinga na hizi zitanusuru wakati wa mvua mmong'onyoko ziondokane na ujenzi wetu maana leo barabara zetu ukipita Mhe. Naibu Spika, asilimia 80 ya barabara zetu utakuta pembeni ya barabara kama mna visu, mipira ya gari inakatika ovyo kwa sababu barabara hazina uzima katika pembe zake. Nimuombe sana Mhe. Waziri kupitia wataalam wetu wazifanyie matengenezo hayo.

Lakini kubwa niipongeze kwa dhati kabisa Wizara hii katika maagizo ambayo kamati imeagiza kuhakikisha kwamba *UUB* wanapatiwa vifaa vya kisasa, hilo nalipongeza kwa dhati kabisa na hasa tukizingatia kwamba *UUB* yetu inaweza kujenga barabara nzuri kuliko *MECCO*. Lakini bahati mbaya wanashindwa kutokana na nyenzo za vifaa. Niishauri Serikali kwa makusudi kwamba imeona pana haja sasa hivi kuongeza fungu la bajeti na limeongezwa, kwa mfano katika ukurasa wa 8 tumeona tu kuna bilioni tano zimeongezwa katika mfuko wa ununuzi wa vifaa mbali mbali kupitia Hazina, lakini kuna bilioni tisa kutoka mfuko wa barabara mimi naipongeza sana Wizara kwa kulijua hili na pana umuhimu wa kufanyiwa kazi haraka na fedha hizi zipatikane ili wenzetu wafanye kazi zao vizuri.

Mhe. Naibu Spika, nchi yetu ina historia yake katika ulimwengu na kila anayekuja hapa anataka kusoma historia ya nchi yetu na historia ni mambo ya kumbukumbu. Pamoja na wenzangu wamesema na mimi nasema kwa uchache kabisa, jengo la Beit el Ajaib ni hazina ya nchi hii na historia kubwa katika nchi yetu, ukisoma mle ndani na ukienda kuelekezwa mengi utakuta kwamba kuna mambo mengi yalijitokeza mpaka kupigwa mzinga ili ipungue nyumba ile pana historia mle ndani.

Niiombe sana Serikali kupitia Mamlaka ya Mji Mkongwe wajitahidi sana wazungumze na *UNESCO* wanapokwenda kufanya kila kitu mazungumzo yao yawe ya haraka lijengwe jengo lile ili tija ya pato la nchi yetu liongezeke, tunaamini Mhe. Naibu Spika, jengo lile kama litajengwa na likakidhi haja watalii wanaongezeka siku hadi siku. Kwa hivyo naipongeza serikali kwa kuliona hilo na Kamati kuishauri Wizara na Wizara imelipokea, basi nawatakia kheri.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa naomba kidogo ukae, Waheshimiwa Wajumbe kwa kuwa muda wetu wa kumalizia leo umekaribia na kwa kuwa tuna uwezo wa kuongeza muda kwa kuweka kando kanuni ningemuomba Mhe. Mwanasheria Mkuu atuongezee muda aweke kando kanuni ili tuweze kumaliza shughuli yetu hii leo hii, Mhe. Mwanasheria Mkuu karibu.

KUAHIRISHA BARAZA KABLA YA WAKATI WAKE

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja ya kutenga kando kanuni ya muda ambayo ni Kanuni ya 23 ili tuweze kuendelea na mjadala mpaka hapo Mhe. Waziri atakapofunga mjadala huu. Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe Mhe. Mwanasheria Mkuu ameshatoa hoja wale wanayokubaliana nayo wanyooshe mikono, wanaokataa waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, jengine nitakalolichangia kwanza niipongeze sana Kamati kwa kuona kuna haja ya kutafutwa X-ray. Katika ulimwengu wa leo Mheshimiwa tuakapopita popote unatakiwa uhakikishwe usalama wetu, usalama wa vifaa uliochukua na mizigo yako. Kwa hivyo niipongeze Wizara kwa kuliona hili na hatua ya mwanzo iliyochukuliwa ukipita katika bandari zetu sasa hivi panapitika salama usalimini.

Mhe. Naibu Spika, naishauri Wizara, dunia ya leo hakuna kuaminiyana na utakaposema mtu upite tu uendezako bila ya kutafuta ukaguzi ni hatari, watu wana njia nyingi ya kuhifadhi mambo yao ambapo unaweza kupita pahala ikawa sio salama. Naiomba sana wizara kupitia Shirika la Bandari wasafiri wote wanaotoka Pemba wanaokuja Unguja wasachiwe na mizigo yao, na wanaotoka hapa kwenda Pemba wasachiwe. Tumeshuhudia udanganyifu mwingi sasa hivi watu wanakamatwa na mabangi, madawa ya kulevya wanapita bandari hiyo wanatoka Unguja kwenda Pemba na wanaotoka Pemba kuja Unguja.

Mhe. Naibu Spika, tumeshuhudia hivi karibuni watu wametoka hapa vizuri tu kufika Pemba wamedakwa, wengine wamejidai Mahajati wakubwa wakubwa na mashungi makubwa wamedakwa na kete. Niiombe sana wizara muhali uondoke sasa hivi sio wakati tena wa kuaminiana. Hili tusilichukulie mzaha tulichukulie kweli kweli.

La mwisho Mhe. Naibu Spika, kwa kuokoa muda, nalipongeza Shirika la Bandari kwa kazi nzuri wanazofanya, nalipongeza Shirika la Meli, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege, lakini juhudi zao Shirila la Meli panahaja ya serikali kama wenzangu walivyosema na mimi nasema na kwa bahati nilileta swali bahati halijasomwa bado ziongezwe meli za kileo zinazoweza kwenda *speed* ya ushindani. Kwa sababu hatari iliyokuwepo moja, mfanyabiashara mmoja akimiliki kila kitu ni hatari huko mbele ya safari tunakokwenda.

Niiombe serikali kwa dhati kwa makusudi haiwezekani mfanyabiashara awe juu kuliko serikali, tutafute meli zetu ambazo zitatusaidia kwa usafiri wa haraka na bidhaa mbali mbali kwa usafiri wa kutoka Unguja kwenda Pemba na Pemba kuja Unguja kwenda Bara mpaka Tanga mpaka Comoro.

Baada ya hayo Mhe. Naibu Spika, naunga mkono asilimia 100 ripoti hii namtakia kheri Waziri na watendaji wake wote ili tufanikishe katika malengo yetu.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Ali Suleiman, mchangiaji anayefuata ni Mhe. Mohammed Said Mohammed ajitayarishe Mhe. Mwanaasha Khamis Juma na mchangiaji wetu wa mwisho atakuwa Mhe. Mussa Ali Mussa.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Naibu Spika, niendelee kukushukuru sana lakini nichukue fursa hii kuwapongeza wote walioandaa taarifa hii taarifa nzuri sana ingawaje inakosa mashiko ya kujadiliwa.

Mhe. Naibu Spika, utaratibu ambao Baraza limefanya ni utaratibu mzuri sana wa kujadili maagizo ya Kamati mbali mbali katika kipindi hichi, ila kila zuri linachangamoto yake, sasa naomba tu nitaainisha baadhi ya changamoto ambazo nimeziona kwenye taarifa hizi kwa ufupi wake sana.

Mhe. Naibu Spika, nataraji sana katika kipindi kijacho taarifa hizi zitaimarishwa ili ziwe bora zaidi na kuweza kuondoa changamoto nyingi sana ambazo zimeweza kujitokeza. Taarifa hizi ni nyepesi sana. Ukiziangalia kwa mtu ambaye kidogo unaziona na una taarifa zimekosa hata *supporting data*, taarifa hizi ni nyepesi sana, hatuwezi leo kuwa tunajadili kitu hichi, maagizo ya wananchi tunaweza kuyajadili rahisi rahisi kwa pamoja. Majibu yametolewa rahisi mno, sasa tungeomba wenzetu wakati watakapokuja.

Mhe. Naibu Spika, nitatoa mifano ya watu wawili lakini nitatoa mfano wa mtu mmoja ndiyo zaidi. Kuna mtu anaitwa Ndute mtu huyu anawadanganya wenziwe siwezi kumjadili, lakini nitamjadili Ndonje. Ndonje maana yake ni yule mtu ambaye anaingia ndani, lakini akiingia ndani ni lazima atoke. Na sisi tumeingia humu ndani tutatoka kwenda kwa wananchi, watatuuliza maagizo yao haya halafu tunawajibu rahisi rahisi wanaona, siku hizi watu wote wanaona. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, Wajumbe wako humu wana msiba mkubwa sana na msiba huo wanalia katika vilio vitatu. Kilio kimoja unaweza ukawaona wametulia kumbe wanatokwa na machozi huyaoni, lakini wengine unaona machozi tu huwasikii sauti, lakini wengine wanapigwa makelele akiwemo Mhe. Mohamed Said, Nadir Abdul-latif na Hamza Hassan Juma na kwa sababu hiyo basi wanataka jambo hili liende vizuri sana. Lakini wengine ambao waliokuwa hawasemi pengine hawajui wajibu wao, au sheria zinawapiga chenga, ndio kama hili wakiambiwa Mhe. Naibu Spika, naongeza muda wanaitikia tu tuongeze lakini *time* imekwisha. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, nilikuwa nataka nipeleke *massage* leo na nitumie ile Kanuni au nitumie Katiba kifungu anachokitumia sana ndugu yangu Mhe. Jaku Hashim Ayoub, kifungu cha 43(5) kuna *collective responsibility* lakini bahati mbaya sana Makamu wa Pili hayupo, salamu hizi apelekewe. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, Makamu wa Pili wa Rais achukue juhudi kubwa kuweza kutuletea ripoti hizi zikiwa zina mashiko, hii ripoti haina mashiko. Ripoti zote nimejaribu kuziangalia hazina mashiko. Tumeletewa ripoti ya Nyaraka imekuwa ndogo sana jana, sikuweza tu kuchangia nilisema hata nisichangie kwa sababu ripoti hizi hazina mashiko ya kujadili Baraza Tukufu kama hili.

Mhe. Naibu Spika, labda sasa niende moja kwa moja kwenye hoja hii. Nataka kuingia kwenye maagizo ya Kamati hoja Namba 7 na naomba niinukuu. "Kamati inaomba Wizara ihakikishe kwamba inatunga kanuni haraka ili kusaidia utekelezaji wa Sheria Nam. 6 ya Mwaka 2014, hali ambayo itapelekea ugumu kwa upande wa Shirika katika kutekeleza majukumu yake.

Utekelezaji, Mhe. Naibu Spika, Shirika linaendelea na utungaji wa Kanuni. Sasa ndiyo nikasema hii *document* ina kasoro mimi sijawahi kuona kuwa Shirika linaweza likaunda Kanuni. Ninayo hapa imenibidi niende nikaitafute haraka ambayo Sheria hii imetiwa na Mhe. Rais saini tarehe 31 Disemba 2014. Naomba ninukuu kifungu cha 52 cha Sheria hii kinasema *"The Minister shall make regulation for the better carring out of the purpose of the profession act"*. Sasa huyu Waziri ndiye anayetunga Kanuni hizi, Kanuni hizi haziwezi kutunga shirika, hizi ndiyo kasoro ambazo zimejitokeza.

Mhe. Naibu Spika, inatia hata kichefu chefu kuijadili hii ripoti, haiwezekana ikawa tunakaa. Lakini huku anasema nyumba za Kilimani anaagizwa hapa katika Nam. 3 Kamati inaomba Wizara kushirikiana na Shirika la Nyumba kuanza kuzifanyia matengenezo nyumba ambazo zinaweza kutengenezeka na baadaye kuongezea mapato.

Mhe. Naibu Spikali nilikuwa nikililalamikia sana nyumba za maendeleo za Kilimani, kwanza *drainage system* zote mbovu halafu wananambia tuna nyumba sita. Mimi nimeshawaambia waje waondoe zile nyumba zao sita watuachie zetu zilizobaki kama serikali haiwezi kuzitengeneza, lakini bado hata suala hili limekuwa gumu. Ningeomba sana Serikali ijitahidi angalau kufanya kitu ambacho kinaweza kuonekana.

Mhe. Naibu Spika, niende kwenye Agizo Nam. 8, Kamati inaitaka bodi ya nyumba ifanye kazi zake kama sheria inavyoagiza au Mwenyekiti, ajiuzulu kwa kushindwa kazi aliyopewa pamoja na Wajumbe wake. Hii kamati ya wananchi inazungumza hivyo, utekelezaji wa Wizara, Bodi na *Management* ya Shirika imepokea agizo hilo na imeahidi kuongeza kasi katika utekelezaji wa majukumu yake.

Mhe. Naibu Spika, inabidi ucheke kwa haya ya utekelezaji tu, huu utekelezaji hauna chochote maana yake imepokea tu kirahisi rahisi, lini inapokea. Mhe. Naibu Spika, mimi niwape wanzangu kwa sababu naona hata nikiijadili hii *document* itakuwa ziro sifuri. Naunga mkono hoja.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mohamed Said Mohamed ahsante, sasa tunampisha Mhe. Mwanaasha Khamis Juma na baada ya hapo wa mwisho atakuwa Mhe. Mussa Ali Mussa na ajitayarishe Mhe. Waziri kwa ajili ya kuja kujibu hoja.

Mhe. Mwanaasha Khamis Juma: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kwa kunipa nafasi hii kutoa ushauri au kuchagia katika ripoti ya Ardhi na Mawasiliano. Kabla sijaanza kutoa ushauri wangu nichukue fursa hii kuungana na wananchi wa Jimbo la Chukwani katika msiba ambao umetupata siku ya jana ya kufariki kwa Katibu wetu wa Tawi la Shakani. Nichukue fursa hii na kuwaambia tuwe pole na tuwe wavumilivu katika

kipindi hiki cha msiba na Mwenyezi Mungu ampe safari ya heri mwenzetu aliyetangulia mbele ya haki.

Mhe. Naibu Spika, mimi nataka nije katika taarifa hii moja kwa moja katika maagizo Nam. 21, Kamati ilitaka Idara hii kuwasliana na Afisi ya Rais Ikulu ili kufuatilia ahadi zote za Mhe. Rais Majimboni na kutekeleza kwa lengo la kuondoa malalamiko. Lakini katika utekelezaji imesema kuwa agizo linafanyiwa kazi pamoja na kujumuisho maagizo aliyoyatoa Mhe. Rais katika ziara aliyoifanya hivi karibuni Agosti 2017 katika Wilaya zote 12 za Zanzibar ili kuandaa mpango kazi wa Utekelezaji wa maagizo hayo.

Mhe. Naibu Spika, mimi nilitaka Mhe. Waziri aje anipe ufafanuzi ahadi zipi za Rais ambazo zinatekelezwa lakini pia Mhe. Waziri anifafanulie kuhusu utekelezaji wa ahadi za Maraisi waliotangulia ambazo zilitolewa na Rais ambaye ilikuwa ni taasisi. Kwa hivyo nataka pia aje atwambie kuhusu ahadi hizo zilizotolewa na Maraisi waliopita. Upo umuhimu wa kutekelezwa ahadi hizo na ndiyo maana wakatoa katika utekelezaji wao, bado ipo haja na sisi kutufahamisha ahadi hizo ni zipi na kwa sababu tu sisi Wawakilishi bado tunaulizwa au wananchi waliotuchagua wana kumbukumbu wa zile ahadi zilizotolewa na Maraisi waliopita. Nilikuwa namuomba sana Mhe. Waziri aje anipa ufafanuzi.

Mhe. Naibu Spika, niende katika agizo jengine ambalo wamesema katika ukurasa wa 10. Kamati ilitoa agizo kuwa ilitaka Shirika la Bandari kushirikiana na TRA kutafuta mashine na kuweza kukagua mizigo kwa uhakika hapo Bandarini. Kwanza niwapongeze sana Wizara kwa sababu wamesema wameshaanza kununua na tayari hizo mashine kwa mwaka huu zinafanyiwa kazi.

Mhe. Naibu Spika, mimi nije katika hoja yangu kuhusiana na umuhimu wa kituo cha Afya Bandarini. Nikuwa naomba sana uwepo wa kituo cha afya ni muhimu katika Shirika na Bandari ili kukidhi vigezo vya Bandari vya kimataifa kwa hivyo hiyo ni muhimu sana kuwepo. Nilikuwa naomba kwa sababu athari mbali mbali zinatokezea pale bandarini kwa kukosekana vituo vya Afya vya uhakika. Kipo kituo cha Afya Bandarini lakini bado hakina vigezo, ndio maana nikasema kuwa lazima umuhimu uwepo na kwa vile hapa tayari walishirikiana na TRA, mimi ushauri wangu nilitaka kuwa washirikiane na Wizara ya Afya ili kuimarisha kile kituo pale Bandarini.

Mhe. Naibu Spika, kwa nini nasema hivyo,tumeona kwama katika nchi za wenzetu kwa mfano nchi kama Sierra leone, Liberia, Guinea, zimepata athari kubwa za kiuchumi kutokana na maradhi yale ya ebola. Katika ripoti ya dunia kuhusu athari hizo, tayari imeonesha kuwa nchi hizo tukianza la Liberia imegharamika kwa kiasi cha dola milioni 812 kwa mwaka 2015/17 na Sierra leone imegharamika karibu dola milioni 844 kwa sababu tu ya kutibu hayo maradhi ya Ebola pamoja na Guinea imetumia karibu dola bilioni 289 kwa mwaka 2015/17.

Mhe. Naibu Spika, hivyo basi ili na sisi nchi yetu iepukane na gharama hizo ambazo kama nchi za wenzetu wamezipata kutokana na kuingiliwa na maradhi kama hayo ya miripuko, basi nilikuwa naomba sana na kuishauri Wizara hii kama walivyoshirikiana na Shirika la Bandari na *TRA* kwa kutafuta hii mashine ya *X-ray* basi washirikiane na

Wizara ya Afya kwa kuimarisha kile kitu cha Afya cha Bandarini hasa kuwepo na madaktari, yawepo na magari ya kuchukulia wagonjwa na mambo yote yanayohusiana na afya kwa kuwanusuru yale maradhi ya mirupuko kwa wale wageni wetu wanaoingia kupitia bandarini. Nilikuwa naomba sana kuishauri Wizara hii wawe na mashirikiano katika kitengo hiki ili tuepukane na zile gharama kama walizozipata wenzetu katika hizo nchi nilizozitaja na Tumuombe Mwenyezi Mungu atuepushie hayo maradhi katika nchi yetu yasije yakaingia.

Mhe. Naibu Spika, mimi nilikuwa na hayo tu machache ambayo na mimi nimeona kidogo niikumbushe au niishauri Wizara hii. Lakini pia na lile suala ambalo nililiouliza kuhusiana na zile ahadi za Rais.

Mhe. Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi kuchangia jioni ya leo, lakini pia naunga mkono hoja iliyoletwa hapa mezani kwa asilimia mia, lakini pia nawapongeza watayarishaji wote wa hii ripoti waliyoileta hapa leo. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Mwanaasha Khamis mchangiaji wa mwisho atakuwa Mhe. Mussa Ali Mussa na baada ya hapo nitampa vile vile Mhe. Mohamed Ahmada Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi na baadaye atafuata Waziri mwenyewe, ahsante Mhe. Mussa karibu.

Mhe. Mussa Ali Mussa: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, nakushukuru na mimi na mzee wako kuniona na ukanipa alau dakika tano nichangie na mimi Ripoti hii ya Mawasiliano, Ujenzi na Usafirishaji.

Kwa kweli nataka nizungumzie ukurasa wa 25 umenifanya nisimame nichangie kwa sababu naona kuna jambo ambalo limeshatokea na halijakamilishwa sasa linakuja jengine kunakuja kuvunjiwa watu kwa barabara kongwe ya Chake Chake kwenda Wete barabara ambayo ina majumba mengi sana, ina mazao mengi ina na mikarafuu mengi, wakati barabara ya Ole, Kengeja mpaka leo watu hawajalipwa panapita usanii tu Julai, Juni, Oktoba, Disemba lakini watu majumba yao yameshavunjwa na hakuna mtu aliyelipwa na sasa kunataka kupita usanii barabara kongwe.

Jambo hilo lisije likafanyika wenzetu wa ujenzi wa barabara wajipange, waanze kuwalipa wananchi kwanza ndio waje wavunje majumba ya watu tumechoka kutukanwa mnatuharibia na siasa ikiwa hawana kumbukumbu nataka niwakumbushe. Kabla ya vyama vingi Zanzibar uchaguzi ukifanyika kwa nembo ya nyumba na jembe, sasa ukipata nembo ya nyumba ulikuwa na uhakika wa ushindi lakini angalia leo nyumba inavyodharauliwa hawa watu walivyo na hatari wanaweza kumvunja mtu nyumba yake bila kumtaarifu yeye wala Sheha wake wakaingia tu wakavunja, wakaa wanaburuza mawe tu, wanaburuza miembe, wanaburuza mihogo wakati Serikali inahimiza kilimo wanaweza wakang'oa hata ile mikarafuu yetu inayotupatia posho la kutuweka sisi hapa.

Sasa nawahadharisha na nawatahadharisha kuwa walipe wananchi kwanza tena waanze kuwalipa wale wa mwanzo waliowavunjia, Gando wamevunja hawajalipa, Ole Kengeja wamevunja hawajalipa, Mtambile, Mwambe wamevunja hawajalipa sasa wanataka

kuvunja Chake Chake kwenda Wete hatukuja hapa kuvunjiana majumba, wasijenge mpaka walipe kwanza, wakisha lipa majumba ya watu tena mara hii wawaite watu wapatane nao bwana nyumba yako tunataka kuivunja, thamani yake ni shilingi milioni 20,000,000 wasemaje aa niongezeni nipeni 30,000,000 wapatane naye mpaka wakubaliane nae ndio sheria inavyosema. Hata sheria ya dini mnapotaka kupatana mpatane ndiyo muuziane muandikiane, kuna watu bwana huko nyuma wameshawapa mikataba wala pesa hawajawapa wala hawana barabara hawana lolote.

Toka 2013 mpaka leo 2017 kesho 2018 hakuna barabara iliyotengenezwa huko Ole Kengeja na majumba yamevunjwa, misikiti imevyunjwa, miembe imeng'olewa, mihogo imeng'olewa, minazi imeng'olewa tunakwenda kumwambia nini Mwenyezi Mungu sisi. Wanakuja hapa hii ni Wizara ya usanii tumechoka usanii Wizara hii wengi wao nusu ni wasanii. Sasa kama wanafanya usanii wende kwa Maalim Rashid Wizara ya Habari na Michezo. *(Makofi)*

Kule ndiko kunakotakiwa usanii wasifanye usanii na mali za watu wanatuharibia siasa 2020 ni kesho tunataka kurudi kwa wananchi kwenda kuomba kura sasa mtu ushamvunjia nyumba yake atakakupa kura.

Sasa turudi kwenye meli nashangaa mimi kuambiwa meli ni ya kisasa viti ni vya kisasa lakini meli si ya kisasa, viti ni vya kisasa na kamba ya kuvungia meli pale ni ya kisasa.

Mhe. Nassor Salim Ali: Kuhusu kanuni Mheshimiwa.

Mhe. Naibu Spika: Kuhusu utaratibu.

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba asome kanuni ya 68 ambayo inasema kwamba mjumbe anaposema mambo yasifaa Mhe. Naibu Spika, nisome au utaniruhusu.

Mhe. Naibu Spika: Sema hilio jambo lisilofaa.

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Naibu Spika, mjumbe aliyepita amesema kwamba kuna lugha ambayo kaizungumza kama kuna usanii sasa, imani inavyonipa mimi na ninavyoamini Serikali hii haina usanii, Serikali hii iko makini na inafanya kazi kwa mujibu wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi, kwa hivyo ningemuomna Mheshimiwa afute kauli yake au aeleze usanii unatokana na nani, Mheshimiwa nakushukuru sana.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mussa futa maneno yako Serikali sio wasanii Serikali hii haifanyi usanii futa maneno hayo.

Mhe. Mussa Ali Mussa: Wizara ya Mawasiliano ndiyo inayofanya usanii, Rais hafanyi usanii, Rais wa Zanzibar ana huruma tena na wananchi wake anawapenda na ndio maana ameongeza mshahara kima kwa asilimia mia moja anambie jengine mjumbe. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mussa muda wako umekwisha kaa chini.

Mhe. Mussa Ali Mussa: Na kama anataka nimuombe radhi namuomba radhi hakuna tatizo lakini ninachotaka kuzungumzia ni meli au unanizuia meli si mpya. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mussa kaa chini muda wako umekwisha umeniomba dakika tano kwa hiyo umeshamaliza dakika zako tano. Tunaendelea sasa nimkaribishe Mhe. Mohamed Ahmada Naibu Waziri wa Ujenzi na Mawasiliano Mheshimiwa karibu.

Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika awali ya yote na mimi nichukuwe nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kujaalia kukutana hapa leo jioni hii tukiwa tunaipitia ripoti ya Kamati ya Ardhi na Mawasiliano ambayo imewasilishwa na Mhe. Waziri.

Vile vile nichukuwe nafasi hii kumshukuru Mhe. Rais, Makamu wa Pili wa Rais, Waziri wangu na Watendaji wa Wizara yetu wote kwani kusema la kweli Wizara hii kama walivyosema wengine ina umuhimu sana katika nchi yetu na Mhe. Rais katuamini katika kuifanya hii kazi na sisi tunachua ahadi tutaifanya hii kazi kwa uadilifu na insafu kubwa kabisa kwa sababu sote tunarejea kwa Mwenyezi Mungu na atatuuliza kwa kile ambacho tumekisimamia nini tumekifanyia.

Mhe. Naibu Spika, moja kwa moja niende katika kutoa mchango wangu kutokana na Wiara yetu hii katika maswali tofauti kama ulivyuosema wewe mwenyewe kwamba huu ni utaratibu mpya kabisa wa namna gani tunapopewa maagizo na Kamati zetu husika na sisi Wizara tunapotakiwa kuyatekeleza yale maagizo.

Mimi nishukuru sana Makamo Mwenyekiti ambaye aliwasilisha taarifa yake pale na kusema la kweli ametupongeza vile vile kwasababu katika maagizo yale 48 takribani maagizo yote tumeyafanyia kazi isipokuwa yake ambayo hatujayafanhyia kazi tutayotolea ufafanuzi hapa.

Kwa hivyo napenda kuchukua nafasi hii kuwaambia wajumbe wa Baraza la Wawakilishi sisi tunafanya kazi kwa imani kabisa na kwamba hatufanyi usanii na vile vile tunafanya kazi kuhakikisha kwamba yake majukumu yaliopewa wizara yetu kwa mujibu wa katiba basi tunatekeleza ipasavyo.

Kwa ufupi limeelezewa suala la *Airport* tumezunguza katika bajeti yetu iliyopita na ripoti hii imeelezea vile vile kuhusu suala hili na kusema la ukweli wanajua jitihada zinazofanyika hivi sasa na tuhakikishe wajumbe hili suala karibu tutaanza ujenzi wa ile *Airport*.

Uko ushauri umetolewa hapa na baadhi ya wajumbe kama vile Mhe. Simai kama vile *VIP* ile ni sehemu ndogo laini nataka kumuarifu tu kwamba ile *design* ambayo tayari imetengenezwa imefanyiwa ukarabati na baadaye kutoka watu milioni 1,200,000 mpaka baadaaye ule uwanja utakuwa unachukua abiria milioni 1,600,000. Kwa hiyo hizo ndio jitihada ambazo mshauri elekezi amezitoa na baadaye watengenezaji wa lile jengo la *Terminal II* wameamuwa kulifanyia kazi.

Yapo maswali yamezungumzwa kuhusu barabara tuna imani kabisa barabara zetu zilipopata mvua nyingi zilikuwa chakavu na ndio maana ikatokea zile athari lakini kama walivyowapongeza wajumbe UUB wamefanya kazi kubwa sana mimi ni shuhuda wa kazi zao wanazofanya nyote ni mashuhuda sehemu nyingi tushatia viraka barabara Jendele mpaka Unguja Ukuu tushaimaliza, Michenzani sasa hivi mnaona jitihada tunazozifanya, Saateni mnaona jitihada tunazozifanya, *Round about* zote ambazo sehemu zimeharibika mnaona jitihada tunazozifanya kwa hivyo watu wanasema mnyonge mnyongeni lakini haki yake mpeni.

Mhe. Naibu Spika, kama alivyosema Mkandarasi wa MECO katika barabara zile za Pemba yeye ndiye aliyeshinda ile tenda na akaanza kutengeneza zile barabara mbili barabara kutoka Wete mpaka Gando na Wete mpaka Konde, kwa hiyo barabara iliyobakia Wete - Chake bado ataendea kuwa yeye mkandarasi na tunakuwa na dhamana mwaka mmoja kuhakikisha zile barabara zinakuwa katika hali yake na iwapo kutokea tatizo lolote basi anawajibu wa kutengeneza zile sehemu. Kwa hiyo anaingia katika tenda kwa uthibitisho na baada ya kupata zabuni ya kushinda nina imani kuwa insafu imefanyika.

Amezungumzia Mwakilishi mmoja kuhusu kuwalipa fidia kwa utaratibu tuliokuwa nao hivi sasa hatuwezi kubomoa jengo la mtu yoyote mpaka tulipe fidia na sasa hivi kwa watathmini wako kule wanafanya tathimini ile barabara ya Chake hadi Wete ya zamani. Kwa hiyo tunahakikishia kama tulivyofanya barabara hizi nyengine kama ambazo karibuni mkandarasi atapatikana barabara kutoka Bububu mpaka Mkokotoni na barabara nyengine kuhakikisha kwamba tunalipa fidia baada ya kulipa fidia baada ya kulipa fidia ndio tunaenda kusafisha zile barabara.

Kuhusu madaraja yamezungumzwa daraja la Pondeani ni kweli lile daraja ni jembamba lakini lina uwezo kupitisha mzigo mpaka tani 15 na juzi tu nimetembea daraja lile na bado tuna nia kama tulivyosema 2017/2018 kutaka kulipananu daraja, tulikuwa tulipanaue mwaka huu lakini kutokana na dharura zilizotozea za maafa ya mvua tumeamua kuliweka mwakani na *Inshaallah* kwa uwezo wake Mwenyezi Mungu lile daraja tutalipanua tunajua ufinyu wake.

Wamezungumzia vile vile madaraja ya kaskazini kama ulivyosema madaraja yote yale ya kaskazini mengine ni finyu Donge tuna daraja zuri tuu yale yataingia ujenzi wa barabara hii ambayo hii sasa tunaitengeneza ambayo mkandarasi karibuni atajulika.

Tumezungumzia kuhusu suala la meli ya MV. Mapinduzi mimi nimepanda ni shuhuda nimeenda nayo mpaka Comoro ni meli mpya, ni meli ya kisasa kabisa ni meli ya kuaminika ni meli ambayo kusema la kweli zile hitilafu ndogo ndogo zimetokana kutokana na kwamba bandari yetu ilipokuja kupima imeonekana *High tag* na *Low tag* ile milango ya pembeni haifunguki, lakini tu kama utaratibu wa kuhakikisha kwamba milango ile mengine tunatengenezea utaratibu kwamba ifungukie ili baadae iweze kuchukua mpaka magari.

Wameeleza kwamba inaharibika ile meli katika kuanza kazi zake tokea Januari 2016 imeharibika mara mbili tu 2015 samahani imeharibika mara mbili, imeharibika mara

moja mwezi wa Juni kifaa kile kikapatikana kwa *dollar Euro* 3000 na karibuni imeharibika tena ni matengenezo ambayo yamekamilika baada aya kuja wataalamu kutoka nje, kwasababu kama nilivyosema mwanzo ni meli ya kisasa. Kwa hivyo nawaomba sana wajumbe watuamini na hivi sasa kwa mujibu wa Ilani yetu ya Uchaguzi tumeamua kutengeneza meli mbili, kuna mjumbe alisema kwanini tusiendelee kuifanyia matengenzo meli hii na hizo nyengine tusizifanyie tunapoahidi katika Ilani hya Uchaguzi lazima tutekeleze ahadi hiyo na ninawakikishia kwamba meli nyengine mbili za mafuta na abiria tutazitengeneza chini ya Uongozi mahiri wa Dkt. Ali Mohamed Shein kusema kwa ukweli tunamshukuru Rais wetu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa ushauri anatupa kila wakati.

Niende haraka haraka vile vile kuna suala limezungumziwa kuhusu nyumba tuna imani kubwa kabisa matengenezo ya nyumba tunaendelea kuyafanya juzi ilikuwa Pemba pale Madungu tunaona tunavyofanya ukarabati, hatua kwa hatua na kwa mujibu wa bajeti yetu tutaendele kuzitengeneza wamesema wengine kwamba pesa tunazozitumia kwamba tuzitumie kwa ungaalifu, tutazitumia kwa ungalifu na kuna wengine wanasema kodi tunayoitoa ni kodi kubwa sana.

Kusema la ukweli ile si kodi kubwa sana 50,000 kwa nyumba za Michenzani ni kodi ndogo sana. Mimi najua kwamba kuna watu wanazitaka zike nyumba kwa zaidi ya laki 200,000 na wako wengine ambao wamepewa nyumba kutokana na kulipwa fidia wanawapa watu na wanakodisha zaidi ya laki 200,000 kwa hiyo Serikali inajali wanyonge ndio maana tukaweka bei ambayo ni *reasonable* kabisa.

Mhe. Naibu Spika, nizungumze haraka haraka kuhusu uwanja wa ndege maeneo ya maegesho kweli kulikuwa na mkataba hapo mwanzo na Chui kampuni kutoka Kenya ambayo ilikuwa na Makao Makuu yake Dar es Salaam tulivunja mkataba nao kutokana kwamba walishindwa kukidhi vigezo tunavyovitaka, baada ya hapo ikaja kampuni ya *Royal* ambayo *Security* ambayo hawa tumeingia nao tenda kwa mujibu wa taratibu zote.

Mhe. Naibu Spika, haraka haraka napenda kuwambia wajumbe kwamba sisi tuna nia ya dhati kuhakikisha zile kero zote ambazo wajumbe wanakuwa wanatuandikia, wanatuambia tunataka kuzitatua.

Kuhusu bodaboda nimejibu hili suala mimi mpaka leo naendelea kusema kwamba mimi nitaendelea na Wizara na Serikali kuzifuata sheria. Sheria inasema kwamba tusiruhusu bodaboda na mimi sijawahi kusema hata siku moja kwamba tumeziruhusu bodaboda, bodaboda kwa mujibu wa sheria haziruhusiwi kukufanya kazi lakini sisi tutakaa na wadau wameshanifuata ofisi kwangu tushazungumza nao sana na baadae tutaangalia, ushauri wao tutauchukua na baadae utakuja katika Bodi ya Barabara na badaye utaakuja Wizarani na baadae tutapeleka Serikalini.

Wamesema kuhusu kanuni za papo papo tubakubaliana kwamba tuna utaratibu tunataka tuangalie tunapo *apply* kanuni hii isijekuwa athari yoyote kwa wananchi ikawa zaidi inachukuwa rushwa, kwa hivyo kila jambo tunalolifanya tunalifanya kwa umakini kabisa ili kuhakikisha kwamba hatukosei.

Mwisho kabisa nawashukuru sana Wajumbe waendelee kutuunga mkono na sisi tutakuwa nao moja kwa moja katika kuhakikisha kwamba nchi yetu hii tunaendelea katika ile ahadi tuliyoiweka yakipato cha kati kupitia dira ya maendeleo 2020, ahsanteni sana kwa kutusilikiza naunga mkono hoja Mhe. Naibu Spika. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Sasa nimpishe Mhe. Waziri wa Ujenzi na Mawasiliano.

Mhe. Waziri wa Ujenzi na Mawasiliano: Mhe. Niabu Spika, kwa ruhusa yako ningependa kuchukua fursa hii kuwashukuru tena kuwashukuru sana Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa kunisikiliza yale ambayo niliyoyaeleza na pia kwa kuchangia wengine kwa maandishi, wengine kwa maelezo.

Baada ya maelezo aliyoeleza Naibu Waziri wangu nahisi mimi sina zaidi ya kuengeza, yeye anapotamka katika baraza hili basi amini kwamba anatamka kwa niaba yangu na yote aliyoyasema sina la kuongeza wala sina la kupunguza. *(Makofi)*

Kwa hivyo niseme tu kwamba yote ambayo tunayoyazunguza hapa tutayafatilia mengi yaliyozungumzwa hapa kuna mambo ya kitaalamu kidogo nilitaka niyatolee ufanunuzi yale yaliyozungumzwa kwamba kuna sheria zinazosema kwamba waziri ndiye anayesimamia hizi sheria na kanuni hilo ni kweli lakini nilikuta kwamba mawaziri wenzangu ambao walitangulia walikwishatunga baadhi ya hizo sheria, lakini mimi natoa ahadi tuu nitakwenda kuziangalia tena. *(Makofi)*

Kwa sababu msitu ukiwa mpya na komba huwa wapya na hii 2015 tunaelekea 2020 msitu ule ule lakini komba wapya kwamba haya yote tutakwenda kuyafanyia kazi. *(Makofi)*

La pili la utaalamu ambalo limezingumzwa na Mhe. Mohamed Said Mohamed (Dimwa) hili nilitaka nilizungumzie kidogo kwamba katika katiba yetu ya Zanzibar kuna mihimili mitatu linatangulizwa muhimili wa utekelezaji ambao unaongozwa na Mhe. Rais na kwa sasa hivi tunaongozwa na Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein. *(Makofi)*

Kikatiba yeye ndio Waziri wa Wizara zote sisi tunakwenda pale ni wakala tuu tunakwenda pale wewe ukafanye kazi uloagizwa na mwenyewe Mhe. Rais Dkt. Ali Mohammed Shein. Hivi karibuni kuna kiongozi mmoja mkubwa sana wa nchi hii alinivuta pembeni akanishukuru sana kwamba unafanya kazi nzuri sana kutujenga njia, nikamwambia sita kidogo wewe una uwezo wa kwenda kumuona mwenyewe Rais siku ukipata nafasi nenda ukamshukuru yeye, maana yake yote tunayofanya haya ya ujenzi wa barabara ni mwenyewe Mhe. Rais, ukija katika mambo ya Mawasiliana na muongozo wake mwenyewe Mhe. Rais na usafirishaji agizo la kununua hizo meli linatoka kwa mwenyewe Mhe. Rais.

Kwamba yale yote miliyazungumza hapa mimi nitayachukua nikayapeleke kwa Mhe. Rais lakini zaidi nitakwenda kumshukru maana wengi mmemshukuru kwa uongozi wake na mimi nasema kwamba na sisi Kiwizara tutajitahidi tunavyoweza kufuata muuogozo wa Rais wetu Mhe. Dk. Ali Mohammed Shein. *(Makofi)*

Sasa hapo nilikuwa nimeona kwamba Kamati yenu imekuwa inatoa maagizo mara nyingi nilikuwa nazungumza na Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ile tulipokutana mimi na yeye tu tukazungumza mambo mengine kabla hatuja katika mazungumzo ya Wizara na kikao, tulikubaliana kwamba *executive branch* ya nchi yetu inayoongozwa na Rais akisaidiwa na Makamu wa Pili wa Rais hawa ndio watatoa muongozo wao wawe wanatupa ushauri maana katika kutoa muongozo kama hujatoa, unatoa muongozo tu bila ya kupeleka hizo pesa hiyo kazi itafanyika.

Sasa tunatengeza bajeti kwenye Baraza la Mapinduzi tunaileta kwenu mnaipitisha mkisha ipitisha basi tunayafanya yale ambayo tumekubaliana kama kuna haja yakutoa muongozo mwengine, nafikiri kwamba Mhe. Spika au Naibu Spika au yoyote anayehusika na kuendesha Baraza hili tukufu ende akamuone Mhe. Rais wakashauriane kule kwamba hizo fedha za ziada za kufanya kazi za ziada tukazitenge kutoka Wizara ya Fedha zikipatikana itafanyika hiyo kazi ya nyongeza ambayo tutapata maagizo kutoka kwenye kamati. Hilo niliona bora niliseme kwa sababu tusifike wakati tukawa tunatoa maamuzi tu kajenge hapa, fanya hiki, fanya kile tuna mahitaji ya kuweza kuzifanya hizi kazi na mahitaji hayo ni nguvu kazi pamoja na fedha hilo nilitaka nilijulishe tufahamiane vizuri.

Baada ya kusema hayo Mhe. Naibu Spika, naomba kwa heshima na taadhima kushukuru tena na pia kutoa hoja ahsante. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri waheshimiwa wajumbe Mhe. Waziri ameshatoa hoja ya kwamba taarifa ipokelewe wale wanaopokea taarifa hiyo wanyooshe mikono nawashukuru sana waheshimiwa wajumbe. *(Makofi)*

Waheshimiwa wajumbe na mimi niwashukuru sana kwa siku ya leo lakini nilikuwa kidogo na mimi nataka niwakumbushe waheshimiwa wajumbe kwa sababu bado tutakuwa tunaendelea na kujadili taarifa za utekelezaji nimeona mara nyingi sana watu wanatoka kwenye mstari. Kwa maana kwamba badala ya kujadili yale ambayo yaliyotakiwa kujadiliwa maagizo ya kamati watu wanatoka kwenye mstari wanazungumzia mambo mengine na hayo yatasababisha kwamba sijui baadae tutakapoanza kujadili wizara kwa wizara tutajadili vitu gani.

Sasa mimi nafiria kwamba Mhe. Wajumbe mnapozipitia hizi taarifa pamoja na taarifa za wenyeviti mhakikishe mnakwenda kwenye mstari ambao umekusudiwa mengine yana wakati wake, mengine ambayo tunayajadili hapa yana wakati wake.

Lakini jengine ambalo nilikuwa nataka kulizungumza waheshimiwa wajumbe lugha kuna lugha nyengine hazifai kuzungumzwa hata kama moja kwa moja hazimtusi mtu lakini sisi Wazanzibari tuna silka na mila zetu za kuzungumza, unapozungumza lugha ambayo itakuwa moja kwa moja mtu ataelewa unamu-*attack* au unai-*attack* Serikali mimi nafikiri turudi nyuma. Tujaribu kuona namna gani tutawasilisha hoja zetu ndani ya Baraza badala ya kutoa lugha ambayo kwa kweli italeta msuguwano baina ya Serikali na sisi Wawakilishi.

Niseme hayo kwa leo lakini niwashukuru sana kwa ushirikiano wenu pamoja na mijadala kwa utulivu wenu kabla ya kumalizia ya kuahirisha kikao ni kuwa nimepata maagizo

kutoka kwa Mnadhimu anaomba wana CCM wajumbe wawakilishi wa CCM wabakie humu baada yakuahirisha kikao hiki.

Baada ya kusema hayo naahirisha hiki kikao hadi kesho tukijaaliwa saaa 3:00 asubuhi.

(Saa 2:30 usiku Baraza liliahirishwa hadi tarehe 4/10/2017 saa 3:00 asubuhi)